SUPA JACKPOT
TZS.1,033,283,276
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3

**ACT- WAZALENDO yapinga azimio la EU bomba mafuta**


Ukurasa 16
MRADI NYUMBA WATUMISHI UMMA
Bosi Dk. Msemwa achanganua wanachokitoa, aliyeuziwa afunguka kilichomo maisha mapya

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 23, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Yaliyojificha tatizo watoto mtaani na ombaomba
Ukurasa 14

RUTO ATINGA KIKAONI UMOJA WA MATAIFA
**Ahutubia akizitaka Benki ya Dunia, IMF zisogeze muda kudai madeni**

anyiko mbaya wa migogoro , mabadiliko ya hali ya hewa na Covid-19,"anatamka Rais Ruto.

Pia, rais huyo anatoa wito kwa nchi nyinginezo kushirikiana na zinazoendelea, kusaidia kukabiliana na janga hilo akifafanua Kenya na nchi za Afrika zinazoendelea, zinahitaji ushirikiano wa kimataifa kukwepa shida za kiuchumi na kukwepa madhila hayo.

Anasisitiza hayo, wito huo ukizingatiwa utasaidia nchi za kipato cha kati kuanza ajenda zao za maendeleo na kuepusha mzozo wa kiuchumi.

Ni maaoni yanayojiri miezi michache, baada ya Hazina ya Kitaifa ya Kenya kuweka wazi deni la Kenya lilikuwa Sh.(za Kenya) trilioni 8.6 kwa mchanganuo, deni la nje Sh trilioni 4.1 na deni la ndani Sh trilioni 3.9.

Pia, katika hotuba yake akahimiza nchi tajiri duniani kupitia kundi lao la G20, kupanua mfu-

UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaa Septemba 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581077
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Utafiti wabaini usugu ARV kwa wajawazito



UKURASA 2

# Msukuma awavunja mbavu wabunge kwa Kiingereza

UKURASA 2


Angela Kizigha (CCM)


Ansar Kachwamba (CCM)


Dk. Abdulla Makame (CCM)


Dk. Ng'waru Maghembe (CCM)


Dk. Shongo Mlozi (CCM)


James Millya (CCM)


Machano Machano (CCM)


Mashaka Ngole (CUF)


Nadra Mohamed (CCM)


Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Kasheku 'Msukuma'

UKURASA WA 4

## KAMPUNI SIMU YAELEZA MAGUMU YA TOZO

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom, imeeleza magumu iliyopitia kutokana na kuanzishwa kwa tozo za miamala ya kielektroniki ikiwamo kupungua kwa wateja wa M-Pesa na kusababisha kushuka kwa mapato. Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo...

# Mtuhumiwa wa utapeli afariki chini ya ulinzi akipata tiba

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAYELE AFUNGUKA WATASONGA MBELE** UK.32

**KABWELA** UK. 7

# Kiingereza cha Msukuma kilivyo wavunja mbavu Wabunge

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Kasheku 'Msukuma' jana 'aliwavunja mbavu' wabunge bungeni wakati akimuuliza swali kwa lugha ya Kiingereza mgombea wa ubunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Habib Mnyaa wa Chama cha Wananchi (CUF).

Msukuma ambaye ni mhitimu wa elimu ya darasa la saba, aliyewahi kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa (PhD) katika masuala ya jamii, jana alionyesha umahiri wake wa kuzungumza lugha hiyo, baada ya kumuuliza swali mgombea huyo wa EALA kwa Kiingereza ambacho hakijanyooka, hali iliyozua kicheko bungeni.

**ILIVYOKUWA**

Wakati wa kipindi cha kuwahoji wagombea hao wa EALA ulipowadia, Msukuma alinyoosha mkono na kumuuliza Mnyaa.

Msukuma: "I want to ask one question (nataka kukuuliza swali moja)... Where are you? (uko wapi?)...What do you do? (unafanya nini?).... What did you do for last five years? (ulifanya nini ndani ya miaka mitano?)....

Hatua ya Msukuma kuuliza swali hilo wabunge waliangua kicheko huku wakishangilia.

Baada ya swali hilo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, alimuuliza Mnyaa kama amelielewa swali la Msukuma...'I think you have heard his question (nafikiri umelisikia swali lake)...Okay, honourable members, please hold on (sawa, waheshimiwa wabunge sikilizeni kwanza).... Honourable Mnyaa, did you hear his question? (Mheshimiwa Mnyaa umelisikia swali lake?) Kutokana na swali hilo la Msukuma, Spika Dk. Tulia aliingilia kati na kusema, "I will help you (nitakusaidia). He is asking what did you do for the past five years, that's his question.

(Anauliza umefanya nini ndani ya miaka mitano iliyopita). Hata hivyo, wakati Spika Tulia akifafanua swali la Msukuma, wabunge waliendelea kuangua vicheko na kujadili namna Msukuma alivyouliza.

Spika Tulia aliendelea kumuuliza Mnyaa: "...You are still showing signs ... (Bado unaonyesha dalili kwamba hujaelewa swali lake) Did you hear me? (umenisikia?) Members of Parliament let's give him a chance to respond (waheshimiwa wabunge tumpe nafasi ajibu).

Baada ya Spika Dk. Tulia kunyoosha maelezo yaliyotolewa na Msukuma kwa lugha ya Kiingereza, Mbunge huyo wa Geita Vijijini alianza kuzurura ndani ya Bunge, akitunzwa noti za Sh. 10,000 na baadhi ya wabunge, waliokoshwa na uulizaji swali lake kwa Kiingereza.

**MATOKEO UCHAGUZI**

Bunge liliingia katika hatua ya uchaguzi wa Wabunge wa EALA, katika matokeo hayo, vigogo wawili wa vyama vya siasa vyenye wabunge walio wachache bungeni, Ado Shaibu (ACT-Wazalendo) na mwanasiasa mkongwe nchini, Habibu Mnyaa (CUF), walishindwa kupenya katika uchaguzi huo, licha ya kupewa nafasi kubwa ya kushinda kiti hicho.

Ado, ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, aliangushwa katika kinyang'anyiro hicho na Mwanasheria, Mashaka Ngole (CUF), aliyepata kura za kishindo 234.

Wakati Mnyaa aliyekuwa akipambana kutetea nafasi hiyo kwa mara ya pili mfululizo, aliangushwa na Dk. Abdulah Makame (CCM), aliyepata kura 305 katika kundi la wagombea wa Zanzibar.

Akitangaza matokeo hayo, Spika Dk. Tulia, aliwataja waliong'ara katika uchaguzi huo kutoka wagombea wanawake kuwa ni Angela Kiziga (CCM) aliyepata kura 322, Shogo Mlozi (CCM) kura 322 na Nadra Mohamed (CCM) aliyepata kura 310.

Katika kundi la wagombea wa Zanzibar, walioshinda ni Dk. Abdulah Makame (CCM) kura 305 na Machano Machano (CCM), kura 291. Aidha, Spika alimtaja aliyeng'ara katika kundi la wagombea wa vyama vya siasa walio wachache bungeni ni Mashaka Ngole (CUF).

Wengine waliong'ara katika kundi la wagombea wanaume Bara ni Ansar Kachwamba (CCM) kura 300, James Ole Millya (CCM) 312 na Dk. Ng'waru Maghembe (CCM) 311.




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan (kulia) na Mwenyekiti wa EEPC India, Mahesh Desai (kushoto), wakikata utepe kuzindua maonyesho ya 23 ya AutoExpo Afrika 2022, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utafiti wabaini usugu ARV kwa wajawazito

**Na Beatrice Shayo**

UTAFITI umegundua dawa zinazotumiwa na wajawazito wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU), kujenga usugu kwa kiwango kikubwa na kuchangia kuongezeka kwa maambukizi ya virusi hivyo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Matokeo ya utafiti huo uliofanyika katika mikoa 19 nchini umeonyesha dawa hizo zimejenga usugu kwa asilimia 27.5 kwa kinamama waliogundulika na maambukizi wakati wa ujauzito, ambao hawajaanza kutumia dawa na asilimia 79.2 kwa ambao tayari wapo kwenye matumizi ya Dawa za Kufubaza Makali (ARV).

Taarifa ya utafiti huo ilitolewa jana mkoani Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH), Dk. David Sando, wakati akiwasilisha matokeo matatu ya utafiti uliofanywa nchini kuangalia udhibiti wa mlipuko, kinga na tiba ya VVU wakati wa ujauzito na kunyonyesha.

Dk. Sando alisema licha ya kuwapo kwa huduma nyingi za kliniki zinazosaidia nchini kwa asilimia 93 bado maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ni makubwa kwa asilimia 11. "Usugu wa dawa za VVU ni tishio moja zaidi kwa ufanisi wa ARV. Taarifa kuhusu usugu wa dawa zinapatikana, lakini hazijumuishi wajawazito wanaoishi na VVU.

"Taarifa hii ni muhimu katika kufahamisha watunga sera ili kuongeza uboreshaji wa huduma za matunzo kwa kundi hili," alisema Dk. Sando.

**UTAFITI ULISHIRIKISHA TAASISI MAREKANI**

Alisema utafiti huo walishirikiana na taasisi ya Kimarekani, washirika na wadau wengine hapa nchini, ambao ulilenga wajawazito waliojifungua wakiangalia huduma za kuzuia maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa watoto inafanya kazi kwa kiasi gani.

Pia, waliangalia usugu wa dawa kwa kinamama wanaoanza kutumia dawa wakiwa wajawazito.

"Tafiti hizi kubwa mbili zimeona afua zilizopo hapa nchini zimeweza kuzuia maambukizi na zinaendelea kusaidia kuzuia maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa kinamama kwenda kwa watoto, kinamama ambao wameanza kliniki wakiwa na maambukizi ya VVU na kuanzishiwa dawa," alifafanua.

Alisema kwa utafiti waliofanya kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kinamama chini ya asilimia mbili wanapeleka maambukizi kwa watoto wao. Dk. Sando alisema: "Usugu wa dawa hizi ambazo tunatumia kwa ajili ya kufubisha makali ya ugonjwa huu wa UKIMWI ni jambo la kawaida kuangalia kujua je? Usugu upo kwa kiasi gani. Kadri usugu unapokuwa mkubwa hizo dawa zinabidi kuondolewa kwenye tiba zilizopo."

**USHAURI**

Alisema suala hilo linashauriwa kimataifa kwamba wakifikia kwenye kiwango cha usugu wa asilimia 10 katika wagonjwa 10, mgonjwa mmoja anawafikia akiwa na virusi ambavyo tayari vina usugu nchi inashauriwa kubadilisha dawa ili kutumia ambayo haina usugu.

Alisema suala hilo ni utaratibu wa kawaida na kwa sasa wanafanya utafiti wa nchi nzima kuangalia usugu wa dawa una ukubwa kiasi gani kwa wajawazito ambao wana Virusi vya Ukimwi.

"Dawa bado hazijafika kwenye usugu wa asilimia 10, lakini kuna dawa ambazo zimeonekana kuwa na usugu wa hali ya juu na ni hatarishi tunakokwenda huko mbele. Tunatakiwa kuja na afua za kuhakikisha kwamba tunapunguza ile kasi ya kuenea kwa virusi vyenye usugu ili isifike wakati tukashindwa kuwa na dawa ambazo zinaweza kusaidia kufubisha ugonjwa huu," alisisitiza.

Vile vile, alisema huo ndiyo msingi wa kuwapo kwa kongamano lao kuona ni namna gani serikali na wadau wote nchini wanaendelea kuboresha huduma ili kuepukana na majanga ambayo yanaweza kuepukana na usugu wa dawa na kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa watoto wanaozaliwa na kinamama wenye maambukizi ya virusi hivyo.

Dk. Sando alisema Tanzania imewekea lengo ifikapo mwaka 2030 hakuna mama atakayemuambukiza mtoto wake ugonjwa wa UKIMWI na nguvu kubwa wanayoiweka ni kuhakikisha serikali inafikia malengo hayo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema mkutano unalenga kumaliza ama kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa kuangalia namna ya kukabiliana na usugu wa virusi vya ugonjwa huo kwa dawa hasa kwa wajawazito na wanaonyonyesha.

Alisema wataalamu wamefanya utafiti katika eneo hilo na kikubwa walichokiona kumekuwa na mafanikio makubwa kama nchi.

"Kitaifa tumepiga hatua asilimia 95 ya watu kutambua hali zao za maambukizi tuna ufanisi wa asilimia zaidi ya 90, hili ni jambo jema na la pili kuhusu upatikanaji wa dawa ukoje na wangapi wameingia kwenye dawa. Tumevuka lengo zaidi ya asilimia 99 na hizi ni taarifa za Julai za mwaka huu," alisema Dk. Mfaume.

**WATU MILIONI 1.7 WANAISHI NA VVU**

Dk. Mfaume alisema serikali imejipanga kuwasaidia wananchi wenye maambukizi ya VVU waanze dawa, inakadiriwa zaidi ya watu milioni 1.7 wanaishi na maambukizi na wanaotumia dawa ni milioni 1.5 (asilimia 88).

Alisema wanatakiwa kuongeza jitihada zaidi za kuhakikisha kuwa watu ambao hawatambui hali zao za maambukizi wanawekwa katika dawa ili kuzuia maambukizi kwenda kwa wengine.

Aidha, alisema dawa hizo zisipotumika vizuri zinaweza kuleta usugu kwa Virusi vya ugonjwa wa UKIMWI na utafiti umewaonyesha.

Dk. Mfaume alisema watafanya suala hilo kwa ushahidi wa utafiti na wamepokea ripoti hiyo na wataenda kuangalia maeneo ambayo yamependekezwa.

Alisema watafiti wamewaeleza na kwa sasa kinachofanyika ni kupata takwimu sahihi ya hali ya usugu.

HABARI KITAIFA

# ACT-Wazalendo yapinga azimio la EU

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimepinga tamko lililotolewa na Azimio la Bunge la Ulaya la kutaka kusitishwa kwa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa madai kuwa utekelezaji wake utaharibu baioanuai (viumbe hai).

Alhamisi iliyopita, Bunge la Ulaya lilitoa kauli kuwa mradi huo utaharibu baioanuai na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Sekta ya Madini, ACT- Wazalendo, Isihaka Mchinjita, madai hayo ni juhudi za kuzuia uanzishwaji wa kiwanda cha kusafisha mafuta na kutoa shinikizo

kwa wawekezaji watarajiwa kusitisha uamuzi wa mwisho wa kuwekeza kwenye mradi huo.

"Tunalaani maazimio yasiyokubalika ya Bunge la Ulaya kwa sababu yanatishia kuingilia mambo ya ndani ya nchi za Uganda na Tanzania. Huu ni ukiukaji wa wazi wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

"Vitendo hivi vinavyofanywa na Umoja wa Ulaya vinakiuka misingi ya sheria za kimataifa na haki isiyoweza kuondolewa ya watu wa Uganda na Tanzania ya kujiamulia mustakabali wao na mamlaka ya kujitawala, vinapaswa kulaaniwa vikali na kupingwa kwa nguvu zote na wadau wote ndani na nje nchi," alisema.

Alisema ACT-Wazalendo inatambua na kuthamini hatua na juhudi zinazofanywa na wanaharakati wa mazingira, watetezi wa haki za binadamu na asasi zingine za kiraia (AZAKI) za ndani ya nchi zote mbili katika kuzitahadharisha na kuziwajibisha serikali hizo, kuzingatia athari za mazingira na kujali haki za binadamu.

Taarifa hiyo ilisema juhudi za wanaharakati na wadau wa ndani hazipaswi kulenga kusitishwa kwa mradi, badala yake kutoa tahadhari ili kupunguza athari zitakazotokana na utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta.

"Ni ukweli wa kihistoria kwamba ikiwa maazimio ya Bunge la Ulaya hayatapingwa vikali katika siku za usoni, yataweka kielelezo kwa chombo hicho kuingilia na kurudisha nyuma mipango yoyote kwa nchi za kiafrika kutumia rasilimali zao katika kujiletea maendeleo yao wenyewe," alisema.

Chama hicho kimetoa wito wa watu wa Afrika kuungana ili kuzuia kutimizwa kwa fikra hizo na kulinda uwezo wa kujiamulia na uhuru wa bara.

Kadhalika, chama hicho kimelitaka Bunge la Afrika Mashariki (EALA) litoe azimio la kulinda uhuru wa Tanzania na Uganda kujiamulia mambo yao na kutaka mazungumzo na wabunge wa Bunge la Ulaya. Pia kimelitaka Bunge la Ulaya kuondoa azimio lake dhidi ya mradi huo.

# Mtuhumiwa utapeli afariki akitibiwa chini ya uangalizi

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

ALIYEDAIWA kujifanya mfanyakazi wa mahakama, Andrea Magembe, amefariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi, baada ya kuanguka ghafla.

Magembe alipelekwa hospitalini hapo kwa ajili ya kupatiwa huduma ya kwanza baada ya kuwekwa chini ya ulinzi katika kiwanda cha vipodozi cha Radiant, Kongowe wilayani Kibaha.

Magembe akiwa na mwenzake, Michael Gerald, anadaiwa kufika katika kiwanda hicho wakijifanya watumishi wa Idara ya Mahakama wakiwa na barua feki ya kuomba mchango kwa madai ya kufiwa na mtumishi mwenzao.

Kamanda wa Mkoa wa Polisi Pwani, Pius Lutumo, aliwaambia waandishi wa habari jana ofisini kwake mjini hapa kuwa watuhumiwa hao walibainika kuwa matapeli na kuwekwa chini ya ulinzi na walinzi wa kiwanda hicho hadi polisi walipofika.

Lutumo alisema baada ya kupata taarifa, polisi walifika katika eneo hilo na kuwakuta watuhumiwa hao na Magembe anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 40 na 45, alikutwa amelala chini akitokwa na povu mdomoni.

"Baada ya watuhumiwa wote wawili kuchukuliwa na polisi, Magembe alifikishwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi ambako alifariki akiwa anapatiwa matibabu," alisema.

Kamanda alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Tumbi kwa uchunguzi wa madaktari.

Kuhusu Gerald, mkazi wa Kigamboni, Da es Salaam, bado anashikiliwa na polisi na baada ya upelelezi, atafikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Kamanda Lutumo, uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa watuhumiwa hao walishafanya matukio ya utapeli na udanganyifu katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro.

Katika tukio lingine, mtoto Salum Sadiki (3) mkazi wa kijiji cha Manerumango Kaskazini, Wilaya ya Kisarawe, amefariki dunia kwa kuzama kwenye kisima cha maji.

Kamanda Lutumo alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 4:00 asubuhi katika Kijiji cha Manerumango akiwa na mwenzake wakicheza pembezoni mwa kisima chenye urefu wa futi 12 ambacho alitumbukia na kisha kuzama.



CGIAR IRRI

POSITION ANNOUNCEMENT

Senior Scientist I - Cropping Systems Agronomy / Climate Change

Job ID : HQ01399
Location Duty station : Tanzania, Dar es Salaam
Closing Date : 12-Oct-2022

Apply

https://www.irri.org/jobs

**About IRRI**
The International Rice Research Institute (IRRI) is dedicated to reducing poverty and hunger through rice science; improving the health and welfare of rice farmers and consumers; and protecting the rice-growing environment for future generations. IRRI is an independent, nonprofit, research and educational institute, founded in 1960 by the Ford and Rockefeller foundations with support from the Philippine government. The institute, headquartered in Los Baños, Philippines, has offices in 17 rice-growing countries in Asia and Africa, and over 1,000 staff.

Working with in-country partners, IRRI develops advanced rice varieties that yield more grain and better withstand pests and disease as well as flooding, drought, and other harmful effects of climate change.

**Job Purpose**
Climate Change impacts rice production through exacerbated and more frequent climate extremes, rising sea levels and temperatures. Understanding future trends is crucial to plan ahead and implement adaptation options to increase resilience of agricultural systems. Working with various national and international partners in different projects, IRRI develops strategies to mitigate climate change (effects) and to adapt to climate change, e.g., through the development and dissemination of climate-smart technologies in rice production.

The Sustainable Impact through Rice-based cropping Systems (SIRS) Platform aims at developing and promoting climate-smart, nature-friendly rice-based farming systems and value chains. Within the platform, the research unit Adaptive Agronomy and Pest Ecology deals specifically with cropping systems analysis, agronomy 'at large', soil science, and pest ecology and management. Within this unit, a research position is open in the field of 'cropping systems agronomy and climate change' (see 'purpose' below), which will be part of a multi-disciplinary team of scientists to optimize production and address climate change challenges.

**This position will be based in Tanzania and is open for international applications.**

**Roles and Responsibilities**
- Develop novel, sustainable and climate-smart (mitigation or adaptation) management practices and farming systems in rice-based, rainfed and irrigated ecologies in Africa that boost and sustain production and income. This may involve the shift from transplanting to direct seeding, novel mechanization options, introduction of new stress-tolerant varieties and associated management practices, novel diversified farming systems, etc.
- Develop of dissemination, scaling and partnership approaches (including digital tools), and/or business models for above-mentioed systems that will lead to impact 'at scale', such as improved resilience to climatic change and climatic shocks, improved food security, and reduced poverty
- Develop and lead (scientific and managerial) of a strong multidisciplinary R4D team on climate- smart agriculture at IRRI in Africa that will execute a well-defined 'climate-smart agriculture' R&D program
- Resource mobilization to support the above-mentioned R4D program.
- Contribute to developing strategic partnerships, knowledge sharing, and capacity development of various stakeholders
- Nurture and initiate collaboration with NARES partners, private sector and development partners, advanced research institutions (ARI) and policymakers in East and South Africa and conduct joint research
- Collaborate with governments, donors, rice R&D partners, and private enterprises to align with client and donor expectations; across CGIAR initiatives and other IRRI projects
- Communicate key messages and project progress with donors, policymakers, and other primary stakeholders
- Coordinate closely with project partners and build a relationship with other stakeholders to ensure research outputs are transferred effectively
- Develop new projects together with IRRI colleagues, ARIs, and NARES in Africa
- Supervise, and mentor junior staff
- Demonstrate scientific leadership through publications and representing IRRI in scientific and strategy forums
- World-class R4D agenda on development and delivery of climate-smart cropping and farming systems in rice-based ecologies in Africa;
- Novel climate-smart cropping and farming systems
- Effective scaling approaches, business models, and partnerships with public and private sector parties, including leading R&D entities (ARIs) in the region
- Articles in peer-reviewed journals, proceedings, technical manuals, and training materials that highlight findings from research activities, showcasing the incumbent's scientific leadership
- An effective resource mobilization strategy and a well-funded portfolio of R4D projects
- A well-functioning and effective R4D team based on principles of mutual trust and respect for gender and inclusion

**Qualifications**
- PhD in agronomy, cropping systems analysis, soil science, climate change, or related fields with at least 4+ years post-PhD

**Skills Required**

**Mandatory**
- Strong background in field oriented research and extension activities
- Have a mix of practical field skills, quantitative abilities; appreciation of interdisciplinary work, and a core commitment to achieving science-led agricultural development
- Excellent interpersonal and organizational skills
- Strong proficiency in written and spoken English

**Preferred**
- Experience with rice; work experience in a developing country environment

**IRRI offers a highly extensive employee benefits package inclusive of globally-covered medical insurance, retirement plan, life and accident insurance and other allowances. Join our team and be part of our story!**

***Please note only shortlisted candidates will be contacted.***

**This position will remain open until filled.**

217058602

# Kampuni simu yaeleza magumu ya tozo

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom, imeleza magumu iliyopitia kutokana na kuanzishwa kwa tozo za miamala ya kielektroniki ikiwamo kupungua kwa wateja wa M-Pesa na kusababisha kushuka kwa mapato.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, alisema hayo jijini Dar es Salaam jana alipokuwa akielezea athari za tozo kwa mapato ya kampuni hiyo.

"Kampuni iliripoti mapato ya huduma ya Sh. billion 956.5 ambayo yameshuka kwa asilimia 1.0 ikilinganishwa na mapato ya mwaka uliopita. Kwa kiasi kikubwa imeathiriwa na upotevu wa mapato ya Sh billion 103.8 yaliyotokana na tozo kwenye miamala ya simu kuanzia Julai, 2021," alisema.

Viashiria vingine vilivyoripotiwa ni mapato ya M-Pesa ya Sh billion 329.5 yakiwa yamepungua kwa asilimia 7.6 ikilinganishwa na Sh. billion 356.8 iliyopatikana katika mwaka wa fedha uliopita.

Hata hivyo, alisema jambo la kutia moyo ni mapato ya data ya simu (intaneti) yaliongezeka kwa asilimia 18.9 na kufikia Sh. billion 204.0

Pia, alisifia kitendo cha serikali kupunguza tozo akibainisha kuwa kitendo hicho kimeleta ahueni na kurejesha ari ya upatikanaji wa mapato.

"Wakati athari za tozo kwenye mapato ya jumla ni vigumu kuzifuta, tunatiwa moyo na serikali kuhusiana na suala hili. Septemba, 2021 tozo zilipungua kwa asilimia 30 na baadaye zikapunguzwa tena kwa asilimia 43 kuanzia Julai Mosi, 2022 na kusababisha punguzo la asilimia 60 tangu kuanzishwa kwa tozo

"Pamoja na hayo yote, Vodacom imedumisha nafasi yake ya uongozi katika soko nchini (market share) na maoni ya kuridhia kwa wateja wa kutumia kipimo kwa zana," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Hilda Bijiku, alisema pamoja na kuwapo kwa shinikizo la mapato, mafanikio ya utekelezaji wa mkakati wa kampuni hiyo umeendelea kuleta matokeo chanya katika maeneo mengine muhimu.

"Mapato yetu ya data za simu yaliongezeka kwa asilimia 18.9 ambayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za data kwa kila mteja. Yaliongezeka kwa asilimia 22.3 kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya simu janja pamoja na uwekezaji endelevu katika mtandao wetu, watumiaji hao waliongezeka kwa asilimia 12.1 hadi kufikia watumiaji Milioni 4.1 wakiwakilisha ongezeko la asilimia 54.2 ya wateja wa data," alisema.

Pia alisema, mwaka huu wameboresha ya M-Mama ambayo inalenga kupunguza vifo vya wajawazito kupitia utoaji wa huduma za usafiri wa dharula kwa wajawazito na watoto wachanga hadi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo ya vijijini.

Vilevile, alitangaza kutokuwapo kwa gawio mwaka huu akidai kuwa kampuni hiyo ilipata hasara iliyochangiwa na shinikizo la mapato.

# Mbarawa aagiza wahandisi wasiofuata sheria kufutwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, ameiagiza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kuwafutia usajili wahandisi wanaokwenda kinyume cha taratibu za taaluma hiyo.

Pia amewataka wahandisi kujiepusha na suala la vitendo vya rushwa na badala yake wafanye kazi kwa bidii ili kulisaidia taifa.

Alitoa maagizo hayo jana mkoani Dodoma, wakati akifungua mkutano wa 19 wa Siku ya Wahandisi (AED) sambamba na maonyesho ya kazi zilizofanywa na wahandisi.

Prof. Mbarawa alisema, hakuna sababu ya kuwaacha wahandisi wanaokwenda kinyume cha maadili na taratibu za kazi ndiyo maana wanakula kiapo kabla ya kuanza kazi ya taaluma hiyo.

"Naomba ERB mwendelee na suala la kuangalia nidhamu ya kazi kwa wahandisi wote. Nawapongeza kwa hatua mliyochukua kwa wahandisi walioKiuka utekelezaji wa kazi, wanaoshindwa waende kufanya kazi nyingine," alisema.

Prof. Mbarawa alisema, kuna miradi mingi ya maendeleo ambayo inatekelezwa nchini, hivyo wahandisi wanapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuendeleza miradi hiyo ya maendeleo ambayo inafaida kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Sambamba na hilo, aliwataka wahandisi kujiunga katika vikundi ili kuwasaidia kupata kazi za miradi mikubwa ikiwamo kuhimili ushindani uliopo kwenye sekta ya ujenzi.

"Naomba mjenge tabia ya kufanya kazi kwa kuungana bila hivyo itawawia vigumu kupata utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo," alisema Mbarawa.

Pia aliitaka ERB kuhimiza wanawake katika fani hiyo, kwa sababu wanawake ni watu wenye weledi hivyo wakiwa wengi watasaidia kuipeleka mbele fani ya uhandisi.

Kuhusu rushwa, Prof. Mbarawa alisema, wahandisi wanapaswa kuepuka kuchukua rushwa badala yake wafanye kazi kwa bidii ili kuendeleleza miradi ya maendeleo.

Alisema, wakiendekeza rushwa watashindwa kutekeleza miradi ya maendeleo na kulirudisha nyuma taifa katika maendeleo.

TANGAZO


Dodsal

Makao Makuu: Dubai, UAE mail@dodsaldxb.ae

# Dodsal Hydrocarbons & Power Tanzania

## Mafuta & Gesi

Dodsal imefanya utafiti katika eneo la Ruvu, kubaini ujazo wa mafuta futi za ujazo trilioni **2.9 cubic,** Pamoja na ujazo wa gesi cubic futi trilioni 4

## Sekta ya madini

Dodsal imeingia mkataba wa uchimbaji madini Itingi (Karibu na Ziwa Malawi) na kubaini latiri **60,000** za dhahabu, zingine zaidi ya latiri **300,000**

## Uhandisi & ujenzi

Dodsal kwa muongo uliopita imefanya miradi yenye thamani ya Dola za Marekani **bilioni 11** katika nchi zaidi ya nane kwenye sekta ya nishati, vituo vya kuzalisha nyuklia **kilometa 20,000** za miradi mitano ya gesi asilia inayoendelea katika nchi mbalimbali.

## Afya, usalama, mazingira

Dodsal imeweza kupewa tuzo zaidi ya **170** kutoka kwa wateja wake duniani kuanzia Algeria hadi Indonesia.

## Utoaji wa huduma za kijamii

Dodsal imefanikiwa kutoa msaada katika jamii zaidi ya Dola za Marekani **milioni 180**, kusaidia utafiti katika magonjwa yanayoambukiza, elimu ya afya pamoja na sanaa.

**Tunawatakia kila la kheri Africa katika Mkutano wa Nishati wa Houston.**

217057802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wauzaji mbegu dumavu vifaranga vya kuku washughulikiwe

**HABARI** kuhusu wafugaji wa kuku kulia kwa kuuziwa vifaranga vilivyodumaa, hazifurahishi na inaua soko la kuku nchini.

Hivi karibuni kulikuwa na kilio cha upungufu wa kuku katika masoko mengi jijini Dar es Salaam, na sababu ikielezwa kuwa kumekuwa na upungufu mkubwa wa soko la vifaranga.

Baadhi ya wafanyabiashara kwenye sekta hiyo wanatumia mwanya huo kuwauzia wafugaji vifaranga ambavyo ni dumavu na kuingia hasara kubwa kutokana na kutumia muda mrefu kuvikuza na gharama ya chakula.

Vifaranga vya kuku vinavyolalamikiwa ni vya kuku wa nyama ambao wana soko kubwa nchini, hasa jijini Dar es Salaam.

Ukiangalia katika migahawa, wauza chips, wanaojishughulisha na upishi wa vyakula kwenye sherehe na hotelini kuku wa nyama ni bidhaa muhimu na pengine ndiyo kitoweo rahisi kukipata.

Inapotokea bidhaa hiyo kuadimika inaathiri sio wafugaji pekee bali hata wafanyabiashara wa sekta tajwa.

Baadhi ya wafugaji wanalalamika kuwa wamekuwa wakipata hasara na kukatishwa tamaa ya kuendelea na biashara hiyo kutokana na udanganyifu unaofanywa na watu wachache wanaojipatia pesa kwa njia isiyo halali.

Wafugaji hao wanachosema ni kuwa wanapouziwa vifaranga hivyo ni vigumu kubaini kama ni dumavu mpaka muda wa kuuza unapowadia, ndipo hubaini kuwa havikui kama ilivyo kawaida kwa vifaranga walivyozoea kuvinunua.

Hali hii haiwaumizi wafugaji pekee bali hata walaji wa kitoweo hicho, kwani wamekuwa wakilalamika kuku wanaouziwa ni wadogo kama ndege.

Kwa kweli soko hili la kuku linapohujumiwa, linaathiri watu wengi ambao hutegemea vipato vyao kupitia ufugaji wa kuku.

Ukiangalia wajasiriamali wengi wanaoanza kufanya biashara huanzia kwenye ufugaji kuku na wengi wao ni kinamama.

Ufugaji kuku umewasaidia kuendeleza familia zao kwa kuwasomesha watoto, kuzalisha biashara nyingine na kujenga nyumba bora na za kisasa.

Ukosefu wa ajira nchini, kwa kiasi fulani umepata ufumbuzi kwa watu kujiajiri wenyewe kupitia ufugaji, ukiwamo wa kuku.

Kwa hiyo sekta hiyo inapohujumiwa kweli inaathiri watu wengi sana na wanapokosa shughuli nyingine ya kufanya serikali pia inaathirika.

Kutokana na kilio hicho, tunashukuru serikali imekisikia na kuahidi kufuatilia kwa kuchukua hatua kwa wote wanaohusika na udanganyifu huo.

Pia serikali imekiri kuna mbegu dumavu za vifaranga mbavyo havikui kwa wakati. Hata hivyo imefafanua kuwa wakati mwingine ni matunzo na chakula cha mfugaji mwenyewe kinaweza kusababisha kuku wasikue kwa wakati.


Ufafanuzi huo ni sahihi kabisa, lakini kuna haja ya kutolewa kwa elimu itakayowaelewesha wafugaji kutambua kipi chakula kinachofaa na kipi kisicho faa kwa sababu wengine hawana elimu hiyo.

Na pia kuna baadhi ya watu wanaotumia fursa ya ufugaji kwa kutambua kuwa kuna mahitaji mengi ya chakula cha kuku, kujitengenezea kienyeji na kuathiri wafugaji.

Ufugaji kuku ni fursa mtambuka ambayo inagusa kila eneo, kitoweo hicho kinahitajika kwa matumizi ya nyumbani na kwa biashara. Wapo wanaojiajiri kwa kutegemea kuuza miguu ya kuku, vichwa, utumbo. Kama kuku huyo hatakuwa kwa kiwango kinachotakiwa hata hiyo biashara haiwezi kuwa na uhitaji unaotakiwa.

Wanaohujumu ufugaji wa kuku lazima washughulikiwe ili wasiendelee kuathiri maisha ya wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Halmashauri zikopeshe vikundi vifaa badala ya utaratibu fedha

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imekuwa ikitenga fedha kupitia mapato ndani ya halmashauri nchini, kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, ili zitumike katika biashara mbalimbali vijiletee maendeleo.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo za kutaka kuinua makundi hayo kiuchumi, kumekuwapo sintofahamu ya kutorejeshwa fedha hizo kwa wakati au kutorejeshwa kabisa hali inayoweza kukwamisha wengine kukopeshwa.

Kwa mfano hivi karibuni, Mbunge wa Kinondoni Dar es Salaam, Abbas Tarimba, alisema katika kipindi cha mwaka jana, Halmashauri ya Manispaa Kinondoni ilitoa fedha za mikopo Sh. bilioni 3.5.

Akaeleza kwamba, kwa kuwa mikopo iliyotolewa kwa vikundi, asilimia 31 ya fedha hazijarejeshwa, anaishauri serikali kufanya ukaguzi, ili kujua mikopo hiyo inawafikia walengwa na kwa nini haijarejeshwa.

Urejeshaji mikopo katika halmashauri mbalimbali nchini umekuwa ukikumbwa na sintofahamu, hasa baadhi ya wanaokopeshwa kushindwa kurejesha. Ingependeza kama utaratibu huo ungebadilishwa.

Nadhani kwamba, badala ya kukopesha fedha, serikali ingeangalia uwezekano wa kununua vifaa na kukopesha vifaa kulingana na mahitaji ya vikundi, ili wahusika wavifanyie kazi ya uzalishaji mali.

Ukopeshaji fedha umeonekana kuwa na vikwazo vingi ikiwamo baadhi ya wakopaji kuzitumia kinyume na malengo na kujikuta wakishindwa kuzirejesha, hali ambayo inakwamisha mzunguko wa kukopesha wengine.

Imefikia wakati halmashauri zinatoa mikopo hiyo bila riba kama njia ya kuhamasisha makundi hayo yakope na kurejesha kwa wakati ili wengine walio kwenye foleni nao wakopeshwe, lakini bado kumekuwapo na ugumu.

Hivyo, nadhani njia nzuri ni kukagua vikundi na kuangalia mahitaji na kisha kuvigawia vifaa vya kufanyia, kama mafundi seremala wakopeshwe vifaa vinavyoendana na kazi yao, na kama ni vya wakulima nao vilevile.

Kama ni mama lishe, baba lishe na wajasiriamali wengine wakiwamo wanaofuga kuku, nao wakopeshwe vifaa vya shughuli zao, kwani hatua hiyo inaweza kusaidia fedha za umma kupotelea mikononi mwa watu wachache. Nitoe mfano maelezo ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI bungeni, Festo Dugange kwamba, mwaka 2015 hadi 2020, serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ilitoa Sh. bilioni 133 kwa ajili ya vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Lakini akabainisha kuwa katika kipindi hicho, jumla ya Sh. bilioni 92.21 tu sawa na asilimia 69.32 zilirejeshwa kutoka kwenye vikundi vya wanufaika, hali inayoonyesha kuwa kuna kiasi kingine cha fedha hizo hakijarejeshwa.

Natambua kuwa serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kutoa mikopo na urejeshaji mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kutoka kwa vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Lakini pamoja na kwamba mfumo huo wa kielektroniki unasaidia kujua kiwango cha mikopo na urejeshaji wake kwenye halmashauri zote 184 nchini, ninadhani utaratibu wa kukopesha vifaa ungefaa zaidi.

Kwa njia ya utoaji wa mikopo ya vifaa vya kufanyia kazi na hata fedha kidogo za mtaji, inawezekana kukawa na nidhamu kwani imeonekana baadhi ya wanaokopeshwa wameshindwa kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha.

Ukopeshaji wa vifaa unaweza kusaidia vikundi vingi zaidi kunufaika na hata kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa na baadhi ya wanaohitaji mikopo, kwamba kuna ukiritimba kuipata.

Waswahili wana msemo wao kwamba dawa ya deni ni kulipa, lakini kwa kuwa inaonekana baadhi ya wakopaji wamekuwa wakishindwa kurejesha mikopo kutokana na kuelekeza fedha kwenye matumizi mengine, suala la kutafuta njia nyingine ya kuwasaidia, ninadhani halina budi kubuniwa.

Njia hiyo ni kuwakopesha vifaa wavitumie kuzalisha mali na kurejesha kidogo kidogo fedha zilizotumika kununua vifaa hivyo, ili wanapokamilisha kulipa deni vinakuwa ni mali yao.

## HABARI KIMATAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (katikati), akizungumza na maofisa tarafa na watendaji wa kata katika ofisi za Hifadhi ya Taifa ya Ruaha juzi, walipofanya utalii katika hifadhi hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Shaka: Chama kinachotaka Muungano uvunjike kimeishiwa hoja na maarifa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

Chama Cha Mapinduzi(CCM) kimesema chama chochote cha siasa chenye shauku ya kuvunja Muungano au viongozi wake wakipania kuligawa taifa, kimeishiwa hoja na kina upeo mdogo na maarifa duni.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema hayo juzi mbele ya waandishi wa habari baada ya kumalizika kikao cha Kamati Maalum ya NEC kilichoketi mjini Unguja.

Shaka alisema hayo alipotakiwa kutoa mtazamo wake juu ya kauli ya baadhi ya wanasiasa hivi karibuni kudai ili Zanzibar itawale ni vyema kuwa na mamlaka kamili ya kufanya uamuzi wa mambo yake.

Alisema baadhi ya viongozi wa upinzani kwa muda mrefu wamekuwa na jitihada za kushawishi wananchi waone Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hauna maana na wala si muhimu, jambo ambalo ni upotoshaji mkubwa.

Kwa mujibu wa Shaka, wanasiasa wa aina hiyo hawana hoja za msingi kuwaeleza wananchi badala yake wamekuwa na kazi ya kuwajaza chuki na matumaini hewa ambayo hawana ubavu nayo wala uwezo wa kubadili lolote.

"Katika uongozi na siasa, viongozi mkishindwa kufikia matlaba yenu jamii huwapuuza. Wako watu bila Muungano wasingepewa hata usheha. Kutambulika kwao na sauti zao kusikika kwao, ni kuwapo kwa Muungano ambao leo wanaudhihaki na kuona si lolote wala chochote kutokana na ubinafsi wao wa nafsi," alisema.

Shaka alisema hata ustawi wa utulivu, amani na umoja katika pande mbili za Muungano, unatokana na uimara wa Muungano kwa kuwa nje ya Muungano si Tanganyika wala Zanzibar itakayobaki salama.

"Ndani ya Muungano kuna uhuru wa kutosha na watu wanaishi kwa amani. Nje ya Muungano usalama utapeperuka. Utulivu wa ndani na wa kisiasa utakosekana. Tusikubali kukichoma kichaka cha Muungano tutakosa mahali pa kujihifadhi," alisisitiza Shaka.

Alisema hata baadhi ya mataifa ya Ulaya Mashariki yalipokuwa chini ya Umoja wa Kisovieti yalijiona yako jela na USSR ilipogawanyika yakajikuta yakigeuka na baadhi yao sasa yemekuwa wakala wa ushetani.

"Tuna baadhi ya wanasiasa wetu wako tayari hata kuuza utu wao ili wamtumikie shetani aliye kizani. Watu hao kwa bahati nzuri ni wachache wenye uchu wa madaraka. Wangeungwa mkono na wengi tungalizamishwa au kupigwa bei mnadani," alisema. Shaka aliwatahadharisha wananchi wa Unguja na Pemba kuendelea kuwa makini na kauli za wanasiasa hao na kulinda umoja uliopo usipeperushwe na kimbunga.

Hata hivyo, Shaka alisifu uongozi bora, makini na wenye uthubutu wa kusimamia sera za mageuzi ya kiuchumi Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar.

Alisema viongozi hao wametawaliwa na uvumilivu, uchapakazi na wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata malengo ya kisera yaliyowekwa na CCM kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 - 2025, jambo ambalo limeendelea kuwafanya wananchi kuwa na imani kubwa na serikali na CCM.

# Ziara maofisa tarafa, watendaji Ruaha yatoa somo kukuza utalii

**Na Steven William,** IRINGA

MAOFISA tarafa na watendaji kata, katika wilaya ya Iringa, wamefanya ziara ya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kufurahishwa baada ya kuona simba wakifanya mapenzi.

Jambo hilo, watalii hao wa ndani wamesema hawajawahi kuliona katika maisha yao, hivyo kuwafanya watamani kupata muda mwingine wa kutembelea hifadhi hiyo.

Wakizungumza juzi wakati wa ziara hiyo iliyoratibiwa na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohammed Moyo, maofisa hao walisema wamefurahishwa namna hifadhi hiyo ilivyo na vivutio vingi.

Maofisa watendaji wa kata, Stella Makali na Aunty Mbilinyi, kwa nyakati tofauti walisema wamefurahi kufanya utalii katika hifadhi hiyo huku wakishuhudia simba jike na dume wanavyofanya mapenzi.

"Hii imetufanya kujifunza mambo ambayo tulikuwa hatuyajui tangu kuzaliwa kwetu. Tunatamani tupange muda mwingine wa kutembelea hifadhi hii kufanya utalii wa ndani," alisema Mbilinyi.

"Yaani ukiwa katika hifadhi unakuwa na furaha muda wote kwa namna ambavyo kuna vitu vingi vya kuvutia," aliongeza.

Emmanuel Ngabuji, Kaimu Ofisa Tarafa wa Pawaga, alisema, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha imejaliwa kuwa na vivutio vingi ambavyo mtalii akifika atafurahia na hatatamani kuondoka kutokana na maajabu yake na ubora wa hifadhi hiyo. Ngabuji, alisema watendaji wengi ni mara yao ya kwanza kutembelea hifadhi hiyo, kwa asilimia kubwa wamejipanga kwenda kutoa elimu ya utalii kwa wananchi wanaowaongoza.

Alisema, amejipanga kuhakikisha wananchi wa tarafa ya Pawaga, wanaandaa safari maalumu ya kwenda kutembelea Ruaha ili watoto na wananchi wengine waupende utalii wa ndani.

Ngabuji alisema, wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo amekuwa akiutangaza utalii wa Tanzania kupitia filamu ya The Royal Tour ambayo imeanza kuleta matokeo chanya ya ongezeko la watalii wa nje na wa ndani kutembelea vivutio mbalimbali. Charles Mhilu, mkazi wa Iringa alimshukuru Moyo kwa kuwaandalia safari ya kwenda kutembelea hifadhi, watendaji wa kata na maofisa tarafa jambo ambalo limefanyika kwa mara ya kwanza na limekuwa kivutio kikubwa cha kuendelea kuvitangaza vivutio vilivyopo katika wilaya ya Iringa. Moyo alisema, lengo la kuwapeleka maofisa hao katika hifadhi ya Ruaha ni kutambua umuhimu wa

utalii na namna ambavyo wanaweza kuwalinda wanyamapori dhidi ya hatari ya kutoweka na kuwarithisha wazao wao rasilimali hiyo. Moyo alisema, maofisa hao kutembelea hifadhi hiyo kunaongeza chachu ya ongezeko la watalii katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ikiwa sehemu ya kuunga mkono

## KABWELA





DAR ES SALAAM GYMKHANA CLUB

**NOTICE OF THE HALF YEARLY GENERAL MEETING 2022**

**[Issued under Article 13 of the Dar es Salaam Gymkhana Club Constitution, 2017]**

NOTICE is hereby given that the **Half Year General Meeting** of the Dar es Salaam Gymkhana Club will be held at the roof terrace of the Club on **Friday 30th September, 2022** commencing at **6:00PM.**

**AGENDA:**

1. To read the Notice convening the Meeting and confirmation of the agenda.
2. To confirm the Minutes of the Annual General Meeting held on Thursday 31st March, 2022.
3. Matters arising from 2 above.
4. To receive the Report of the Management Committee for the first six months of the year and the Audited Accounts for 2021 in accordance with Article 13(b)(i) and (ii).
5. At the discretion of the Chairman, to consider any other business of which the Half Yearly General Meeting is competent to discuss.

**Issued in Dar es Salaam this 09th day of September 2022**

**By Order of the Management Committee.**

**Ronald Kato**
**HONORARY SECRETARY**

217059102

SOS CHILDREN'S VILLAGES

SOS Children's Villages Tanzania
P.O.Box 13196 Arusha
www.sos-childrensvillages.org
A loving home for every child

**INVITATION FOR TENDER
FOR
WATER BOREHOLE DRILLING**

**23rd September 2022**

**Introduction**
SOS Children's Villages Tanzania is a local Non-Government Organization affiliated to SOS Children's Villages International, a worldwide child care and protection organization that provides orphaned and destitute children with a permanent home and educational opportunities. Established 60 years ago, SOS Children's Villages International the umbrella organization currently has Children's Villages and other projects in 135 countries around the world. Globally, it runs the SOS Children's Village Programme which has two main arms, i.e. Family Based Care based at SOS Children's Villages and Family Strengthening Programmes supporting families in local communities. SOS has been working in the United Republic of Tanzania since 1991 and implements its programs in the following locations Zanzibar, Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, and Iringa.

SOS Children's Villages Tanzania invites qualified Contractors to bid for the water Borehole Drilling at Ngaramtoni Urban within Arusha District Council as per the below specifications:

a) Direct mud rotary or percussion method of drilling is recommended right from the start to avoid caving in of the unconsolidated sediments during the drilling operation;
b) The recommended depth and well assembly for the borehole to be drilled are 150metres, and 15.24 cm respectively. The borehole diameter is recommended to be 20.32 cm.
However, the final drilling depth can be altered by the site supervisor depending on the rock strata penetrated, and the quality and quantity of water struck during the drilling operation;
c) A pilot hole should be drilled to the recommended depth and reaming to be done after the of the water;
d) Drilling of the borehole, design, and installation of well assembly, pumping test should be carried out under the supervision of a Hydrogeologist/Senior Technician;
e) Large, well-rounded quartz pea-size gravels (2 — 4mm diameter) should be used in packing the borehole.
f) Water from different strikes/aquifers should be chemically analyzed for quality at the Water Quality Laboratory
g) A concrete slab should be built around the top of the good assembly for sanitary Protection. The top five (0 — 10) meters should be cement grouted to avoid Pollution. After construction, the borehole should be fully developed by compressed air until the water becomes absolutely silt free before a production testing of at least 4 hours.
h) An interest Constructor should possess a valid class 1 Operation License

**Table No. 1: Detailed Specifications of the required Drilling**

| SIN | AB/2(M) | NN/2(m) | K | R^ | KxR (Am) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1.5 | 0.5 | 6.28 | 30.0 | 188.4 |
| 2 | 2.0 | ‘’ | 11.78 | 15.0 | 176,7 |
| 3 | 2.5 | | 18.84 | 8.0 | 150.72 |
| 4 | 3.0 | ‘’ | 27.48 | 2.5 | 68.7 |
| 5 | 4.0 | ‘’ | 49.46 | 1.05 | 51.93 |
| 6 | 5.0 | ‘’ | 77.77 | 0.5 | 38.88 |
| 7 | 6.0 | ‘’ | 112.26 | 0.3 | 33.67 |
| 8 | 8.0 | ‘’ | 200.18 | 0.15 | 30.02 |
| 9 | 10.0 | ‘’ | 313.22 | 0.089 | 27.87 |
| 10 | 10.0 | 2.5 | 58,88 | 0.27 | 15.89 |
| 11 | 12.0 | ‘’ | 86.51 | 0.20 | 17.30 |
| 12 | 15.0 | ‘’ | 137.38 | 0.11 | 15.11 |
| 13 | 20.0 | ‘’ | 247.28 | 0,075 | 18.54 |
| | 25.0 | ‘” | 388.58 | 0.059 | 22.92 |
| 15 | 25.0 | 5.0 | 1884 | 0.43 | 81.01 |
| 16 | 30.0 | ““ | 274.75 | 0.63 | 170,9 |
| 17 | 40.0 | ‘’ | 494.55 | 0,369 | 182.48 |
| 18 | 50.0 | ‘’ | 777.15 | 0.25 | 194.28 |
| 19 | 50.0 | 10.0 | 376.8 | 0.495 | 186.51 |
| 20 | 60.0 | ‘’ | 549.5 | 0.34 | 186.83 |
| 21 | 75.0 | ‘’ | 867.43 | 0.25 | 216.85 |
| 22 | 100.0 | ‘’ | 1554.3 | 0.15 | 233,14 |
| 23 | 100.0 | 25.0 | 388.75 | | |
| 24 | 125.0 | ‘’ | 942 | 0.375 | 353.25 |
| 25 | 150.0 | ‘’ | 1373.75 | | |
| 26 | 180.0 | ‘’ | | | |

***Note:** Interested Contractors Should apply for Drilling Permits from Pangani Water Basin Office-Moshi in accordance with Water Resources Management Act No. 11 of 2009.*

**Requirements:**
- A duly completed and signed price offer in Tanzania shillings VAT inclusive;
- Bidder should submit a **certified** copy of the valid Business license, Contractor's Registration Certificate, Certificate of Incorporation, VAT/TIN registration, Water Drilling Permit, and current Tax Clearance Certificate;
- Bidder must submit/indicate experience in carrying out similar Works;
- Bidder must indicate Defect Liability Period of the Borehole;
- Bidder should indicate completion time upon submission of their priced bids; and
- Bidder should state his terms of payment.

**Opening of Bids**
At the indicated time and place, the opening of Bids shall be carried out by SOS Children's Villages Tanzania, Arusha. It reserves the right to conduct the opening of Bids in Public or not.

**Submission of Bids:**
Bids must be submitted in a sealed envelope physically to SOS Children's Village of P.O.Box 13196 Arusha
***Bids shall be submitted by hand delivery to the above address on or before Wed, 6th October 2022at 14:00 EAT***
***Late Bids, bids not received and opened shall not be accepted irrespective of circumstances.***

***Note: No tender document will be issued, all enquiries should be addressed to** National.Office@sos-tanzania.org*

217057202

# Bibi, wajukuu walivyofariki kwa kukanyagwa na basi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKAZI wa Bonite mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, Kaslita Agust (57) akiwa na wajukuu zake wawili, Jasta Erick (9) na Wittines Erick (7), wamefariki dunia kwa kugongwa na basi.

Wakizungumza Nipashe baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, Laizer Daniel, alidai bibi huyo pamoja na wajukuu zake waliteremka kutoka kwenye bajaji kwa lengo la kuwavusha barabara watoto hao waliokuwa wanakwenda shule.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni basi la Kampuni ya Machame Express, lililokuwa kwenye mwendokasi kukata kona kwa haraka bila kuchukua tahadhari na kuwagonga.

"Walishushwa kwenye bajaji, kutoka Bonite wakawa wanasubiri chenji kutoka kwa dereva wa bajaji ndipo basi hilo lenye usajili namba T525 DZP lilipowaparamia na kufariki dunia papo hapo," alidai shuhuda huyo.

Alisema wakati wanakwenda kuwaokoa walisikia milio na kukuta bibi amepasuka kichwa, mtoto mmoja akiwa amekanyagwa kiunoni na mwingine kifuani.

"Tunaomba jeshi la polisi kuangalia uwezekano wa kuweka vivuko maalumu pamoja na kuongeza askari watakaosaidia uvukaji wa watoto nyakati za asubuhi na jioni, hapa pana bajaji nyingi, magari mengi na wafanyabiashara," alisema mmoja wa mashuhuda, Mwajuma Ramadhani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, hakuweza kuthibitisha ajali hiyo kwa madai kuwa alikuwa kwenye ugeni wa kimkoa wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.



Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika (wa pili kulia), akipokea msaada wa kitanda maalum cha kujifungulia wanawake wenye ulemavu kutoka kwa Mwasisi wa Taasisi ya Ikupa Trust Foundation ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Stella Ikupa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju (wa nne kulia), jijini Dodoma juzi. Msaada huo, ni sehemu ya fedha zilizotolewa na Taasisi ya Nos Vies en Partage Foundation (NVeP), inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ITF yatoa kitanda maalumu kujifungulia wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Ikupa Trust Fund (ITF) imekabidhi msaada wa kitanda maalum cha kujifungulia wanawake wenye ulemavu, chenye thamani ya Sh. milioni 1.3 kwa hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma.

Msaada huo wa ITF ulioasisiwa na Mbunge wa Viti Maalum, Stella Ikupa ni sehemu ya fedha zilizotolewa na Taasisi ya Nos Vies en Partage Foundation (NVeP), inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow.

Akiwa nchini hivi karibuni, Bristow alikabidhi msaada wa Dola za Marekani 10,000 kwa taasisi hiyo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanawake wenye ulemavu.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi kitanda hicho, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, ambaye pia ni Mwenyekiti wa ITF, inayoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu alisema wametoa msaada huo ikiwa ni moja ya jitihada za kuwarahisishia huduma wanawake wenye ulemavu.

"Sisi kama Ikupa Trust Foundation, tumeona tuanze kwa mfano kuja hapa katika hospitali hii ya Benjamin William Mkapa kukabidhi hiki kitanda lakini msaada huu tutaenda kutoa pia katika Mkoa wa Shinyanga na Dar es Salaam kwa kuanzia na mipango tuliyonayo ifikapo mwezi Juni 2023 tuwe tumekabidhi vitanda vipatavyo hamsini katika hospitali mbalimbali hapa nchini," alisema Amon Mpanju.

Muasisi wa taasisi hiyo na Mbunge wa Viti Maalumu kundi la wenye ulemavu Ikupa, aliishukuru serikali kwa kujali sana kundi la watu wenye ulemavu kwa kuweza kuona ipo haja ya kuwa na vyumba maalum vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu kwa kuielekeza serikali yake kuwa ipo haja ya kuwa na vyumba maalum vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu.

Ikupa aliwataka watu wenye ulemavu hasa wanawake kuona kuwa suala la kujifungua au kuleta uzao duniani ni maelekezo ya Mungu na ifike mahala waone kwamba mwanamke mwenye ulemavu ni kama wanawake wengine.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Benjamin William Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, amesema anaishukuru sana taasisi ya ITF kwa kuwapatia kitanda hicho kwa kuwa itaongeza ufanisi katika kuhudumia wajawazito wenye ulemavu.

Dk. Chandika, aliwaahidi wananchi kuwa kwa msaada huo watambue kuwa wao kama Hospitali ya Benjamin Mkapa, wanawajali sana kina mama hao walemavu.

## Benki yaanza kusaidia wajasiriamali wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imedhamiria kusaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kutoa huduma zinazokidhi mahitaji yao na kutatua changamoto zinazowakabili.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkuu wa Uzalishaji wa Benki hiyo, Kai Mollel, katika kongamano la sita la mwaka la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lenye kaulimbiu: "Uwezeshaji wa Watanzania katika Uwekezaji" lililofanyika Septemba 19, jijini Dodoma.

Jukwaa hilo la siku moja lilihudhuriwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye aliwapongeza wadhamini wakuu kwa kuisaidia NEEC kufanikisha jukwaa hili, huku akitilia mkazo kuwa serikali inathamini mchango wao kwa kuzingatia serikali iko katika mpango wa kutengeneza mazingira mazuri ili Watanzania waweze kushiriki katika shughuli za uwekezaji.

Wakati wa hotuba yake, Mollel aliahidi kuwa benki itafanya kazi bega kwa bega na serikali kusaidia ukuaji wa Wajasiriamali. "Tunapenda kuihakikishia serikali, wafanyabiashara na wadau wote wa maendeleo kwamba sisi kama benki tutaendelea kushirikiana nanyi katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu," alisema Mollel.

Aliipongeza NEEC kwa kuandaa kongamano hilo na kufurahia mazungumzo yatakayochochea uwekezaji wa ndani. "Benki yetu inaongoza kwa uwekezaji na mwaka huu tumetunukiwa tuzo ya Benki Bora ya Uwekezaji na EuroMoney Market Leaders kwa mwaka 2022 zote kutoka kwa jarida la EuroMoney. Hii ni kwa sababu tumeendelea kutoa huduma mbalimbali zinazowawezesha Watanzania kushiriki na kunufaika na uwekezaji nchini," alisema Mollel.

Alisema benki hiyo imekuwa katika safari ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati na hivi karibuni imeingia ubia na NEEC kutekeleza programu ya 'Supplier development' na wajasiriamali 50 watapatiwa mafunzo na kupatiwa vitendea kazi vya kuwawezesha kutumia fursa za uwekezaji nchini na kuongeza ushindani wao kikanda na kimataifa.

"Benki ya Stanbic inaendelea kupiga hatua katika kukuza uwekezaji miongoni mwa wateja wake nchini. Kuunga mkono jukwaa hilo ni ishara kuwa benki imejizatiti kuimarisha sekta ya uwekezaji, pamoja na kuwawezesha wananchi kutumia rasilimali na fursa zilizopo ili kuleta maendeleo ya kiuchumi katika taifa."

# TAKUKURU yaanza uchunguzi madai ya ubadhirifu mamilioni ujenzi VETA

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU), imeanza kuchunguza tuhuma za ubadhirifu wa mamilioni ya fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu Sabasaba kilichoko mjini Singida.

Kuanza kuchunguzwa kwa suala hilo kunatokana na agizo alilolitoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, kwa TAKUKURU baada ya kutembelea chuo hicho na kubaini ubadhirifu mkubwa uliofanywa na watendaji wa serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi (CP) Salum Rashid Hamduni, akizungumza jana katika mahojiano na gazeti hili kwa njia ya simu, alisema taarifa za ubadhirifu katika chuo hicho zilishaifikia taasisi hiyo na uchunguzi umeshaanza.

"Taarifa tushaipokea ni tuhuma dhidi ya hawa watendaji wa kwetu na tangu ilipopokewa mpaka sasa inafanyiwa kazi. Unajua tuhuma zinahitaji kuchunguzwa na huwezi ukakimbilia kwenye kutoa majibu kabla ya kufanya uchunguzi," alisema.

Hamduni alisema uchunguzi utakapokamilika utaielekeza taasisi hatua sahihi za kuchukua dhidi ya watendaji watakaobainika walihusika na ubadhirifu huo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Prof. Ndalichako alifanya ziara mkoani Singida na kubaini ubadhirifu wa mamilioni ya fedha za UVIKO-19 katika chuo hicho.

Ubadhirifu alioubaini ni katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo vimenunuliwa kwa bei kubwa kuliko uhalisia, kuweka makadirio makubwa ya mahitaji ya vifaa vya ujenzi (BOQ) na kutopelekwa kwa baadhi ya vifaa katika chuo hicho wakati inaonyesha fedha zilishatolewa kwa ajili ya kuvinunua.

Prof. Ndalichako alibainisha vitu ambavyo vina utata kuwa ni matofali yaliyokuwa yanatakiwa katika ujenzi kwenye chuo hicho ni 7,000 lakini kwenye BOQ iliyoandaliwa na watendaji ni 14,700 na pesa ikatolewa.

Aliongeza kuwa bei ya saruji iliwekwa kubwa Sh.18, 000 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na pia kwenye BOQ iliandikwa itatumika mifuko 2,912 wakati inayotakiwa kwa ajili ya kazi hiyo ni 900 kwa mujibu wa mkandarasi huku pesa iliyotolewa ni kwa mifuko 2,912.

Kuhusu nondo ziliandikwa kuwa zinahitajika 1,198 lakini uhalisia zinazohitajika ni 50 tu lakini pesa iliyotolewa ni ya nondo 1,198 na bei iliyowekwa kwa nondo moja ni Sh.8,000 badala ya Sh.5,000.

Alisema vioo bei ambayo chuo ilinunua ni Sh. 120,000 lakini kwenye BOQ imeandikwa kuwa vimenunuliwa kwa Sh.220,000 jambo ambalo linaondoa maana halisi ya kutumia 'force account'.

"Kwa ujumla kazi hii haifai hata kidogo. Vitu haviko katika uhalisia kabisa na BOQ iliyotumika kwenda kuombea fedha haiwiani na jinsi vifaa vilivyonunuliwa. Hapa itabidi watu wa ununuzi watusaidie je, huu mfumo wa 'force account' umezingatiwa?" alisema.

Prof. Ndalichako alisema tatizo kubwa katika mradi huu vitu vya kununua viliwekwa vingi kuliko uhalisia mfano vikiwekwa vifaa vya kuanzishia kazi kwamba yatanunuliwa mashoka 22, majembe 22, koleo 22, nyundo 22 na matoroli 22 na pesa ilishatoka lakini hakuna hata kitu kimoja kilichotoka.

Pia marumaru zinazohitajika kwa ajili ya kazi hiyo ni maboksi 900 lakini pesa iliyotoka ni ya boksi 1,105 na pia bei ya mabati imeandikwa kuwa yamenunuliwa kwa bei kubwa ya Sh.99,120 lakini chuo kilinunua kwa Sh.60,000 tu.

Aliongeza kuwa katika mchanganuo wa gharama za ukarabati wa chuo hicho ilikuwa ziletwe Sh. milioni 812 lakini zimeongezwa na kufikia Sh. milioni 862 na kwamba jambo hili halikubaliki kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza watendaji kuwa waadilifu kuhakikisha wanalinda fedha za serikali.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu Sabasaba, Fatma Malenga, kila alipoulizwa na Waziri kuhusu utata wa ununuzi wa vifaa hivyo, alisema mambo mengi yalikuwa yanafanywa na watu wa wizarani hivyo hajui lolote.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emmanuel Mjema (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza kilele cha harambee ya kutafuta Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa mabweni ya wasichana itakayofanyika Jumamosi hii jijini Mbeya. Kushoto ni Naibu Mkuu wa chuo (Mipango, Fedha na Utawala), Dk. Emmanuel Munishi na Ofisa Uhusiano wa chuo, Leonidas Tibanga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa kuzindua kampasi CBE Mbeya

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimekamilisha ujenzi wa kampasi yake mkoani Mbeya na kimeendelea kuwaomba wadau wachangie ujenzi wa mabweni ya wasichana.

Majengo ya kampasi hiyo yanatarajiwa kuzinduliwa Oktoba 8, mwaka huu, jijini Mbeya na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Hayo yalisemwa jana chuoni hapo na Mkuu wa chuo hicho, Profesa Emmanuel Mjema, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kilele cha harambee inayotarajiwa kuwa Jumamosi hii jijini Mbeya.

Majengo ya kampasi hiyo yanaweza kuchukua wanafunzi 2,000 na mpaka sasa kimeshachukua wanafunzi 1,000 tayari kwa kuanza masomo.

Alisema majengo yaliyokamilika ni ya utawala, kumbi za mihadhara, maktaba na ofisi za wafanyakazi.

Prof. Mjema alisema mpaka kukamilika kwake majengo hayo yamegharimu Sh. bilioni 1.46 ambazo zimetokana na mapato ya ndani.

"Napenda kutoa taarifa kwamba ujenzi umekamilika ambapo kwa sasa mazingira ni mazuri kwani miundombinu mipya na ya kisasa inakifanya chuo kutoa huduma kwa ufanisi na tunaomba wadau wajitokeze kuchangia tujenge mabweni ya wasichana," alisema Profesa Mjema. Alisema wanafunzi wakike wanaishi kwenye mazingira magumu kwani wengi wao wanaanza chuo wakiwa na umri mdogo na ndiyo sababu wametoa kipaumbele kwao kujengewa bweni.

Profesa Mjema alisema kilele cha harambee ya kujenga mabweni ya wasichana itafanyika Jumamosi ya tarehe 24, mwezi huu, jijini Mbeya na mgeni rasmi atakuwa Spika wa Bunge ambaye ndiye mlezi wake, Dk. Tulia Ackson.

Alisema chuo kimefanya juhudi za kuwafikia wadau mbalimbali zikiwamo taasisi na mashirika ya serikali na yasiyo ya kiserikali pamoja na sekta binafsi kuchangia ujenzi huo.

Vilevile, alisema chuo kimeweza kufikisha jambo hilo kwa wabunge kwani pia ni wadau muhimu wa maendeleo ya elimu nchini.

"Tunawaomba wadau wote wenye mapenzi mema na maendeleo walipo ndani na nje kutushika mkono kwa kuchangia chochote ili tuweze kukamilisha harambee pia tukimuunga mkono mlezi wa Kampasi ya CBE Mbeya, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Spika wa Bunge la Jamhuri wa Tanzania pia Mbunge wa Mbeya Mjini," alisema.

Aliwashukuru wadau ambao tayari wamechangia na wengine kutoa ahadi zao.

# Spika aiweka kikaangoni wizara tofauti ya takwimu kesi za kodi

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameagiza Wizara ya Fedha na Mipango kuandaa upya majibu ya swali la msingi la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, lililoulizwa kuhusu kesi za kodi kutokana na takwimu kutofautiana.

Katika swali la msingi alilouliza bungeni jana. Mpina alihoji nini kinachosababisha kesi 1,097 za kodi za muda mrefu zenye thamani ya Sh. trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.4 kutoamuliwa hadi sasa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alisema hadi Agosti, mwaka huu, kulikuwa na idadi ya mashauri 854 kwenye hatua mbalimbali za usikilizaji yenye kodi inayobishaniwa ya Sh. Trilioni 4.21 na dola za Marekani milioni 3.48 katika taasisi za rufani za kodi ambazo ni TRAB na TRAT.

"Hivyo, kwa sasa TRAB na TRAT zinaendelea kusikiliza mashauri hayo pamoja na mashauri mapya yanayoendelea kusajiliwa," alisema.

Aidha, alisema kwa nyakati tofauti, idadi ya mashauri ya kodi hupungua au kuongezeka kulingana na kasi ya usikilizaji na usajili.

Kutokana na majibu hayo, Mbunge huyo alisema swali limeuliza Sh. Trilioni 360 lakini majibu yanaonyesha Sh. trilioni 4.21.

"Kwa nini serikali ilikubali kupokea Sh. bilioni 700 kutoka kwenye kesi za malimbikizo ya madini (makinikia) badala Sh. trilioni 360 ambazo ni madai halali katika nchi yetu?" alihoji.

Kutokana na mkanganyiko huo, Spika Tulia alilazimika kumkatisha Mbunge Mpina na kuhoji serikali ukweli wa takwimu hizo za kesi na fedha.

"Kwanza nipate ufafanuzi swali linazungumzia kesi 1,097 jibu linazungumzia mashauri 854, haya ndiyo mashauri yaliyopo ambayo serikali inayajua ni tofauti na mbunge au ni kati ya yaliyopo ndiyo mmeleta majibu? Nataka kuelewa hapo," alisema.

Naibu Waziri Chande alimwambia Spika kuwa mashauri hayo ndiyo ambayo yako kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali huku Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akisema serikali haijapokea kimya kimya Sh. bilioni 700 na kuacha Sh. trilioni 360.

"Kuna utofauti kesi Sh. trilioni 360 aliyozungumzia Mpina ni ya makinikia ambayo haiko kwenye kesi za rufani za kikodi na hii ya mashauri ya Sh. trilioni nne ni ya kesi zingine ambazo ndizo serikali inaendelea kufanyia kazi," alisema.

Hali hiyo ilimlazimu Spika Tulia kueleza kuwa majibu ya serikali bado hayajaonyesha kujibu swali la msingi la mbunge na kuagiza majibu yawasilishwe upya bungeni kulingana na swali lilivyouliza.



Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, akichangia hoja Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Marekebisho sheria ununuzi, ukandarasi yaja

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2022/23, marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Ukandarasi kupitia ushirikiano wa serikali na sekta binafsi (PPP) yatakamilika.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Katika swali lake, Shangazi alihoji lini sheria ya manunuzi na ukandarasi kupitia PPP itaanza kutumika.

Naibu Waziri Chande akijibu swali hilo, alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ipo na inatumika sambamba na Sheria ya PPP Sura 210 na kwamba mchakato wa zabuni za miradi ya PPP unazingatia sheria zote mbili.

"Pamoja na sheria hizo kutumika kama rejea wakati wa uunuzi wa miradi ya ubia, serikali inaendelea na utaratibu wa kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau ili kurekebisha vifungu vyenye changamoto katika utekelezaji wake," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kwa mujibu wa sheria ya PPP kiwango cha mtaji kwa wazawa ni Dola za Marekani milioni 20 na kuhoji kuwa serikali haioni kiwango hiko ni kikwazo kwenye utekelezaji wa sheria hiyo.

"Serikali ina mpango gani wa kupunguza masharti ya kimkataba kwenye miradi inayoibuliwa na sekta binafsi ili kutekelezwa kwa ufanisi kupitia PPP?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Chande alisema sheria PPP iko kwenye mchakato wa kufanyiwa marekebisho ambapo kwa sasa ukusanyaji maoni unaendelea.

Pia alisema masharti yaliyopo ni kwa mujibu wa sheria na taratibu na kwamba huenda yakapungua baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa wadau.

# TAMISEMI yaomba kibali ajira za walimu

IMEELEZWA kuwa kwa mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeomba kibali cha kuajiri walimu 42,697 na kipaumbele kitatolewa kwa walimu wa sayansi na hisabati na wanaojitolea maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, wahitimu 20,109 wa kada ya ualimu wa masomo ya sayansi na hisabati kati ya 33,492 hawajaajiriwa katika shule za serikali, kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2022.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji takwimu za wahitimu wa kada ya ualimu wa masomo ya sayansi na hisabati ambao hawajaajiriwa tangu mwaka 2015.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema wahitimu ambao hawajaajiriwa ni wa stashahada 8,154 na wa shahada 11,955.

"Kati ya wahitimu ambao hawajaajiriwa katika shule za serikali, wako wahitimu mbalimbali walioajiriwa katika shule binafsi 1,522 za sekondari na 2,449 za awali na msingi nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kuajiri ili kukidhi mahitaji ya walimu katika shule.

Awali, alisema tangu mwaka 2015 hadi 2022, wahitimu 33,492 (stashahada 13,534 na shahada 19,958) wa kada ya hiyo katika vyuo mbalimbali vya ualimu vya kati na vyuo vikuu.

"Kati yao wahitimu 13,383 (stashahada 5,380 na shahada 8,003) wameajiriwa katika shule mbalimbali nchini tangu mwaka 2015,"alisema.

Katika maswali yake ya nyongeza, Mbunge huyo alisema ambao hawajaajiriwa ni asilimia 60 na wanajitolea bila ajira rasmi na kuhoji kwa nini serikali isiwaajiri kwenye maeneo wanayojitolea sasa.

Kipanga akijibu swali hilo, alisema: "Kwa mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeomba kibali cha kuajiri walimu 42,697 na kwamba kipaumbele kitatolewa kwa walimu wa sayansi na hisabati na wanaojitolea maeneo mbalimbali nchini."




Habari zote: Augusta Njoji
DODOMA

## Shule Sekondari ya Irkisongo yapewa msaada kompyuta 20

**Na Allan Isack,** MONDULI

SHULE ya Sekondari Irkisongo, iliyoko wilayani Monduli mkoani Arusha, imepewa kompyuta 20 zenye mfumo rahisi wa kufundishia, kuongeza tija na hamasa kwa wanafunzi kupenda kusoma hususani somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA).

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, aliyasema hayo jana wakati akikagua mradi wa kompyuta katika Shule ya Sekondari Irkisongo, wilayani humo.

Kompyuta hizo zimewekewa mfumo bora na imara wa kufundishia ili kuongeza chachu kwa wanafunzi wa shule hiyo kupenda zaidi kusoma kwa njia ya mtandao.

Kutokana na umuhimu wa teknolojia ya kompyuta hizo, Katibu Tawala Mkoa huo, alimwagiza Ofisa TEHAMA wa Mkoa huo, David Nyangaka, kuongeza kompyuta nyingine 10 katika shule hiyo ili wanafunzi wapate fursa ya kujifunza kisasa kwa njia ya mtandao.

"Shule hii bado inauhitaji wa kompyuta nyingine hivyo nakuagiza ongeza nyingine 10 ili wanafunzi wengi wapate nafasi ya kujifunza kwa kuwa ukizingatia teknolojia kwa sasa duniani inakwenda kwa kasi mno hivyo watoto wetu wakipata kuelewa itakuwa ni jambo muhimu kwa maslai yao na Taifa," alisema.

Hata hivyo, alisema mfumo wa kufundisha kwa kutumia kompyuta umeongeza ufanisi na kurahisisha ufundishaji kwa walimu na wanafunzi wanajifunza kwa vitendo na hivyo kuongeza hamasa ya kupenda masomo hasa ya sayansi.

Pia katika ziara hiyo alikagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Miserani uliogharimu Sh.milioni 600 hadi kukamilika kwake, aliridhishwa na utekelezaji wa mradi kwa kuwa ameikuta idara ya elimu katika halmashauri hiyo, ikiendelea kusimamia vizuri miradi yote.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Monduli, Rose Muhina, alisema wataendelea kusimamia miradi yote ili iweze kukamilika kwa wakati ili wananchi kupata huduma bora.

Alisema: "Sisi viongozi wa halmashauri tukiwa ni watendaji na watumishi wa serikali tutahakikisha tunasimamia miradi yote ya maendeleo ikamilike kwa wakati na wanachi waweze kupata huduma bora na za uhakika.

"Kwa kuwa lengo la serikali ni kutoa kuwahudumia wananchi tukiwa sehemu ya watumishi serikalini hatuwezi kuwa sehemu ya kuikwamisha serikali kutokufikia malengo yake," alisema.

# Sumaye awapa mbinu wafugaji kukabiliana mabadiliko tabianchi

**Na Allan Isack,** HANANG'

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye, amewataka wafugaji wilayani Hanang' mkoani Manyara, kutumia teknolojia ya kuhifadhi malisho ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana wilayani humo, wakati akiwatembelea wafugaji wanaotumia zana kuchakata na kuhifadhi mazao yanayotokana na nafaka zinazotengenezwa na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMATEC).

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi imesababisha madhara makubwa duniani kwa baadhi ya maeneo nchini yanakosa malisho ya kutosha kutokana na uhaba wa mvua.

"Wafugaji mnatakiwa kutumia teknolojia hii kwa ajili ya kuhifadhi chakula cha mifugo yenu kwa kuwa mkitegemea mvua tu itakuwa ni tatizo kubwa kwa kuwa zimekuwa hazitabiriki wakati wa kunyesha kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema Sumaye.

Alisema kutumia teknolojia za kuchakata na kuhifadhi malisho hasa kwa mazao ya nafaka ikiwamo ya mahindi itawasaidia wafugaji kuwa na uhakika wa chakula cha mifugo yao nyakati zote bila ya kutegemea mvua.

"Ndugu zangu wafugaji kutokana na shughuli za kibinadamu kumekuwapo na athari mbalimbali hivyo tukitumia teknolojia hizi zitakuwa na faida kwenu hasa mtakuwa na chakula cha uhakika cha mifugo kadhalika mtafanya ufugaji wa tija na itawasaidia kuowaongezea kipato na kukuza uchumi wenu," aliongeza.

Ezekiel Sumari, mtengenezaji wa mashine za kuchakata malisho, alisema teknolojia hiyo, itasaidia kuzuia kupoteza malisho kwa kuchakata na kuhifadhi na kutumia nyakati za kiangazi.

"Teknolojia hizi ni rafiki endapo wafugaji watazitumia kwa kuwa nyakati za kiangazi wamekuwa wakiangaika maeneo mbalimbali nchini kwenda kutafuta malisho ya mifugo, hivyo wakiitumia itawasaidia kuhifadhi chakula na mifugo yao na haitateseka au kufa kwa kukosa malisho," alisema.

Jacob Baso, mnufaika wa teknolojia hiyo na mfugaji wilayani humo, alisema imemsaidia kuweka akiba ya kutosha ya chakula cha mifugo, pia imemsaidia kufuga kwa uhakika bila ya kuwa na hofu ya mifugo yake kufa kwa kukosa malisho.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, akikagua gwaride la wahitimu wa mafunzo ya awali ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kwa mujibu wa sheria ya operesheni Jenerali Mabeyo 2022, katika kambi ya Makuyuni, wilayani Monduli, mkoani humo, jana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

## Katibu Tawala akoshwa ujenzi Hospitali ya Wilaya

**Na Allan Isack,** KARATU

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, amesema kuwa ameridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa Hospitali ya Wilaya Karatu, kwa kuwa ujenzi huo umekidhi viwango na kuzingatia matumizi ya fedha zilizotolewa hadi kukamilika kwake.

Ujenzi wa hospitali hiyo, umegharimu Sh.bilioni 2.9 huku serikali ikitoa Sh.bilioni 1.7 na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wakichangia Sh.milioni 700.

Aliyasema hayo jana alipokuwa kwenye ziara yake ya kikazi kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Karatu mkoani humo.

"Napenda kuwapongeza viongozi wa Wilaya ya Karatu wakiwamo watumishi na wataalamu kwa usimamizi mzuri na utekelezaji wa ujenzi wa mradi kwa kweli binafsi nimeridhishwa na ujenzi huu kwa kuwa umezingatia ubora na matumizi ya fedha," alisema Musa.

Alisema kukamilika kwa hospitali hiyo, kutaleta unafuu kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo ya jirani kwa kuwa watapata huduma za afya za uhakika karibu na makazi yao bila ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Kiongozi huyo wa serikali mkoani humo, alisema hadi sasa tayari majengo ya wodi ya wazazi, mionzi, kufulia, dawa, huduma za dharura, nyumba ya watumishi, Jengo la Wagojwa wa Nje (OPD) na maabara ujenzi wake umefikia katika hatua za mwisho kukamilika na huduma zitaanza kutolewa hivi karibuni.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, alisema wamewekeza nguvu kubwa katika ujenzi wa hospitali hiyo, kwa kuwa eneo hilo, halijawahi kuwa na Hospitali ya Wilaya.

Vilevile alisema watahakikisha hospitali hiyo inaanza kufanya kazi mapema iwezekanavyo ili wananchi wapate huduma za afya kwa kuwa wako katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi.

Katika hatua nyingine, Katibu Tawala huyo, alikagua miradi mingine ya maendeleo ikiwamo ya shule, kituo cha afya na Hospitali ya Wilaya kwa lengo kujiridhisha kama kazi imefanyika ilivyokusudiwa.







Mbunge wa Simanjiro, mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka (kulia), akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Naepo, kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo, katika mkutano kijijini hapo juzi. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Naisinyai, Taiko Laizer. **PICHA: GIFT THADEY**

# Madaktari Uholanzi, KCMC wafanya utafiti wa chanjo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANASAYANSI na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu kutoka Uholanzi, kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, wameanza kutafuta suluhisho la utofauti wa kiufanisi wa chanjo mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi.

Hayo yamejiri baada ya madaktari hao, kubaini uwapo wa utofauti wa ufanyaji kazi wa chanjo hizo, katika miili ya binadamu kutokana na aina ya mazingira.

Daktari wa Magonjwa ya Ndani katika Hospitali ya KCMC, Dk.Elichilia Shao, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kwenye mahojiano maalum.

Alisema, nchi za Afrika zinahitaji sana chanjo kutokana na uwapo wa milipuko ya magonjwa ya kuambukiza, lakini chanjo hizo zimekuwa na matokeo tofauati ya ufanisi kati ya mtu mmoja na mwingine.

Alisema, katika kutafuta suluhisho la utofauti huo, baadhi ya watafiti wameanza kufanya utafiti kwa wananchi wanaoishi mijini na vijijini kwa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, kuangalia ufanisi wa chanjo kutokana na mazingira na aina ya vyakula na hatimaye kujua aina ya chanjo inayohitajika.

Mwanasayansi wa Maabara, Dk.Jeremia Pyuza, alisema kumekuwapo na utofauti kubwa kwa baadhi ya maeneo kwa wananchi wanaopata chanjo imeonekana kufanya kazi na maeneo mengine imeshindwa kufanya kazi.

Akizungumza juu ya utafiti huo, Dk. Pyuza, alisema umelenga kubaini utofauti wa kinga ya mwili uliyoko kati ya watu wanaoishi mjini na vijijini, pia utatumia chanjo ya homa ya manjano kubaini ufanisi wa chanjo hiyo katika maeneo hayo.

"Matokeo ya utafiti huu, yanakwenda sambamba na kutuelekeza dhima kubwa ya kwamba je chanjo mbalimbali zinazotolewa kwa watu wa Tanzania zinafanyaje kazi kwa watu wa vijijini na mijini na kama kuna utofauti je unatafsiriwa vipi kwenye masuala ya kinga ya mwili.

"Hii itatupa picha kwamba kama tunatakiwa kuongeza dozi, au kubaki na dozi zilezile tunazozitumia kwa kuwa itaisaidia hata nchi kwenye matumizi ya chanjo na ugawaji wa chanjo katika maeneo mbalimbali. alisema" Alisema kinga ya mwili inaathiriwa na vitu mbalimbali, ikiwamo vimelea wanavyokutana navyo kwenye mazingira ya kazi, chakula na kazi kati ya watu wa mjini na vijijini ni tofauti ndiyo sababu wakati wa mlipuko wa UVIKO- 19, watu wanaoishi mijini waliathirika zaidi kutokana na kinga zao kuwa chini ukilinganishwa na wanaoishi vijijini.

Mtaalamu wa Masuala ya Afya ya Jamii, Anastazia Ngowi, aliwataka wananchi watakapotembelewa na watafiti hao, kutoa ushirikiano ili waweze kufanya utafiti sahihi wa kuiwezesha nchi kupata chanjo inayoendana na mazingira ya kitanzania.

"Utafiti huu ni fursa kwa wananchi wetu, kwa kuwa unakwenda sambamba na kutoa elimu juu ya kinga ya mwili, jamii itaelimishwa kuhusu kinga ya mwili na namna ya kuiboresha, kuitunza kinga kwa kuwa ni muhimu kwa kuwa inapokua bora ndio inakusaidia kujikinga na maradhi,"alisema Ngowi.

## TRA yawataka wafanyabiashara kuainisha matatizo

**Na Mary Mosha** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA),Mkoa wa Kilimanjaro, imewataka wafanyabiasha kuainisha matatizo yanayowakabili na vikwazo katika ulipaji wa kodi mbalimbali ili waweze kuzungumza na kutatua.

Akizungumza jana wakati wa semina maalumu kati ya wafanyabiashara na mamlaka hiyo juu ya mabadiliko ya sheria mbalimbali zilizofanyika marekebisho, Meneja TRA Kilimanjaro , Masawa Masatu, alisema wako tayari kufanya mazungumzo na kupokea ushauri wa namna bora ya ulipaji wa kodi kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

Alisema, wameanza utaratibu wa kukaa na wafanyabiashara na kujenga uhusiano mzuri ili kupokea matatizo na ushauri wa namna ya kutatua.

Aliwataka wafanyabiashara hao, kutoa taarifa endapo kuna ofisa yeyote wa mamlaka hiyo, atakayemtishia au kuomba rushwa kwa ajili ya kumsaidia kutatua matatizo yao.

"Tumekutana na wafanyabiashara kutaka kufahamu matatizo yao, kadhalika suala la mfumo, ambalo tayari serikali ilishaanza kulifanyia kazi kwa kuwekeza fedha nyingi na imani mpaka ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2022/23 itakuwa historia kwa kuwa kazi itakuwa imekwisha.

"Bado suala la magendo ni tatizo katika mkoa wetu,kwa mpakani na uko wazi, hivyo baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu hutumia mwanya huo kutekeleza makosa ya kiuhalifu TRA, tumejipanga na vikosi vya doria kwa kuwa tumekuwa tukiwakamata na wengine wamepewa adhabu na kutaifishwa mali zao," alisema.

Alisema, vituo vya forodha vilivyoko mkoani ni rafiki na aliwataka wafanyabiasha kuacha kutumia njia za magendo na endapo kuna matatizo wako tayari kuwasikiliza.

"Serikali haina nia ya kufilisi mitaji ya watu kwa kuwalipisha fidia au kutaifishwa mali zao na kukuacha kwenye umasikini mkubwa na badala yake, imeweka sheria ili kulinda afya za walaji pamoja na kudhibiti ushindani wa soko hapa nchini," alisema Meneja.

Ofisa Msimamizi wa Kodi, Elimu na Huduma kwa Mlipa Kodi Mkoa wa Kilimanjaro, Odupoi Papaa, alisema tayari serikali imeanza kuchukua hatua za kutatua kero za wafanyabiashara kwa kuwa wamefanya mabadiliko ya sheria mbalimbali ili kuweka mazingira bora na wezeshi ya kibiashara.

"Tutaendelea kukaa na wafanyabiashara kuwasikiliza na kupokea maoni yao, ili kila mmoja aweze kufanya biashara na kulipa kodi bila kusukumwa,"alisema Papaa.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara,Mkoa wa Kilimanjaro, Sanifa Nkya, alisema mazungumzo hayo yatasaidia kujenga uhusiano mzuri kati ya wafanyabishara na taasisi hiyo, kadhalika itasaidia kuwapo kwa ulipaji wa kodi kwa hiyari na kwa wakati.

Mhasibu Mkuu wa Manispaa ya Moshi, Pontian Kahwa, alisema wamehudhuria kwenye semina hiyo, kwa lengo kusikiliza matatizo yanayowakabili wafanyabiashara na kuangalia namna ya kuyatatua.

Baadhi wafanyabiashara hao, akiwamo Filipho Makungu, aliishauri TRA kuwashirikisha wafanyabiashara katika mchakato wa utozaji wa kodi, ili kila mmoja awe na ufahamu wa kutambua umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari.

Ukurasa 16



MRADI NYUMBA WATUMISHI UMMA

## Bosi Dk. Msemwa achanganua wanachokitoa, aliyeuziwa afunguka kilichomo maisha mapya

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 23, 2022

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe



## Yaliyojificha tatizo watoto mtaani na ombaomba

Ukurasa 14

RUTO ATINGA KIKAONI UMOJA WA MATAIFA

# Ahutubia akizitaka Benki ya Dunia, IMF zisogeze muda kudai madeni




Rais William Ruto akihutubia kikao cha Umoja wa Mataifa (UN).

Wajumbe wakifuatilia kikao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS William Ruto wa Kenya, amezitaka Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kuongeza muda wa msamaha wa madeni kwa mataifa yanayoendelea, katika hotuba yake ya kwanza kama mkuu wa nchi katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York.

Kiongozi huyo wa Kenya, anabainisha kwamba nchi nyingi bado zinaendelea kupata ahueni kutokana na athari mbaya za janga la Covid-19 na msamaha wa madeni utasaidia sana kufanikisha miradi ya maendeleo ambayo tayari imeanzishwa na nchi hizo.

Ruto, ambaye amekuwa ofisini kwa muda wa wiki moja, anasema kuwa Kenya, kama ikiwa ni nchi ya kipato cha kati, bado inakabiliana na kushuka kwa uchumi na shinikizo la mfumuko wa bei hivyo basi, haja ya kurekebisha mipango ya ulipaji wa mkopo.

"Ninaungana na viongozi wengine kutoa wito kwa Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa na wakopeshaji wengine wa kimataifa kupanua misamaha ya madeni yanayohusiana na janga kwa nchi zilizoathiriwa zaidi, hasa zile zilizoathiriwa na mchanganyiko mbaya wa migogoro , mabadiliko ya hali ya hewa na Covid-19,"anatamka Rais Ruto.

Pia, rais huyo anatoa wito kwa nchi nyinginezo kushirikiana na zinazoendelea, kusaidia kukabiliana na janga hilo akifafanua Kenya na nchi za Afrika zinazoendelea, zinahitaji ushirikiano wa kimataifa kukwepa shida za kiuchumi na kukwepa madhila hayo.

Anasisitiza hayo, wito huo ukizingatiwa utasaidia nchi za kipato cha kati kuanza ajenda zao za maendeleo na kuepusha mzozo wa kiuchumi.

Ni maaoni yanayojiri miezi michache, baada ya Hazina ya Kitaifa ya Kenya kuweka wazi deni la Kenya lilikuwa Sh.(za Kenya) trilioni 8.6 kwa mchanganuo, deni la nje Sh trilioni 4.1 na deni la ndani Sh trilioni 3.9.

Pia, katika hotuba yake akahimiza nchi tajiri duniani kupitia kundi lao la G20, kupanua mfumo wa pamoja wa kusimamisha au kupanga upya ulipaji madeni miongoni mwa nchi za kipato cha kati, wakati wa kipindi cha kujiponya dhidi ya janga la korona.

Rais Ruto, anafafanua kwamba katika nchi zinazoendelea, zimeelemewa sana na ulipaji madeni, hali inayohatarisha maendeleo, kutokana na ugumu unaozaliwa na janga la maradhi korona.

"Ninatoa wito kwa taasisi za fedha za kimataifa na jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka na kutoa vyombo vyote vya kifedha vilivyopo na kutoa ukwasi wa kifedha unaohitajika na kupata nafasi bora ya kifedha kwa nchi zinazoendelea kama Kenya," anatamka.

***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***

UCHUMI

# Yaliyojificha tatizo watoto wa mtaani na ombaomba

- Serikali yakiri limezidi, utaratibu unakuja
- Polisi kuanzisha msako mitaani, mabasi
- Makala awaandalia makao Kigamboni



Wahitaji katika sura mbalimbali wakisaka riziki kwa mbinu tofauti. **PICHA:MTANDAO**

**Na Maulid Mmbaga**

WATU ni msingi namba moja wa maendeleo, ndiyo nguvu kazi, ndiyo maana Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema ili Taifa liendelee linahitaji vitu vinne: Watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Lakini, idadi kubwa ya watu, inayozidi uwezo wa taifa ni changamoto inayogeuka kitendawili hasa wengi wao wakiwa ni wale wenye hali ngumu ya maisha na wanaoshindwa kumudu mahitaji yao ya msingi.

Ili kupata mahitaji yao, wapo wanaoamua kuishi mitaani na kutumia visingizio mbalimbali kwa mfano, uchunguzi unaofanywa na Nipashe jijini Dar es Salaam, unabaini kwamba wapo wanaosaka riziki kwa kuomba barabarani kwa udanganyifu.

Mfano, kusingizia maradhi ya kushindwa kumudu gharama za matibabu, kudanganya wana ulemavu, kutelekezwa na wengine kutumikishwa kuomba kama kibarua ambacho jioni hutakiwa kupeleka hesabu kwa tajiri.

Kuombaomba kugeuzwa njia ya kujiingizia kipato kumesababisha idadi kubwa ya watoto, watu wenye akili timamu na nguvu wa umri na jinsia zote kutoka maeneo mbalimbali kuzamia mijini ili kuomba, hasa Dar es Salaam, jambo linaloiamsha serikali na wadau kuingilia kati ili kutafuta ufumbuzi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu Dk. Dorothy Gwajima, wakati wa mkutano wa wadau wa ustawi wa jamii uliofanyika Dar es Salaam, hivi karibuni, anazungumza na Nipashe, akisema kitendo cha watu kutoa fedha barabarani na kuwapatia ombaomba hakiwasaidii badala yake kinakuza tatizo.

Anafafanua kuwa, endapo ombaomba atapatiwa fedha kila leo hataondoka barabarani bali ataendelea zaidi, akitoa wito kwa wananchi wanaotaka kuwasaidia kuweke utaratibu maalumu kama kupeleka misaada katika eneo lenye usimamizi maalum ili uwe na tija.

"Nafahamu kwamba kutoa kwa wahitaji ni suala la kiimani, ieleweke kwamba unapompa mtu fedha barabarani haujamsaidia kwani kesho utamkuta mahali palepale akiwa na shida ile ile na huenda dhamira yako njema ya kumsaidia isitimie," anasema na kuongeza:

"Kutoa fedha mitaani bila utaratibu ni kuongeza tatizo la ombaomba badala ya kulidhibiti, licha ya baadhi ya halmashauri kuwa na sheria ndogondogo zikiwamo za jiji la Dar es Salaam, kuna umuhimu wa kutunga sheria maalumu. Nawasihi kuacha tabia ya kutoa fedha kwa ombaomba."

"Tuje na utaratibu mzuri wa kusaidia watu hawa wakiwa mahali sahihi kwenye vituo vya ustawi wa jamii, tunao wahitaji, lakini tuwe na mfumo ambao utakuwa ni endelevu utakaokuwa na tija, ili tukiwachukua kule waliko tukawapeleka mahali panapofaa," anasisitiza.

Anakumbusha kuwa barabarani wanagongwa na magari, wanafanyiwa ukatili kama kubakwa na kulawitiwa, pia wanakoomba kunageuka eneo la kufanyia biashara haramu kama dawa za kulevya na wengine wanawatumia vibaya.

Pia, anashauri kuwa ni vyema kuwe na mpango wa kuwatoa ombaomba waliko na kuwaendeleza, kuliko kuwaacha kuumizwa na jua na mvua, kwa imani kuwa wanasaidiwa, jambo analolitaja kuwa ni kuongeza tatizo.

Anasisitiza kuwa hajazuia watu kuwasaidia wengine, ila anapendekeza kwanza kuwatambua wahitaji na kuwapeleka mahala ambapo watawahudumia kwa mpango maalum.

Anautaja utafiti wa mwaka 2021, uliofanyika Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza, na Iringa, uliobaini kuwapo watoto 5,732 kati yao wa kiume ni 4,583 na wasichana 1,149 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Anabainisha kwamba, bado jamii haioni ukubwa wa tatizo, kwa kuwa wapo wananchi ambao wanaendelea kuwaajiri kinyume na sheria, kuwasafirisha bila uangalizi na baadhi ya wazazi na walezi kutowajibika katika kuwalinda na kuwatunza watoto.

**JUHUDI KUDHIBITI**

Waziri anasisitiza kila mzazi na mlezi pamoja na jamii, atakayebainika kumruhusu mtoto kufanya kazi hatarishi na kukiuka haki zake atawajibika kisheria, huku akitoa wito kwa mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na maofisa wa ustawi wa jamii kulishughulikia suala hilo.

"Hawa watoto ambao tunawaona huku mijini, ambao wazazi na walezi mmewatelekeza, kila mmoja atafute utaratibu wa kumrejesha mtoto wake maana sisi tukimchukua tukajua ni wakwako utatusaidia mambo kadhaa, hivyo kuanzia sasa kila mtoto wa mtaani tutakayemrudisha ni lazima tumkute mzazi,mlezi wake ana namba ya taarifa ya polisi (RB) inayoonyesha kwamba mtoto alipotea," anasema na kuongeza.

Anaongeza: "Hatuwezi kuona watoto wanalala chini ya madaraja halafu pamoja na wadau wapo, huku wakisema kwamba wanatetea haki za watoto, ambao amewataka maofisa wa ustawi wa jamii na wadau mbalimbali kuja na mpango wa namna ya kutatua jambo hilo."

Aidha, anasisitiza kwamba mzazi ambaye mtoto wake hatakuwa nyumbani na akapatikana yeye akawa hana RB, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa kuhusika na uzembe na kutowajibika katika malezi.

"Mtoto amekushinda, suluhu sio kumtelekeza na wewe ukanyamaza ukalala, tunatangaza namba za ustawi wa jamii kila siku, piga tuma 'huyu ameanza kunishinda mnanisaidiaje? Tutajipanga na maofisa tutafanya kitu kujua kulikoni ili mtoto asikimbilie mtaani, huyu ni mali ya taifa," anasisitiza.

**MUONGOZO KISHERIA**

Sheria ya mtoto sura ya 13 inaelekeza mzazi au mlezi kuwajibika katika matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto na kwamba adhabu ya Shilingi milioni tano, kifungo cha miezi sita au vyote kwa

INAENDELEA UK.15

# Watoto mtaani, ombaomba mageuzi yao yako jikoni

INATOKA UK.14

pamoja vitatolewa kwa atakayekiuka sheria hiyo.

Waziri Gwajima, pia analiomba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mahakama kuchukua hatua kali dhidi ya wazazi na walezi watakaothibitika kisheria kukiuka kanuni za maadili ya malezi ya watoto, akikumbusha kuwa watoto wa leo ndiyo wazazi wa kesho, hivyo wasipochukua hatua sasa watakuwa na taifa lisilokuwa na wananchi wanaowajibika.

Pia, anawaagiza maofisa wa ustawi wa jamii ngazi ya mikoa kuwasimamia wale wa halmashauri ili wafanye ufuatiliaji kwa kushirikiana na polisi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 20 na 86 cha sheria ya mtoto.

Analitaka jeshi hilo kukagua mabasi na malori katika vituo na maeneo yote yanakopita, ili kama kutakuwa na watoto waliojificha wasaidiwe , akibainisha kuwa taarifa zianaonyesha kwamba ndiyo usafiri mkuu unaotumika na watoto wa mitaani kufika maeneo waliko kwa sasa.



**DAR -ES -SALAAM INATISHA**

Waziri anasema, ombaomba ni suala mtambuka likihusisha wazee waliotelekezwa, watoto wanaowaongoza watu wazima vipofu na vimwendo kupita mitaani kuomba na kwamba tabia hiyo imekithiri kwenye miji mikuu hasa Dar es Salaam.

Gwajima anasema, katika kushughulikia tatizo hilo mwezi Machi mwaka huu aliunda kikosi kazi cha watu 10 akiwamo yeye na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Amos Makalla, kuandaa mkakati maalumu wa kumaliza tatizo la watoto wa mtaani.

Anabainisha kwamba, kikosi hicho pia kimeandaa mkakati utakaohitaji gharama kuutekeleza, akiomba wadau kushirikiana katika utekelezaji na kutaka kila mmoja aone ashiriki.

Amos Makalla, akizungumzia suala hilo anasema watatatua changamoto ya ombaomba na watoto wa mtaani na eneo limetangwa Kigamboni, ambalo litatumika kujenga kambi ya kuwatunza yenye huduma mbalimbali muhimu.

"Jitihada za serikali ni kuona makundi maalum tunayatambua. Watoto wa mitaani na ombaomba, mkakati ni kuwajengea mazingira mazuri na kuwapeleka shule, anayetakiwa kupata ujuzi na mahitaji ya kuwezeshwa kumudu maisha yake," anasema na kuongeza;

"Tumekubaliana na wizara kuwapo na kituo, tumetafuta eneo na mpangokazi umetengenezwa na wizara, Dar es Salaam tunahakikisha kwamba watoto wa mitaani na ombaomba tunawajengea mazingira mazuri ya kuwatambua na kuona nani anafanya nini kwa wakati gani na umri gani."

Anatoa wito kwa wenyeviti wa seriakali za mitaa ambapo ndiko makazi mengi yalipo, washirikiane kubaini na kutoa taarifa, akieleza kuwa anaamini uongozi huo wana uwezo wa kubaini na kutoa taarifa ili kamati za ulinzi na usalama kwa kushirikiana na ustawi wa jamii waweze kuvunja mtandao wa watu wanaowaleta watu kuwatumikisha mtaani.

**MIKAKATI KIPOLISI**

Kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Mudathiru Makora, ambaye pia ni mjumbe wa kamati maalum ya kitaifa inayoweka utengamano wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani, anasema polisi itachukua hatua kwa wale ambao watabainika kuwasafirisha watoto kuwatumikisha.



Anabainisha kuwa, katika kila kituo cha mabasi na stesheni za treni wameweka maofisa watakaokuwa wanakagua magari na kujiridhisha kuwa hakuna mtoto aliyejificha ili kuingia mijini.

"Wako ambao kwa umri watahitaji kurejea kwenye familia zao na pale tutakapowarudisha Jeshi la Polisi linahimiza wazazi kwamba wawe na RB, kwamba mtoto hakuwapo nyumbani uliripoti wapi, tukikuta mtoto ameletwa mpaka kwenye himaya yako halafu hakuna ripoti yoyote utawajibika kupitia sheria ya mtoto," anasema Makora.

Anasema, hakuna mtaa unaozaa watoto ila kinachoonekana kwa sasa ni matokeo ya baba na mama aliyeshindwa kutimiza wajibu wake.

**500 WANASURIWA**

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Baba Watoto Mgunga Mwamnyenyelwa, anasema wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kwamba hadi sasa wamewachukua zaidi ya 500 wa kike na wakiume na kuwapeleka kwenye vyuo vya ufundi (VETA), ili kuwapatia elimu ya ujasiriamali na ujuzi kwa miezi sita utakaowasaidia katika kujikwamua kimaisha na kutoka katika maisha ya mtaani.

"Tumefanya kazi na watoto wa mtaani kwa muda mrefu lakini ni kama tunatwanga maji kwenye kinu, unakuta tunawarudisha 20 ukirudi unakuta wengine wamekuja, hawa uliowabeba hata kabla hawajafika unapowapeleka wengine wameshuka tena kwenye kituo cha mabasi cha Magufuli Mbezi jijini Dar es Salaam, hivyo sheria ichukue nafasi yake mzazi asiyetimiza wajibu wake awajibishwe," anashauri Mwamnyenyelwa,

Aidha, anatoa wito kwa sheria ya mtoto ya 2009 ifanye kazi, akieleza kwamba mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam anapata shida ya kukamata na kuwarudisha watoto wa mitaani na ombaomba lakini baada ya muda mfupi wanarudi na anabainisha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watoto wanaowahudumia wanatoka mikoani.

Anabainisha kuwa watoto wengi wa mitaani walioko Dar es Salaam wanatoka, Bukoba, Geita, Mwanza na Dodoma, huku akitoa wito kwa serikali za maeneo hayo kuchukua hatua dhidi ya wazazi na wazembe wasiotekeleza wajibu wao, ili kukomesha tatizo hilo.

Rashidi Abdalah, mkazi wa Dar es Salaam anayeendesha shughuli zake Posta Dar es Salaam, anadai kwamba kumekuwa na tabia kwa baadhi ya madereva wa bajaji walemavu ambao hufanya shughuli zao asubuhi na inapofika mchana muda ambao abiria sio wengi huacha vyombo vyao vya usafiri na kwenda kukaa mahali na kuanza kuomba na inapofika jioni hurudi tena kazini.

UCHUMI

MRADI WA NYUMBA WATUMISHI UMMA

# Bosi Dk. Msemwa achanganua wanachokitoa, aliyeuziwa afunguka kilichomo maisha mapya

- Mpango maalumu wa vipato vidogo waja
- Cha walimu wa mazingira magumu chaja

**Na Beatrice Moses**

"Kwangu kati ya nyumba na gari, nilichokipa umuhimu wa kwanza ni nyumba, hivyo nimeshasikia aina tofauti za mkopo ikiwamo wa fedha ambayo pengine ningeweza kuitumia kununulia gari, lakini mimi nilichagua mkopo wa nyumba ni nzuri inanipa utulivu kwa kiasi fulani," anasema Mwalimu Prisca Kisha

Mwalimu Prisca anaiambia Nipashe, kwamba umuhimu wa kumiliki nyumba iliyokamilika, hasa zilizojengwa kwenye maeneo yaliyopimwa na yenye huduma za kijamii, yeye anajivuna amefanikiwa kuwa miongoni mwa wamiliki, baada ya kuingia mkataba na Watumishi House Investment (WHI), ambayo ni taasisi ya serikali inayohusika na kumilikisha watumishi.

Kauli ya Mwalimu Prisca, inafikirisha kuhusu watu kadhaa ambao wamejikuta kwenye wakati mgumu kumiliki nyumba, baada ya kujenga kwenye maeneo ambayo hayakupimwa, hivyo wakaishia kubomolewa huku wakiachwa na madeni ya mikopo ya fedha walizojengea, wengine wamejenga kwenye maeneo yaliyo mbali na huduma za kijamii hivyo wanaishi maisha yenye usumbufu ambao wangeweza kuepuka.

"Japo kipato changu ni cha kati, niliamua kufanya uamuzi mzuri, baada ya kusikia WHI, wanautaratibu wa kukopesha nyumba maeneo tofauti nchini kwa kuwa nipo Morogoro, nilikwenda kutazama na nilivutiwa na jinsi zilivyojengwa na eneo ilipo,gharama yake ni zaidi ya shilingi milioni 50, hivyo nikaingia mkataba ili niimiliki," anasema Mwalimu Prisca.

Anabainisha kuwa, kuanza kuishi alijisikia anapata amani na utulivu kwa kuwa, nyumba hiyo ilikuwa imekamilika kila eneo, hali ambayo ilimsaidia kumpunguzia mawazo aliyokuwa anayapata wakati alipokuwa anajenga nyumba yake mkoani Kagera.

Mwalimu huyo anasema, kuwa yeye ni mwalimu mzoefu wa miaka 20, ana kipato cha kati, hivyo kuna wakati alijaribu kuanza kujenga nyumba mkoani Kagera, lakini hakufanikiwa kuikamilisha, kutokana na mambo mbalimbali aliyoshindwa kuyazuia, hivyo akawa katika hali iliyompa kero kubwa.



" Fikiria unakopa fedha, unatumia kujenga nyumba haikamiliki, huku deni lako unapaswa kulipa. Pia, unaweza kukutana na fundi ujenzi asiye mwaminifu au anajenga kwa ubabaishaji, anakusababishia hasara. Lakini, nyumba iliyokamilika unakatwa deni lako huku ukiwa unajua faida ya kulipa," anasema.

Kwa upande wake Gaudensia Chale, ni Katibu Muhtasi kwenye taasisi mojawapo ya serikali nchini, anasema kuwa maono ya kumiliki nyumba baada ya kupata taarifa za uwepo wa WHI alimshirikisha mume wake anayemtaja kwa jina, Godfrey Mwaitolola.

Anasema, jambo muhimu walilokubaliana, ni kuhakikisha wananunua nyumba ambayo wana uwezo wa kumudu gharama za kulipia, kulingana na kipato chao mara baada ya taratibu za kuuziwa nyumba zilipokamilika, hivyo walijiwekea mipango ya kuhakikisha wanakuwa na uwezo wa kulipia fedha, ambayo watakuwa wamekubaliana na WHI.

Gaudencia anakili kwamba, kuna tofauti kubwa kati ya mtu akinunua nyumba, hasa ikilinganishwa na masharti nafuu ya makato, kwamba siyo fedha taslimu, kwa kuwa ndani ya muda mfupi baada ya kukamilisha taratibu zote, waliruhusiwa kuanza kuishi ndani, eneo la Gezaulole, Kigamboni Dar es Salaam.

Gaudencia anaamini, uamuzi wake ulisaidia kukwepa usumbufu wa baadhi ya mafundi ujenzi iwapo angejenga nyumba yake, hivyo kununua nyumba WHI, ilitokana na nia aliyokuwa nayo ya kupata nyumba katika eneo linalofikiwa na huduma zote muhimu za kijamii huku akiwa ni mtumishi wa kawaida wa serikali .

Mama huyo anadema, alishawishika kuingia kwenye mipango ya kununua nyumba, badala ya kununua kiwanja na kujenga mwenyewe, akifikiri jinsi ingechukua miaka mingi kuanza ujenzi mpaka kukamilisha.

"Nilivutiwa kupata nyumba nzuri za kisasa na zenye ubora kwa bei nafuu kuliko kama ningeijenga mimi mwenyewe. Pia, upande wa malipo kuona mteja una uhuru wa kuchagua unataka kufanya malipo kwa kutumia njia ipi kati ya zile zilizoelekezwa, " anasema.

"Kwa ujumla sikupata changamoto yoyote, hii ni kutokana na mipango mizuri tuliyojiwekea hasa ya kununua nyumba kulingana na kipato, gharama yake ni shilingi milioni 58, napaswa kuilipa kwa miaka 15,"

**BOSI MKUU WHI**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WHI Dk. Fred Msemwa, anasema kuwa jumla ya nyumba zilizojengwa ndani ya miaka minane ziko 981 na kati yake, 591 zimeuzwa kwa watumishi wa umma wa kada mbalimbali, wakiwamo walimu, makatibu muhtasi na maofisa wa kati na waandamizi serikalini.

Anasema, nyumba hizo zimeuzwa kwa mkopo wa bei tofauti kulingana na ukubwa wa nyumba husika, bei ikianzia shilingi milioni 38 na ya juu ni shilingi milioni 85. Hata hivyo, anasema baadhi ya watumishi wa umma kutokana na kipato chao kuwa kidogo, wameshindwa kujitokeza kukopa.

"Kwa kulitambua hilo, WHI ina mpango wa aina mbili wa kwamba,kwanza kwa kushirikiana na serikali kupitia Mamlaka ya Elimu TEA, imetekeleza mpango wa makazi ya nyumba 186 za walimu kwenye sekondari za kata zenye mazingira magumu kwenye mikoa 19," anasema.

Anautaja mpango wa pili, ni kwamba WHI, kusanifu nyumba za gharama nafuu zitakazotosheleza mahitaji ya wafanyakazi wa kina cha kati, kufanya uamuzi wa kununua ili wenye uhitaji wa kumiliki nyumba nao watimize ndoto zao.

" Tutafanya hivyo kwa kuwa tumebaini kuwa japo tunaanzia shilingi milioni 38, wapo ambao wanashindwa kujitokeza kununua. Hivyo, ili kujenga zenye gharama nafuu tunawasiliana na halmashauri zitoe maeneo ambayo yana miundombinu muhimu, huko tutajenga nyumba zenye vyumba vitatu vya kulala sebule na stoo," anasema.

Pia, WHI inakusudia kuangalia utaratibu wa ulipaji kwa watumishi wa kipato cha kati ili waweze kumudu. Hapo anafafanua:" Kwa sasa tumeanzisha mpango wa mpangaji mnunuzi. Mhusika anaanza kwa kuwa mpangaji kadri anavyomudu kulipa.

"Mkataba unawekwa wa kumuwezesha kulipia kwa miaka miwili hadi 15 inategemea na vyanzo vyake vya fedha akifanikisha anakuwa mmiliki halali."

Dk. Msemwa anasema, kwa sasa wawaaundia mfumo waajiriwa wa sekta ya umma na binafsi, wawe na mahali pa kukimbilia wanapohitaji kupata nyumba, akatoa mfano ni jengo lililopo Magomeni Dar es Salam, ambako watu wameuziwa nyumba eneo ambalo ingekuwa ngumu kwa mtu wa kipato cha kawaida kumiliki makazi.



Nyumba za mikopo ya watumishi wa serikali katika sura tofauti. **PICHA ZOTE: BEATRECE MOSES.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Nani yuko, nini kiko nyuma ya Panyarodi?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WANAJULIKANA kama Panyarodi, Komandoyoso, Watu wa Kazi, Panyabuku, angalau kwa sasa wanaweza kuwa ni hao. Ni makundi ya vijana wadogo tu wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 17.

Ni wasumbufu na hatari sana katika jamii. Wanavamia majumba usiku na mchana na kufanya uharibifu wa mali na maisha, wanaiba, wanapora na kujeruhi watu hata kuua.

Si wa kubeza na si wa kudekeza, ni wa kupambana nao ili kudhibiti nyendo zao hatari kwa mustakabali wa mtu mmoja mmoja, lakini hata kwa taifa kwa ujumla wake.

Wanatembea makundi ya watu zaidi ya 30 kwa wakati mmoja wakiwa wamesheheni silaha za jadi, kwa maana ya mapanga, marungu, nyundo na hata nondo, kwa ajili ya kuvunja milango na kushambulia yeyote mpinzani wa azma yao ya kupora.

Kwa kauli zao, wanasema wana viongozi ambao huwatuma kuvamia mahali na kupora kinachoweza kuporwa na kisha kwenda kuuza na kugawa na kinachopatikana kwa maana ya fedha, kuanzia Sh 50,000 na kuendelea.

Awali walichukuliwa kwanza kwamba ni vijana wadogo wanaokwenda kwa miguu na kufanya uhalifu, lakini hivi karibuni wanakamatwa wakiwa na gari aina ya Toyota Noah, wamesheheni silaha zao hizo zilizotajwa hapo juu, wakielekea kutekeleza uhalifu maeneo ya Makongo, Dar es Salaam.

Wao wanakiri kuwa wengi wao ni wahitimu wa darasa la saba waliofeli na kukaa majumbani kwa kukosa cha kufanya, hivyo kutafuta njia za mkato kujipatia kipato. Bahati mbaya mkato huo unakata maisha ya watu na mali zao.

Wanakiri pia kuwa, baadhi yao walipata kuwa kifungoni magerezani kwa uhalifu. Hilo limethibitishwa pia na uongozi wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam.

Ukiwauliza, wanakwambia wanatoka jela kwa sababu wanaweza 'kuzungumza' ,na baadhi yao hukamatwa bila vielelezo, na hivyo kutoka kiulaini bila kuchukuliwa hatua zozote na hivyo kurejea uraiani kuendelea na uhalifu wakijua watachomoka tena kwa njia hizo hizo.

Wafanywe nini? Hilo ni swali ambalo limekuwa likijibiwa kwa hisia tofauti na baadhi ya watu. Wapo wanaotaka wamalizwe kwa kuuawa. Wapo wanaotaka haki za binadamu zizingatiwe kwa kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria na haki kuonekana imetendeka.

Lazima hisia tofauti ziwepo, kwani kuna waliokwishakumbana na kadhia ya madogo hawa, pia wapo ambao hawajawahi hata kuwasikia achilia mbali kuwaona, wakifanya matendo yao hayo. Bila shaka ukiuliza familia ya mwanafunzi wa uandishi wa habari aliyeuawa na watoto hawa, jibu litakuwa kali.

Lakini, hata kwenye vitabu vya Mungu, kuna maandiko yanasema "auaye kwa upanga atauawa kwa upanga! " Vikifuatwa hivyo, bila shaka jibu la wamalizwe litakuwa halal bin haki, bika kujali kinachoitwa haki za binadamu.

Mwaka 1978 kwa waliokuwa wamezaliwa na kujitambua wakielewa kinachozungumzwa na viongozi, watakumbuka pale Diamond Jubilee, Dar es Salaam, siku Rais Mwalimu Julius Nyerere alipoutangazia Ulimwengu, kuhusu nia, sababu na uwezo tulivyokuwa navyo Watanzania katika kukabiliana na uvamizi wa majeshi ya kiongozi dhalimu wa Uganda wakati huo, Nduli Iddi Amin Dadah.

Mwalimu alilazimika kutoa tamko hilo, baada ya kusikia majeshi hayo yamevuka Mto Kagera na kuvamia mkoa wa Ziwa Magharibi (sasa Kagera) na kufanya uharibifu mkubwa, ikiwa ni pamoja na kuua watu. Unadhani alichokitangaza Mwalimu Nyerere kilikuwa cha kwenda kuimba nyimbo na kuvuna kahawa? La hasha!

Kilikuwa ni cha kwenda kulipiza kisasi kwamba walishaua kwa upanga nasi tukawaue kwa upanga huohuo. Hapakuwapo ametupiga shavu hili, tunamgeuzia lingine. Hapana! Ilikuwa ni kukabiliana nao na ndicho kilichofanyika na matokeo yakajulikana mwaka mmoja baadaye.

Sasa tunapaswa kujiuliza kwanini 'panya' hawa wanatamba? Tutafakari ni nani yuko nyuma yao mpaka kutumia Noah kufanya mashambulizi yao. Tumekaa na makundi ya bodaboda kuzungumza nayo? Iweje 'panya' waingie majumbani na kupora pikipiki na kuendesha na kutokomea?

Nani wa kulaumiwa, wazazi? Walimu? Serikali? Au mfumo wetu wa elimu unaowarudisha majumbani baada ya kufeli na kukosa cha kufanya na badala yake kukalia kubeti na kucheza kamali na bahati nasibu? Je, tukiwakamata tuwaue kweli au tuwaache? Tukiwaacha tuwapeleke wapi ili wasirudie uovu? Alamsiki!

BIASHARA

# Madalali madini wajisafisha kwa ajenda atakayenaswa akitorosha watamtenga

## • Leseni yake nayo wanamnyang'anya

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

NI kipindi ambacho jamii inaamua kuchambuana, aliye na mchele na pumba ajulikane, katika kile wanachokitaja kwamba kujiengua na lawama za uhujumu uchumi, kupitia bidhaa wanayohusika nayo madini.

Hapo wanaamua kujisafisha, kwa kila mmoja sasa mzigo wake katika uhujumu huo, kwani dhamira walio nayo sasa, ni kufanya biashara kwa mujibu wa maelekezo ya leseni zao.

Katika hilo, Chama cha Mabroka wa Madini Tanzania (CHAMMATA) kimeamua kujipanga upya kukabiliana na madalali wenzao wanaojihusisha na utoroshaji madini kwa njia za panya na kuendelea kuisababishia serikali kukosa mapato yake kupitia madini.

Katika kikao chake, CHAMMATA inasema ni vitendo vinayofanywa na madalali wenye mitaji midogo, wanaotumiwa na wafanyabiashara wakubwa wa madini kupitisha mizigo ya madini kinyemela na pale wanapokamatwa na vyombo vya dola, huwa wanakanwa na wafanyabiashara, hata wanaishia kufilisiwa tu.

Katika mjadala wao wa kukosoana madalali hao, mambo ambayo yamekuwa yakiwachafua madalali mbele ya serikali wakionekana wote wanajihusisha na hujuma hizo, huku wakikiri Tume ya Madini imetengenezea utaratibu mzuri wa kununua madini, kwa kuanzisha masoko maalumu kwenye mikoa yote inayojihusisha na uchimbaji madini.

Ilielezwa, Kanda ya Kaskazini, hususani mikoa ya Arusha na Manyara, wachimbaji madini ya Tanzanite wanadaiwa kujihusisha na utoroshaji madini, lakini kupitia ushirikishaji viongozi na wachimbaji, wakafanikiwa kutokomeza vitendo hivyo na biashara sasa kufanyika kwa ufanisi .

Chama hicho kinadai, awali hawakuwa na wawakilishi wa kuwasemea changamoto zao na badala yake waliwakilishwa kitaifa na vyama vilivyopo, ikiwamo Chama cha Wachimbaji Wadogo mkoani Shinyanga (SHIREMA), wakisisitiza msimamo wao sasa, hawatakubali na baadhi yao waendelee kuchafua tamaa zao.



Makamu Mwenyekiti CHAMMATA Taifa, Bahati Damiani, akipokea kadi ya uanachama wa chama hicho kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya, ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa kadi hizo. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**MWENYEKITI AZUNGUMZA**

Jeremia Kituyo, Mwenyekiti wa CHAMMATA, anasema baada ya chama kusajiliwa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, wamekuja na mikakati mipya kuwakabili madalali wanaojihusisha na utoroshaji madini, kwa lengo la kukwepa kodi za kitaifa.

Kituyo anasema, kodi wanazotozwa kupitia madini wanayokusanya ya asilimia saba ya mzigo unaopatikana, sehemu yake inarejeshwa kwa wananchi kugharamia miradi ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za msingi na sekondari, vituo vya afya na maji hivyo, hatakubali chama kuhusishwa kwenye tuhuma hizo.

Anafafanua, dalali wa madini atakayekamatwa na kuthibitika anatorosha madini kwa njia za panya kwa lengo la kukwepa kodi ya serikali, atanyang'anywa leseni na kutojihusisha na biashara za ununuzi wa madini kwa kuwa ni jukumu lao kutokomeza vitendo hivyo.

Hapo anatoa tahadhari kwa mkoa wa kimadini utakaothibitika kunaswa na vyombo vya dola wanatorosha madini, viongozi wake watawajibika kisheria, kwani watakuwa wameshindwa kusimamia majukumu yao ipasavyo.

**KUKAMATWA MADALALI**

Kituyo anadema, madalali wa madini wanakamatwa hovyo katika sehemu za biashara, hali inayowaondolea uaminifu kwa wateja wao na hata wanapowafuatilia vituo vya polisi wakati mwingine hawawakuti na kuwafanya kuingiwa na shaka, ila hata wanapowakuta, wananyimwa nafasi ya kuzungumza nao.

"Hatukatai pale tunapokosea tusikamatwe na kuchukuliwa hatua, ila tunapokamatwa tusidhalilishwe mbele ya wateja wetu, kwani inatuondolea uaminifu na kuonekana matepeli. Hiyo ndio sababu inayotukosesha mzigo na kushawishika kuingia kwenye uovu," anasema Kituyo.

Katika hilo, anawataka madalali wenzake kuacha tabia ya kufanya biashara na wageni kutoka nchi za jirani, ambao hawajafuata taratibu za kuingia nchini, kwani sheria zinawataka kuwa sehemu ya madalali wa madini na atakayebainika atawajibika.

Analalamika kwamba kufanya hivyo ni kuwanyima fursa ya ajira vijana wa Kitanzania wanaoweza kufanyabiashara hizo na kuwasihi kuajiri walio waaminifu katika ofisi zao, ili wasiwaingize katika kashfa chafu kuwaeungua na matatizo ya wizi, kwa sababu ya vijana hao wasiokuwa wadilifu.

**WATAALAMU**

Kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini Kahama, Mhandisi, Jeremillah Hango, anasema kuna tatizo kubwa la utoroshaji madini kwa madalali ambao sio wadilifu.

Hivyo, anaungana nao kusisitiza utaratibu wa kuwapoka leseni wale wanaojihusisha na vitendo hivyo kinyume, utasaidia kufata nidhamu mbaya kwa tabia hiyo.

Anasema, alichobaini ni kwamba mpaka madalali wa madini wanatorosha madini kwa njia za panya, lengo ni kukwepa kodi na wafanyabiashara wakubwa ndio wanaowatumia kupitisha mali nyingi na pale wanapobainika, wanawakana na serikali kuwataifisha mali walizo nazo muda mrefu, ikiwamo mitaji.

"Ni kitendo cha ajabu kutumia muda mwingi kukusanya mzigo kwa fedha nyingi tena kuna wakati mkopo, unapopata kilo moja unapata tamaa ya kukwepa kodi nasisi tunapokukamata tunakutaifisha kila kitu mpaka kile ulichokusanya," anasisitiza Hango.

Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, Salum Rashidi, anasema sekta hiyo ina mwingiliano wa wageni wengi kutoka mataifa mbalimbali ikiwemo India, Zimbabwe, Afrika Kusini na China, hivyo wanaposhirikiana nao wahakikishe wanakuwa na vibali halali vinavyowaruhusu kufanya shughuli hiyo.

Anasema, wageni wanatakiwa kufuata utaratibu wa kuwa na vibali vya makazi ya muda na kazi, kinyume chake ni kwamba, kwani bila ya kuwa na vibali hivyo, anakuwa amevunja sheria nchini.

Mwenyekiti wa Soko la Madini Kakola, katika Halmashauri ya Msalala, Baraka Lazaro, anasema wizi wa madini katika eneo lake umepungua kwa kiasi kikubwa, baada ya kuanza kuwachukulia hatua za kuwaondoa sokoni wanaobainika na vitendo vya namna hiyo.

Anasema, changamoto wanayokutana nayo ni wakati wa kuhuhisha leseni ya ununuzi wa madini, wamekuwa wakiwekewa vikwazo vingi ikiwamo kuwasilisha taarifa za fedha hali ambayo inawakatisha tamaa ya kufanya biashara hizo.

Dalali Damian Makaya, anaiomba serikali kuwaruhusu kuuza madini nje ya mikoa wanayotoka, kwani kuna wakati masoko yao wafanyabiashara wake wanakosa fedha za kununua madini na kuruhusiwa kununua madini kutoka viwanda vya kuchenjua madini ili waendelee kukuza mitaji yao.

**DAS WA KAHAMA**

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya, anaupongeza uongozi wa chama hicho kuanza kazi kwa kuwashughulikia wanachama wake watakaojihusisha na utoroshaji madini, huku serikali ikiandaa mazingira bora ya biashara.

Ndanya, anawataka kuanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani madini, kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali kuondokana na kuuza madini ghafi na itawafanya kukuza mitaji yao na kuwaajiri vijana wengi walioko mitaani.

Ndanya anasema, madini yanachimbwa nchini na kuuzwa nje ya mipaka na baadaye kutuuzia bidhaa zinazotokana na madini kwa bei kubwa, huku inawezekana wafanyabishara wetu kuungana na kutengeneza viwanda vidogo vya kuongeza thamani madini ghafi.



Mwenyekiti wa Chama cha Madalali wa madini Tanzania, mkoa maalumu wa kimadini Kahama, Daniel Masanja, akitoa taarifa ya chama kwa wanachama wake..

UCHUMI

MILA AINA YAKE KIJIJINI...

# Mama asimulia kifo cha mume wake kilivyoenda na mtoto kumpora urithi

- Mpangaji shemeji, mwana atekeleza
- Ikaanzia godoro, shamba, nyumba...
- Aambulia ekari mbili, 38 zaondoka
- Serikali wilaya yashituka, inafuatilia

**Na Neema Hussein, aliyekuwa MLELE**

KATIKA kijiji cha Mapili, kata ya Ilela katika Halmashauri ya Mlele mkoani Katavi, inaagukia kashfa ya kupata tukio lililopitwa na wakati, mahasusi katika ukatili wa kijinsia.

Hiyo ni aina ya mambo ambayo siku chache zilizopita, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amelikemea vikali katika dhana ya ukatili wa kijinsia.

Inafafanuliwa, mila na desturi katika baadhi ya familia za kijiji hicho, inamzuia mwanamke kuolewa na kuishi kwenye nyumba ambayo walijenga na mume wake pindi mume itatokea amefariki.

Pia, mwanaume wa kijiji hicho kupitia mila hiyo, inamruhusu kuoa na kuishi kwenye nyumba ambayo walijenga na mke wake pindi mke amefariki.

Faustina Daud, ni mwanamke anayeishi kijijini hapo akiwa na simulizi binafsi kwamba, hayo yamemkuta hata kupatwa na misukosuko pindi mume wake alipofariki mwaka 2010.

"Niliishi na mume wangu miaka 20 baada ya hapo mume wangu alifariki mwaka 2010 akaniachia watoto sita, watoto watano nilizaa nae, ila mtoto mmoja alikua ni wake ambaye alizaa nje.Basi mimi niliishi na hao watoto wote sita na walikuwa wanasoma, nilikaa nao kwenye ile nyumba tuliyojenga mimi na mume wangu.

"Baada ya miaka mitatu kupita tangu afariki, mume wangu nilipata mwanaume mwingine ambaye alinitafuta, nilimkubalia kwa sababu watoto wengine walikuwa bado wadogo ili awe ananisaidia kutunza hao watoto.

"Nilikuwa nikiishi naye pale nyumbani. Baada ya hapo, walisikia wale ndugu zake na mume wangu. Sasa yule mtoto wangu wa pili ndio alichukua mavazi ya baba yake baada ya msiba. Walimchukua yule mtoto wangu wakaenda kufanya kikao naye.



Faustina Daud, mkazi wa kijijini Mapili, Wilayani Mlele Mkoa wa Katavi. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

"Baada ya kufanya kikao, walimwambia hivi inatakiwa umfukuze mama yako pale nyumbani na umnyang'anye godoro na kweli yule mtoto wangu alikuja akaniambia 'mama nataka unipe godoro.'

"Sikumpa! Ila alisubiri nimetoka, akaingia ndani akachukua godoro. Basi nilivyorudi nikakuta yule mtoto ameishachukua godoro, mimi nikaendelea kulala chini nikiwa na watoto wengine," anaeleza Faustina.

Anasema, baada ya hatua hiyo mtoto akaanza kuchukua mashamba yaliyoachwa na baba yake akiendelea na simulizi: "Aliendelea kufanya umiliki wa mashamba ya mume wangu aliyeacha ekari kama 40.

"Yule mtoto amechukua mashamba karibuni nusu nzima, mimi amenipa ekari mbili tu, sehemu zingine zote ameuza akatumia hela yote peke yake bila ya kuwapa hata watoto wenziwe.

"Hata hizo ekari mbili mimi kuzipata, ni kwa sababu nilienda kwa Ofisa Mtendaji Kata, kulalamika kwaiyo, aliiona ile barua kwa mtendaji wa kata, akanijia saa 12, akaniambia 'ulikuwa umeenda baraza la kata kunishtaki, aya twende ukachukue shamba unalolitaka' Ndio akafika akaniambia chukua ekari mbili.'

Anasema, akatishiwa iwapo angechukua hatua za kisheria dhidi ya mwanawe, wangemlipiza kisasi. Hivyo akagopa kusonga zaidi hatua za kisheria.

Faustina anasimualia kwamba baada ya hapo, akajikua anafukuzwa kwenye nyumba hiyo, akidaiwa kuwa anaitumia kwa tabia mbaya.

"Nyumbani walinifukuza wakasema unaanza kuleta wanaume hapa hapa sio sehemu ya kukutana na mwanaume hapa. Nenda ukatafute sehemu nyingine, kwa hiyo niliondoka mimi na watoto wangu wale wengine watano. Huyo mtoto aliyenifukuza ni wangu kabisa," anatamka, akifafanua akimzaa kabla ya kuolewa na marehemu.

Anadai baada ya kwenda kulalamika kwa Ofisa Mtendaji wa Kata, alikosa msaada stahiki, huku ndugu wa mumewe wakimpa vitisho iwapo angeenda kishitaki katika Baraza la Kata.

"Maisha yangu kwa sasa sio mazuri sana, japokuwa nimejenga, ila nimejenga kwa msaada wa ndugu zangu, huyu alinipa bati mbili, huyu tofali huyu hiki hadi nyumba ikakamilika ndio naishi hapo kwa shida, hivyo hivyo na watoto. Sijaolewa kwa sasa, yule mwanaume tuliachana....

"Mbona hata humuhumu kijijini mimi ninawaona kinamama waliofiwa na waume zao na kuachiwa mali kama vile nyumba, mashamba na wanayamiliki wenyewe, watoto wako chini yao? Ila mimi 'nimepigwa kadi nyekundu' kabisa na yule mtoto kupitia wale ndugu zake mume wangu." anasema

**USTAWI JAMII**

Finner Soka, ni Ofisa Ustawi jamii katika Halmashauri ya Mlele, anayeiambia Nipashe hana taarifa za tukio hilo, akiwa na ufafanuzi wa msimamo wake:

"Tumelisikia hapa. Kama serikali tutalifuatilia kujua ni nini hasa kilisababisha mpaka mtoto akamfukuza nyumbani na maisha yake kwa sasa yakoje, ili tujue tunamsaidia vipi kiserikali.

"Tunaweza tukamuunganisha na vikundi akapata mikopo kupitia maendeleo ya jamii kwa Mkurugenzi (DED), akaendelea kujikimu, lakini hilo suala la nyumba na mashamba tutalifuatilia na ikiwezekana lifikishwe kwenye vyombo vya sheria, mahakama iamue.

"Kama alichuma mali na mume wake kwa miaka 20 'automatiki' zile mali ni za kwake na watoto, haiwezekani mtoto akatoka tu akaenda kumfukuza," anaeleza Finner.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlele, Theresia Ilafay, alipoulizwa kuhusu suala hilo, akawajibu: "Kwa kesi (tukio) moja kama hilo ofisi iko wazi na kuna wataalamu, kuna wanasheria wa halmashauri nina maafisa watendaji wa kata na vijiji.

"Tunaendelea kuwajengea uwezo namna ya kusolve (kutatua) hizi kesi, lakini tuna mamlaka kama mahakama, tuna mamlaka ya polisi na wao wana jukumu la kufanya kuhusu hayo."

Mkurugenzi huyo anatumia wasaa huo kumkaribisha ofisini mama huyo na wananchi wote, endapo kuna yeyote anayenyanyasika, atahudumiwa kwa ajili ya kuwanyooshea njia watu wanaonyanyasika.

BIASHARA

# SHUHUDIA UTAPELI WA KISOMI KUPITIA PENZI NDANI YA UHUSIANO MTANDAONI

Ni ajabu, wahalifu wa Nigeria wanavyotapeli wakijifanya wanawake warembo mitandaoni. Kunakuwapo mteja mwanaume na msichana anayevutia anayezungumza naye mtandaoni kwa jina Gingerhoney, mwanamitindo ambaye picha yake wasifu unamuonyesha amelala kitandani kwake.

Mteja anafikiri Gingerhoney yuko karibu, lakini hajui kwamba yeye ni mwanaume aliye mbali, nchini Nigeria. Wanaume kote ulimwenguni kote hulipa mamia ya Dola za Marekani kwenye tovuti za watu wazima, ili kupiga gumzo na kile wanachofikiri nao mabinti wa kuvutia.

Ushahidi wa miezi kadhaa ulifichua oparesheni ya kimataifa dhidi ya wasifu huu feki, kutoka Uholanzi, Marekani hadi Nigeria.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu wa Nigeria Abiodun (si jina lake halisi) ni mmoja wa wasimamizi wengi wanaotumia wasifu bandia kwenye tovuti za uchumba zinazomilikiwa na kampuni ya Uholanzi.

Abiodun, hubadilisha wasifu katika akaunti feki anazosimamia kwenye tovuti hizi, lakini kila wakati anajidai msichana mzungu wa kuvutia.

Kwenye tovuti, amekuwa mwanamitindo mwenye umri wa miaka 21 aliyevalia nguo ya rangi ya waridi iliyozungushwa kiunoni mwake kwa njia ya kuvutia.



Sehemu ya mambo yanayojitokeza ndani ya tovuti hiyo ya kitapeli. **PICHA: MTANDAO.**

Sio Abiodun, pekee aliye na uwezo wa kufikia wasifu wa Gingerhoney - wasimamizi wengine wengi hudhibiti saa nzima kwa zamu.

Wasimamizi kama vile, Abiodun hutumia zana ya kina ya ramani kughushi eneo la Gingerhoney hadi umbali wa kilomita 50 kutoka kwa mteja.

Mteja analipia mazungumzo haya na anapewa matarajio kukutana naye.Ingawa tovuti ziko huru kujiunga, wateja wanapaswa kujisajili kwa vifurushi, ambavyo hugharimu kutoka Dola za Kimarekani sita hadi 300, kupokea au kutuma ujumbe kwa 'mpenzi'.

Ingawa wateja wachanga wanataka kukutana kimwili na wanawake wanaofikiri wako karibu nao, wateja wakubwa mara nyingi wanaridhika na gumzo za ngono na picha na video za ngono, Abiodun anasema.

Madhumuni ya Abiodun na wasimamizi wengine wa gumzo ni kuwashikilia wafuatiliaji hawa kwenye tovuti kwa muda mrefu iwezekanavyo kwa nia ya kutumia fedha zao. Wasimamizi wanaagizwa kwamba kila ujumbe lazima uwe na angalau herufi 150 na uwe 'wazi, kuendeleza mazungumzo.

"Ni kama kazi ya huduma kwa wateja, mteja pekee ndiye anayefikiri kuwa anazungumza na Mkurugenzi Mtendaji," imebainika.

Imeshuhudiwa, ushahidi kwenye akaunti za WhatsApp, Telegram na Skype zilifichua kampuni ilikuwa imeajiri na kutoa mafunzo kwa mamia ya wasimamizi wa mazungumzo, wengi wao wakiwa katika majimbo ya Lagos na Abuja Nigeria.

Kazi za msimamizi wa gumzo zinatangazwa kwenye Instagram, Twitter na Telegram zinazolenga kundi la vijana wasio na ajira, waliosoma kama "majukumu ya mtandaoni", "kazi za uuzaji wa kidigitali", "majukumu ya msimamizi wa gumzo", bila kutajwa kwa wafanyakazi wa maudhui ya watu wazima.

Mmoja wa waajiri, anayeishi Ujerumani, anashughulikia matangazo ya kazi kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii, anaonesha mtindo wa maisha wa glitz na urembo na likizo katika maeneo ya kigeni.

Huyo amekuwa akiajiri wasimamizi wa mazungumzo ya mtandao huo kwa zaidi ya miaka miwili na katika harakati moja ya kuajiri watu Novemba mwaka jana, mamia ya watu walijiandikisha. Hata hivyo hakujibu maombi ya kupata maoni yake.

***Kwa mujibu wa BBC.***

## CHEMSHABONGO NA -00 5 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
2. mji mkuu wa Mali
5. hua
8. kinyume cha leo
10.ongezeka kimo
11.kutembea taratibu
12.mwezi ambao siku ya saba saba huadhimishwa
13.Binadamu
15.hutumika kuvulia samaki
16.ndege mwenye tabia ya kuruka njiani wakati wa usiku

Chini:
1. kortini
2. mji mkuu wa Gambia
3. Rais wa Zanzibar
4. keti
6. siku iliyopita
7. doa, bato
9. tegemewa
11.ndege mweusi anayesafisha mazingira jiji la Dar Es Salaam
14.hutumika kufukiza





## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| ILIKI | JIJI |
| ULAYA | JANA |
| ARAKA | JUTA |
| OROMO | NOTI |
| UPANGA | UMA |
| ANGUA | PONA |
| GAUNI | AINA |
| GITAA | ADAA |
| AMANI | AYA |
| ADAMU | UFA |
| NAMBARI | SIMBA |
| MADARAKANI | |
| SHAURI | |

A M A N I

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | Y | A | M | A | Z | I | S | H | W | A |
| Y | | N | | N | | | | | | U |
| U | | D | | D | | | | | | S |
| M | K | A | T | E | | | | | | T |
| B | | M | | S | | | | | | R |
| A | R | A | B | I | K | A | | D | O | A |
| | | | | | A | | D | | | L |
| | | | | R | U | T | O | | | I |
| | | | | A | S | I | L | I | | A |
| | | | | I | H | S | A | N | I | |
| | | | | S | A | A | | I | | |





| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Z | A | N | Z | I | B | A | R | | U |
| O | G | A | | | A | N | A | | B |
| M | A | D | A | | I | G | I | Z | O |
| E | | A | D | A | N | A | | | R |
| A | S | M | I | N | I | | O | K | A |
| | H | A | M | A | K | I | | A | |
| | A | | U | S | A | L | A | M | A |
| O | N | A | | A | | I | G | A | |
| | G | | | | M | K | O | S | I |
| T | A | M | A | A | | I | | I | |

maoni: 0755429240





## RC ahimiza matumizi miundombinu ya usafiri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameshauriwa kutumia miundombinu ya usafiri na usafirishaji inayojengwa na serikali kujipatia kipato kwa kusafirisha mazao wanayozalisha kwenda kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na watendaji mbalimbali wa mkoa huo kuhusu tathmini ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwamo ujenzi wa barabara, sekta ya kilimo na shughuli zingine za usafirishaji.

Homera aliwataka watendaji wa serikali kuwahamasisha wananchi kuzalisha mazao mbalimbali kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya masoko ikiwamo mazao ya chakula, biashara na mazao ya bustani ambayo alisema yana soko kubwa.

Alisema kwa sasa serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yote na hivyo wananchi wanatakiwa kuongeza uzalishaji.

Miundombinu hiyo, alisema inawarahisishia usafirishaji wa pembejeo za kilimo kwenda mashambani na kusafirisha mazao kutoka mashambani kwenda nyumbani na sokoni.

"Uwanja wetu wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) sasa hivi umeboreshwa. Ndege zimeanza kutua usiku na mchana na ndege kubwa na ndogo zinatua kwa hiyo baadhi ya mazao yatasafirishwa kwa ndege. Ni jukumu letu kuwahimiza wananchi kuzalisha mazao kwa wingi," alisema Homera.

Aliwataka pia wananchi wa maeneo ambayo miundombinu hiyo inajengwa kuilinda ili iwasaidie kwa muda mrefu na kuokoa gharama ambazo serikali imekuwa ikiingia kwenye ukarabati wa barabara hizo.

Alisema hivi karibuni TARURA imeingia mikataba 92 na makandarasi kwa ajili ya kuanza kujenga barabara mbalimbali kwa kiwango cha lami na changarawe na hivyo akawataka watendaji wa serikali kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo.

# Mabaki ya mwanafunzi aliyepotea yakutwa porini baada ya miezi tisa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MABAKI ya mwili wa mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Ikuti wilayani Rungwe, Levice Mwailemale (16) aliyepotea katika mazingira ya kutatanisha miezi minane iliyopita, yamekutwa porini hali iliyozua taharuki miongoni mwa wananchi.

Baba mkubwa wa mwanafunzi huyo, Edward Mwambagi, alisema juzi kuwa mtoto huyo alipotea Januari 9, mwaka huu, alasiri katika kijiji hicho na walimtafuta kwa kushirikiana na wananchi wa kata nzima ya Ikuti bila mafanikio.

Alisema kijana huyo alikuwa hana tatizo lolote la kiafya wala kiakili na kwamba kwa muda huo alikuwa anajiandaa kuingia kidato cha nne katika shule hiyo.

Mwambagi alisema Septemba 18, mwaka huu, baadhi ya vijana waliokuwa wanakwenda mtoni kuvua samaki walibaini mabaki ya mwili huo ndipo wakatoa taarifa serikalini.

Alisema walibaini kuwa mabaki ya mwili huo ni ya kijana huyo kutokana na kuzikuta pia nguo alizokuwa amevaa wakati anapotea ambazo ni fulana yenye rangi ya damu ya mzee na suruali nyeusi.

"Ilikuwa kama bahati maana njia waliyopita vijana hao huwa haipitiki. Walipoona zile nguo, walishtuka na walipokwenda mbele kidogo walikuta mifupa na fuvu ndio wakaja kutoa taarifa kijijini na kweli tukabaini ni yeye," alisema Mwambagi.

Alisema baada ya hapo walitoa taarifa polisi na askari polisi walifika na kuwaruhusu kuendelea na taratibu za maziko, hivyo wakazika Septemba 19.

Mama mdogo wa marehemu, Enea Mwijumileghe, alisema kijana wao hajawahi kuwa na tabia mbaya kijijini hapo, hivyo hawaelewi alikufa kwa tatizo gani.

Alisema alikuwa anahudhuria shuleni bila tatizo lolote na alikuwa hajawahi kuugua jambo ambalo linawapa wasiwasi kwamba huenda aliuawa na watu wenye nia ovu.

Baada ya kupotea, alisema walitumia kila mbinu kumtafuta kwa kuitisha hata mikutano ya hadhara lakini hawakuwahi kumuona wala kupata taarifa za aina yoyote kuhusu mtoto huyo mpaka walipoambiwa mabaki yake yameonekana porini.

"Tumeumia sana maana mtoto huyu alikuwa hana tatizo lolote. Tulihangaika sana kumtafuta lakini hatukufanikiwa tukakata tamaa. Kwa sasa mtoto angekuwa anaelekea kuhitimu kidato cha nne na wenzake," alisema Enea.

Baadhi ya vijana wa kijiji hicho waliiomba serikali kufanya mikutano ya mara kwa mara maeneo ya vijijini ili kutoa elimu kwa kuwa matukio mengi yamekuwa yakitokea ambapo mengine yanahusishwa na imani za kishirikina na mengine yanahusishwa na visasi.

Mmoja wa vijana hao, Uswege Mwakota, alisema katika kipindi cha karibuni vitendo vya mauaji ya watu yametokea mara tatu kwenye kata yao jambo ambalo alisema imeanza kuwatia wasiwasi. Alisema kijana Elvice alikuwa anashirikiana vizuri na wenzake na hakuwahi kuwa na ugomvi na yeyote jambo ambalo linawapa wakati mgumu kubaini cjhanzo cha kifo chake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alisema bado hajapata taarifa za tukio hilo lakini ataagiza vijana wake kufuatilia ili kubaini ukweli wa tukio hilo.

Kamanda Kuzaga alisema amesafiri yuko mkoani Dodoma kikazi, hivyo ufuatiliaji ukikamilika atatoa taarifa kupitia vyombo vya habari.



Mwalimu wa Shule ya Msingi inayohudumia watoto wenye ulemavu ya Child Support Tanzania (CST), Libera-tus Mzuwa, akitoa huduma kwa mtoto Ethan Laswai, katika hafla ya kupokea fedha zaidi ya Sh. milioni 200 kutoka Ubalozi wa Ujerumani, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Walimu watoro watangaziwa kiama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya imewatahadharisha walimu wanaotoroka kazini na kwenda kufanya shughuli zao kuwa watachukuliwa hatua kali za kinidhamu na kisheria kwa kuwa wanakiuka mikataba ya kazi zao.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Vincent Mbua, alitoa tahadhari hiyo juzi alipokuwa anazindua Mkakati wa Uimarishaji wa Ujifunzaji Ngazi ya Elimu ya Msingi na Sekondari ulioandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mkakati huo umeanzishwa na serikali kwa lengo la kuboresha elimu katika ngazi za chini ambao inaelezwa kuwa unalenga kubaini matatizo yanayoikabili sekta ya elimu na kutafuta mbinu za kuyatatua.

Mbua alisema utafiti uliofanyika hivi karibuni umebaini kuwa asilimia kubwa ya walimu wamekuwa wakifika shuleni asubuhi na kuondoka kwenda kufanya shughuli zao bila kufuata utaratibu jambo ambalo linazorotesha elimu.

Alisema walimu hao wamekuwa wakijiandikisha kwenye vitabu vya mahudhurio na kisha kuondoka, hivyo kusababisha wanafunzi kukosa baadhi ya vipindi ambavyo wanatakiwa kufundishwa.

"Utafiti huo ambao tuliufanya kwa siri, ulionyesha kuwa walimu hawa wakiondoka asubuhi huwa wanarudi tena jioni na kutia saini kuashiria kwamba walikuwapo kazini. Jambo hili nawahakikishia kwamba tutaanza kuwachukulia hatua za kiutumishi," alisema Mbua.

Alisema jambo hilo huwa linasababisha hata wanafunzi kuwa watoro na kuanza kuzurura mitaani jambo ambalo alisema linaweza likasababisha kuongezeka kwa makundi ya uhalifu mitaani.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalimu Tanu Kameka, aliipongeza serikali kwa kuanzisha mkakati huo kwa maelezo kuwa utasaidia kuboresha kiwango cha elimu nchini.

Alisema kwenye kitabu cha mpango huo kuna matatizo mbalimbali yanayoikabili sekta ya elimu yameainishwa, visababishi vyake pamoja na mbinu za kuyatatua matatizo hayo, hivyo akawataka wadau wote kuusoma na kutekeleza vizuri majukumu yao.

Kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya elimu, alisema kunahitajika ushirikiano wa hali ya juu miongoni mwa wadau wakiwamo wazazi na walezi pamoja na walimu.

"Ukikisoma kitabu hiki unaona kabisa kuna mikakati ya kisasa ya kuboresha elimu yetu, sasa ni jukumu letu wadau kuhakikisha tunashirikiana kutekeleza mikakati hii kwa utimilifu," alisema Kameka.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Mbeya, Aliko Mbuba, alisema mbali na mpango huo kuainisha matatizo ya elimu na namna ya kuyatatua, pia umeeleza njia bora za kuwapata viongozi katika sekta hiyo ya elimu.

Alisema mkakati huo unaonyesha namna ya kuwateua wakuu wa shule, walimu wakuu na maofisa elimu katika ngazi zote ili kupata viongozi sahihi kwenye sekta hiyo.

Alisema watahakikisha wanafuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa mpango huo ili kupata matokeo sahihi ambayo serikali inayahitaji kwa ustawi wa taifa.





# Mradi wa afya mimea kugharimu Euro mil. 10

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), na Umoja wa Ulaya (EU), imezindua mradi wa kuimarisha huduma za afya ya mimea na usalama wa chakula nchini utakaotekelezwa kwa miaka mitatu na nusu kwa gharama ya Euro milioni 10.1.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema jana jijini hapa kuwa mradi huo utasaidia kudhibiti visumbufu vigeni kwa kuhakikisha mazao yanayoingia au kutoka nchini yanakuwa na ubora unaokidhi viwango vya kimataifa.

Mavunde alisema, mradi huo una lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa utoaji wa usafi wa mazao yanayoingia na kutoka nchini.

"Mradi huu umetokana na ukaguzi uliofanyika mwaka 2017 katika mifumo maalumu ya udhibiti wa mimea na mazao yanayosafirishwa kwenda nchi za Umoja wa Ulaya na ukaguzi huo kubaini upungufu wa afya katika mimea," alisema.

Alitaja baadhi ya maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu ni maarifa madogo kwa wakaguzi kuhusu matakwa ya usafi wa mazao hayo, kukosekana kwa mfumo kukusanya takwimu za visumbufu vya mimea, kukosekana kwa maabara zenye uwezo wa kufanya uchunguzi muhimu ili kuthibiti cheti cha usafi wa mimea.

"Kutokana na kubainika huko na gharama za kufanya biashara ya mazao kuwa juu, serikali ilichukua hatua kwa kuunganisha majukumu ya TPRI, na ya afya ya mimea na viwatilifu TPHPA ambacho kimekuwa chombo kinachotambulika kimataifa," alisema.

Hata hivyo, alisema kuja kwa mradi huo utawezesha kufikia malengo ya kuhakikisha ukuaji wa sekta ya kilimo nchini kwa asilimia 10 na mauzo ya mazao ya kilimo yanaongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 za sasa hadi kufikia Dola bilioni tano ifikapo mwaka 2030.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Dk. Efraim Njau, alisema sekta ya kilimo ni muhimu kwa kuwa imeajiri takribani asilimia 67 ya Watanzania na kuchangia takribani asilimia 29 ya pato la taifa.

"Matokeo tarajiwa ya mradi huu ni kuziongezea uwezo maabara za mamlaka kujenga, kukarabati na kuweka vifaa katika maabara za mamlaka, kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa visumbufu na masalia ya viuatilifu katika mnyroro wa thamani ya uzalishaji wa mazao hususani ni yale mbogamboga na matunda," alisema.

Mwakilishi wa FAO, Nyebenyi Tipo, alisema mradi huo umelenga kuhakikisha usalama wa chakula hasa kwa mazao yanayovuka mipaka kwa kuhakikisha yanakuwa na ubora.



Msajili wa Bodi ya Wahandisi nchini, Mhandisi Bernard Kavishe, akizungumza na waandishi wa habari wa Jiji la Dodoma juzi, kuhusu siku ya wahandisi itakayoenda sambamba na maonyesho ya kazi zao, jijini humo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Waziri azipigia debe bidhaa asilia Jua Kali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha wajasiriamali vijana watakaoshiriki maonyesho ya 22 ya wadogo na kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanapeleka bidhaa za asili za mikoa au wilaya wanazotoka.

Maonyesho hayo yanayojulikana kama Nguvu Kazi au Jua Kali yamepangwa kufanyika Desemba 8 hadi 18, jijini Kampala, Uganda, yatashirikisha wajasiriamali 1,000 wa jumuiya hiyo huku Tanzania itawakilishwa na wajasiriamali wasiopungua 250.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza kuhusu maonyesho hayo.

Alisema, serikali imejipanga kuwawezesha vijana wajasirimali wa Tanzania kushiriki na itatoa kipaumbele kwa watakaozalisha bidhaa za Tanzania zenye ubora unaokidhi soko la jumuiya hiyo.

"Lengo la maonyesho ni kuwawezesha vijana wajasiriamali kurasimisha shughuli zao kwa kuwapatia fursa ya kutangaza bidhaa zao, kubadilishana taarifa, kukuza ujuzi, kukuza masoko ya bidhaa na kukuza teknolojia ya utengenezaji wa bidhaa na kuongeza fursa za ajira za staha kwa vijana, serikali imepanga kuongeza wigo wa mchango wake.

"Ninayo furaha kuwajulisha kuwa serikali imejipanga kufanikisha maonyesho haya kwa lengo la kuwawezesha vijana wajasiriamali wa Tanzania kutumia fursa hii ya kutafuta masoko katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki,"alisema.

"Kwa miaka mingi, pamoja na mambo mengine, serikali imekua ikichangia usafiri wa mizigo ya Wajasiriamali kwenda kwenye maonesho. Kwa mwaka huu, Serikali imepanga kuongeza mchango wake kwa kuwezesha usafiri wa basi la wajasiriamali kwenda na kurudi Uganda," alisema.

# Wahandisi 200 warejeshewa usajili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAHANDISI 200 kati ya 800 waliochukuliwa hatua kwa makosa mbalimbali wamerejeshewa usajili wao huku wengine wakiendelea kuchunguzwa.

Msajili wa Bodi ya Wahandisi (ERB), Bernard Kavishe, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Wahandisi (AED) inayofanyika jijini hapo.

Kavishe alisema, bodi hiyo imekuwa ikichukua hatua za kuwapa onyo kali ikiwamo kufutiwa usajili ili kuhakikisha wahandisi wanatekeleza kazi zao vizuri na kwa weledi na kufuata maadili ya uwajibikaji yanavyoelekeza.

"Sisi kwetu kumfukuza mhandisi ni sawa na kupata msiba kwa sababu tunakuwa tumepoteza mtu muhimu kwenye fani ndiyo maana bodi imekuwa ikiwafuatilia katika miradi mbalimbali wanayotekeleza," alisema Kavishe.

Kavishe alisema, bodi hiyo imekuwa ikiwafuatilia wahandisi wake katika miradi mbalimbali wanayotekeleza na wanafanya hivyo ili kuepuka kwenda kinyume cha kazi ambazo wanakabidhiwa hasa za ujenzi wa miundombinu.

Kuhusu usajili wa wahandisi kwenye bodi hiyo, alisema mpaka sasa tayari wamesajili wahandisi 33,000 lakini walioko kazini mpaka sasa ni 26,000 huku wengine wakiwa wamestaafu.

Mhandisi Kavishe, alisema ERB kwa kushirikiana na bodi za nchi za Afrika Mashariki, wameanza mchakato wa kuhakikisha mhandisi aliyesajiliwa nchini, akifika Kenya au Uganda afanye kazi kwa usajili uleule, lakini kuna viwango ambavyo wanaviangalia ambavyo vinakubalika kwa pamoja.

"Tayari tumeanza mchakato huo. ukikamilika tutauweka bayana,"alisema Kavishe.

Kuhusu kampuni za nje kufanya kazi za miradi nchini, alisema suala hilo lipo na wameanza mchakato wa kutafuta wahandisi wa Tanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ,ili kuwa na kanzidata ya kuwatambua wote katika nchi mbalimbali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya AED, Benedict Mukama, alisema wanatarajia kuhudhuria wahandisi 3,500 lakini wengine watashiriki kwa njia ya mtandao kutokana na kukabiliwa na majukumu mbalimbali.

Mukama alisema, mpaka sasa tayari kila kitu kimekamilika na kuongeza kuwa kutakuwa na ugeni wa wahandisi kutoka nje ya nchi ili kubadilishana mawazo na wahandisi wa ndani katika masuala ya utendaji kazi zao za kila siku.





## Waziri aanika sababu kupotea wazee, watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Anna Athanas Paul, amesema kupotea kwa watoto au kuibwa kunatokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa usimamizi na uangalizi wa kina kwa wazee wa watoto.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi Hamad, aliyetaka kujua idadi ya watoto waliopotea au walioibwa na kushindwa kupatikana kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Naibu Waziri alitaja sababu zingine kuwa ni kuachwa na watoto wenzao bila ya ufuatiliaji pamoja na harakati za kimaisha kwa wazazi.

Alisema matukio hayo huwa yanatokea kwa uchache na kasi yake si kubwa kama ambavyo inazungumzwa.

"Mheshimiwa Spika, Wizara yetu bado haina takwimu halisi kuwa matukio haya yanapotokea huwa yanaripotiwa katika vituo vya polisi, redio na televisheni na masheha wa shehia kwa msaada wa taarifa na upatikanaji wa watoto hao," alisema.

Pia alisema serikali inachukua jitihada mbalimbali katika kudhibiti janga hilo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya malezi na uangalizi wa watoto, mawasiliano na watoto, kushauri wazazi kuwachagulia watoto wao marafiki ambao wanawaamini na watakaosaidia kuwalinda watoto wao pindi kukitokea tatizo la aina yoyote.

Alisema hatua nyingine ni kutoa ushauri nasaha kwa wazazi, walezi na jamii juu ya umuhimu wa malezi ya pamoja.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inasisitiza matumizi ya Namba 116 kama sehemu ya kutolea taarifa za matukio ya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto ili kurahisisha na kusaidia upatikanaji wa miongozo sahihi ya ulinzi wa watoto.

Pia alisema wizara inakusudia kuendelea kutoa elimu ya malezi kupitia vipindi vya redio, televisheni na uandaaji wa makala kama sehemu ya kukabiliana na janga hilo na kujenga kizazi chema katika jamii.

"Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwaomba waheshimiwa wa baraza lako tukufu kuendelea kuunga mkono jitihada hizi ili kwa pamoja tujenge kizazi chema na kizazi chenye usawa katika taifa letu," alisema.

# Zanzibar, USAID sasa kuboresha sekta afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema wizara yake itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo likiwamo Shirika la Misaada la Maendeleo la Marekani (USAIDO ili kuimarisha sekta ya afya.

Mazrui amesema USAID inasaidia sekta ya afya katika maeneo mbalimbali ikiwamo kutokomeza malaria, kifua kikuu, homa ya ini na huduma zingine za kijamii.

Akizungumza jana na Mshauri Mkuu wa USAID, Magret Toylor, ofisini kwake Mnazi Mmoja, Waziri Mazrui alisema kutokana na jitihada za serikali ya Zanzibar na washirika wa maendeleo, ikiwamo USAID, wizara imepiga hatua katika kupambana na malaria na sasa yako chini ya asilimia moja.

Alisema USAID imesaidia katika kudhibiti ugonjwa wa Ukimwi ambao umeathiri nguvu kazi ya Watanzania na kwa sasa UKIMWI Zanzibar umepungua kwa kiasi kikubwa cha asilimia tatu.

Pia alisema bado magonjwa ya homa ya ini na kifua kikuu, yanawasumbua Wazanzibari na matibabu yake yanagharama kubwa, hivyo aliwataka washirika wa maendeleo kuendeleza misaada yao kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na vifaa tiba na mafunzo kwa wafanyakazi.

Kwa upande wake, Toylor alisema shirika hilo litaendeleza misaada yake kwa Zanzibar ili kuimarisha huduma za afya.

Alisema lengo la kufanya ziara visiwani hapa ni kutembelea vituo vya afya na jumuiya wanazozisaidia na kujua maendeleo yaliyofikiwa.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akizungumza na ujumbe kutoka Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kuhusu uimarishaji wa Sekta ya Afya, walipofika ofisini kwake, Mnazi Mmoja, mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yakiri hatari kutoweka haiba mazingira maeneo uchimbaji mchanga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini, imekiri kuwa uchimbaji wa madini ya ujenzi unasababisha kupotea kwa haiba ya asili ya maeneo yanayochimbwa mchanga na kifusi.

Imesema ikiwa uhuishaji wa maeneo hayo hautafanyika baada ya kumalizika kwa uchimbaji, kuna hatari ya kuwepo athari kubwa za kimazingira.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Shaban Othman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana wakati ajikibu swali la Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake, Mwantatu Mbaraka Khamis. Mwakilishi huyo alitaka kujua serikali imejipanga vipi kurejesha haiba ya maeneo yaliochimbwa mchanga na kifusi.

Naibu Waziri huyo alisema kwa kulitambua hilo, wizara yake imeanza uhuishaji wa maeneo yaliyochimbwa mchanga na serikali kwa kuanzia maeneo matano yenye ekari 104 kwa kupanda miche 104,000.

Alisema hadi sasa wizara imepanda takriban miche 40,000 katika maeneo mawili yaliyoko eneo la Panga Tupu mkoa kwa Kaskazini Unguja.

Pia alisema wizara tayari imewaandikia barua wananchi ambao maeneo yao yamechimbwa maliasili zisizorejesheka kwa kuwataka kuanza kuyahuisha.

"Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kusisitiza kwa wale wote ambao hawajaanza uhuishaji kwenye maeneo yao kuanza kutekeleza takwa hilo la kisheria mara moja," alisema.

Naibu Waziri alisema kushindwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mkataba wa uchimbaji wa maliasili husika, hivyo wizara haitasita kumchukulia hatua mtu yoyote ambaye hatatekeleza agizo hilo.



## Bei ya vyakula yazidi kupanda

**Elizabeth Faustine na Neema Emmanuel**

BEI ya nafaka katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza imeendelea kupanda huku baadhi ya watumiaji wa bidhaa hizo wakishindwa kumudu kununua.

Baadhi ya wateja waliiambia Nipashe kuwa mabadiliko hayo ya bei yalianza Juni mwaka huu na kwamba kila siku imekuwa ikiongezeka.

Nipashe ilitembelea baadhi ya masoko katika Jiji hilo na kubaini mabadiliko hayo ya bei kwa baadhi ya nafaka ambazo zinatumiwa na wananchi kila siku.

Katika Soko la Kisesa wilayani Magu, bei ya mahindi ya jumla kwa gunia la kilogramu 100 ni Sh. 120, 000 kutoka Sh. 90,000 miezi miwili iliyopita.

Aidha, alisema bei ya mchele huuzwa kulingana ubora wake na kiwango cha chini katika soko hilo Sh. 2,500 kwa kilo na maharage huuzwa kuanzia Sh. 2,600 hadi Sh. 3000 kwa kilo moja.

Katika Soko la Mirongo jijini Mwanza bei nazo zinabadilika kila siku na kwa sasa kilo moja ya mchele ni Sh.2,800 kutoka Sh.1,800, Juni mwaka huu na maharage ni Sh. 2, 800 hadi Sh.3,000 kutoka Sh. 2,400 miezi miwili iliyopita na choroko zinauzwa Sh. 2,000 kutoka Sh. 1500.

Martha Paulo mkazi wa Mabatini jijini Mwanza alisema awali alikuwa akifanya biashara ya kuuza chakula katika soko hilo, lakini kutokana na kupanda kwa bei ya nafaka amelazimika kufunga biashara hiyo na kuanza kuuza mihogo ya kukaanga ili kujipatia kipato.

"Kwa sisi tunaonunua bidhaa kidogo kidogo kwa sababu ya mtaji mdogo hali hii ya kubadilika bei kila kukicha inatuathiri sana kwa sababu tungekuwa na mtaji mkubwa tungenunua mzigo mkubwa ili tuweke ndani, lakini kwa sababu tunaenda kuhemea kila siku, lazima tuathirike na mabadiliko hayo," alisema Matha.

Juma Meeda mkazi wa Kijiji cha Ihayabuyaga wilayani Magu, alisema ongezeko hilo la bei ya mahindi haliwaumizi watu wenye familia kubwa pekee bali hata wateja wanaokula kwenye migahawa na kwa mamantilie kwa kuongezewa bei ya chakula.

"Sisi ambao tunakula kwa mamantilie na migahawani bei imepanda, lakini pia wamepunguza kiwango, 'aise' unapewa ugali kama ngumi ukichukua mara moja, mara ya pili ugali umeisha hata haujashiba inabidi uongeze mwingine, sasa hapo ndiyo unapoona athari ya kuongezeka kwa bei ya mahindi," alisema Sungura.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Soko Kuu la Mirongo jijini Mwanza, Hamadi Nchola alisema kupanda kwa bei za bidhaa hizo kumechangia wateja kupungua na waliopo kupunguza kiwango cha kununua.

# DC ataka wadau kuenzi aliyoyafanya Dk. Mengi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka wadau wa maendeleo kuyaenzi matendo mazuri yaliyoachwa na Dk. Reginald Mengi, ya kusaidia watu wenye ulemavu wa ngozi (albino).

Alisema enzi za uhai wake, Dk. Mengi ambaye alikuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, alikuwa akisaidia watu wenye ulemavu kutatua matatizo yao mbalimbali pamoja na kuwapatia faraja ya kula nao chakula.

Alibainisha hayo juzi wakati akigawa mafuta ya ngozi aina ya sunscreen lotion kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi wanaolelewa kwenye Kituo cha Buhangija katika Manispaa ya Shinyanga kwa ajili ya kuwakinga na mionzi ya jua ili wasipate ugonjwa wa saratani.

Alisema wadau wa maendeleo wanapaswa kuendelea kujitoa kusaidia watu wenye ulemavu kwa kutatua matatizo yao mbalimbali ili waishi kama watu wengine wasio na ulemavu.

Aliongeza kuwa Dk. Mengi aliwapa faraja kama alivyokuwa kwa kuwasaidia, ikiwamo kula nao chakula kila alipopata nafasi ya kufanya hivyo.

"Watoto hawa wenye ualbino wanahitaji msaada wetu, ndiyo maana tumefika hapa kituoni kwao kuwapatia mafuta haya ya Ngozi ili kulinda ngozi zao zisiathirike na mionzi ya jua na kupata saratani ya ngozi," alisema Mboneko.

Aidha, aliwaagiza madaktari kujenga utamaduni wa kutembelea watoto hao mara kwa mara ili kuangalia afya zao na kuwapatia matibabu.

Katika hatua nyingine alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha katika Shule ya Msingi ya Buhangija Jumuishi ili kuboresha miundombinu.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Dk. Elisha Robert, aliahidi kuwatembelea watoto hao mara zote, huku akibainisha kuwa mafuta hayo wameyanunua kwenye Bohari ya Dawa (MSD) kwa Sh. milioni 5.8.



Mwendesha pikipiki akiwa amewabeba wanafunzi wanne kwa mtindo maarufu kama 'mshikaki' katika kata ya Luchelele, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. Wazazi wengi wamekuwa wakitumia usafiri huo kuwapeleka watoto wao mashuleni kutokana na kushindwa kumudu gharama za mabasi ya shule ambazo ziko juu. **PICHA: VITUS AUDAX**

## TFS yawapa mafunzo ufugaji nyuki wenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANACHAMA 30 wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) wilayani Kahama, wamepatiwa mafunzo maalumu ya ufugaji nyuki kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ili kujikwamua kiuchumi.

Ufugaji huo unatarajiwa kufanyika katika misitu mbalimbali inayopatikana kwenye Halmshauri ya Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Meneja wa TFS, Ester Josephat katika ukumbi wa chuo cha uuguzi Kahama alisema, ofisi yake itaangalia namna ya kuwawezesha wanachama hao ili kufikia malengo yao walioyojiwekea. Alisema mafunzo hayo yalitolewa kwa wanachama 30, baada ya kuandika barua ya kuomba kupewa elimu ya ufugaji wa nyuki na utengenezaji wa mkaa mbadala ili kujikwamua kiuchumi kwa kutumia asilimia mbili ya mikopo inayotolewa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani.

"Asali soko lake ni la uhakika zaidi mafunzo hayo yakawe chachu kwenu ya kujikwamua kiuchumi na mtakapopata matatizo yoyote ya kiufugaji jaribuni kutatua kwa pamoja na zile zitazokuwa nje ya uwezo wenu hakikisheni mnatushirikisha," alisema .

Ofisa Ufugaji Nyuki wa TFS, Martha Machibya alisema wamekuwa wakitoa elimu hiyo kwa vikundi mbalimbali vya ujasiriamali.

Alisema mwaka wa fedha 2014/2015 TFS ilitoa mizinga 200 ya ufugaji nyuki kwa vikundi vya ujasiriamali na mwaka 2015/2016 ilisitisha utoaji wa mizinga hiyo kwa sababu mbalimbali na mwaka 2017/2018 Wilaya ya Kahama ilikuwa na jumla ya mizinga ya nyuki 5,201 iliyopo katika msitu wa Mkweni.

Machibya alisema soko la asali linapatikana nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya na kwamba mwisho wa mafunzo hayo anategemea kuona uzalishaji unaongezeka.

Mwenyekiti wa CHAVITA, Rucy Lutege alisema wenye ulemavu wengi wanabaguliwa katika ajira na kwamba mafunzo hayo yatawasaidia kujiajiri.

Katibu wa Shirikisho la Vyama wenye Ulamavu wilayani Kahama mkoani Shinyanga (SHIVYAWATAKA), Zawadi Masoudi alisema watatumia asilimia mbili ya mikopo inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya ufugaji wa nyuki wa kisasa.

# Rais Iran aikosoa Marekani

**NEWYORK,** Marekani

HUTUBA za viongozi mbalimbali zinaendelea kutolewa katika hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa unaofanyika mjini New York, Marekani.

Katika hotuba yake ya kwanza mbele ya hadhara hiyo, Rais mpya wa Iran, Ebrahim Raisi alisema Marekani imeyakanyaga makubaliano kuhusu mpango wa kimataifa wa nyuklia ya Iran uliosainiwa mwaka 2015.

Alisisitiza kwamba, nchi yake haina nia ya kuunda silaha za atomiki, badala yake ni kwa ajili ya matumizi ya nishati pekee.

Kiongozi huyo pia alisema kuwa Iran inayo nia ya kuwa na uhusiano mwema na majirani zake wote.

Aidha, Raisi alipinga vikali vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na nchi za magharibi dhidi ya nchi yake, akivitaja kuwa adhabu ya jumla kwa watu wake.

Hata hivyo, Rais wa Marekani Joe Biden, alitarajiwa kutoa hotuba yake, akielekezwa kuishambulia vikali Russia kwa uvamizi wake dhidi ya Ukraine, na kuhamasisha uungwaji mkono wa mataifa mengine kuisaidia Ukraine kujilinda **DW**

========================

## Macron awakutanisha Tshisekedi, Kagame

**NEWYORK**, Marekani.

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amewakutanisha viongozi mahasimu Félix Tshisekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Paul Kagame wa Rwanda katika kujadili mgogoro wa usalama mashariki mwa DRC.

Mkutano wa viongozi hao ulifanyika pembezoni mwa kikao cha Umoja wa Mataifa mjini New York.

Katika hotuba yake siku ya Jumanne, Tshisekedi aliituhumu vikali Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 mbele ya mkutano wa Umoja wa Mataifa.

Siku ya pili yake, Kagame alijibu kwa kuambia mkutano huo kuwa mchezo wa kurushiana lawama hausuluhishi matatizo.

Baada ya hotuba hiyo, wawili hao walikutana chini ya mpango wa Macron wa kutafuta suluhu.

Kwenye mkutano huo, Kagame aliunga mkono mchakato wa kikanda kama suluhu la mzozo huo lakini alisema utahitaji usaidizi thabiti wa kifedha kutoka kwa jumuiya ya kimataifa.

Mamlaka za kikanda zimekubali kuunda kikosi cha kikanda ili kupambana na makundi ya waasi wa mashariki mwa DR Congo, bado haijafahamika ni lini kikosi hicho kitaanza kazi

Kundi la waasi la M23, linadhibiti sehemu za Jimbo la Kaskazini mwa Congo tangu Juni. **BBC**

# Watu zaidi waambukizwa Ebola Uganda

**KAMPALA,** Uganda

WIZARA ya afya nchini Uganda imetoa orodha ya wagonjwa wapya sita wa Ebola baada siku chache baada ya kuthibitisha mlipuko wa ugonjwa huo.

Visa hivyo vipya vya maambukizi viliripotiwa katika wilaya ya kati ya Mubende, ambako mwanamme mwenye umri wa miaka 24 alithibitishwa kufariki juzi baada ya kuonyesha dalili za ugonjwa huo.

Msichana wa mwaka mmoja pia anashukiwa kufariki kutokana na ugonjwa huo.

Kati ya wagonjwa hao sita, mmoja aliripotiwa kutoka wilaya jirani.

Mlipuko huo ni wa tatu wa ugonjwa wa ebola nchini Uganda.

Zaidi ya watu 40 ambao walitangamana na familia iliyopatikana na maambukizi katika mji wa viru wamefuatiliwa.

Watu hao, kumi na moja kati yao wametengwa, alisema Kyobe Henry Bbosa,kamanda wa usimamizi wa matukio kutoka Wizara ya Afya.

Nchi jirani zilisema ziko katika hali ya tahadhari iwapo ugonjwa huo utasambaa katika mipaka.

Wataalamu wanasema kuwa ugonjwa wa ebola aina ya Sudan kihistoria una viwango vya chini vya maambukizi na vifo ikilinganishwa na aina ya Ebola Zaire.

Mamlaka ya Uganda inaendelea kuhakikishia umma na jumuiya ya kimataifa kwamba wana uwezo wa kudhibiti janga hili.

**BBC**



Wafungwa wa vita waliobadilishana akiwamo raia wa Uingereza, Shaun Pinner (aliyevaa fulana ya rangi ya chungwa), wakiwa wamekaa baada ya kuteremka kwenye ndege yao kuelekea Saudi Arabia, kabla ya kurejea katika nchi zao.

# Russia, Ukraine zabadilishana wafungwa

**KYIV,** Ukraine

KATIKA hali ya kushangaza nchi za Russia na Ukraine zimebadilishana wafungwa juzi, na kuelezwa hatua hiyo ni kubwa zaidi tangu kuanza kwa vita kati ya majirani hao.

Tukio hilo limekuja siku mbili baada ya Rais Vladmir Putin, kutangaza kuanza kuwasajili wanajeshi wa akiba kwa ajili ya kutekeleza mpango wa mapigano nchini Ukraine.

Katika zoezi la kubadilishana wafungwa hao kulihusisha watu 300, wakiwamo raia 10 wa kigeni na makamanda walioongoza operesheni ya kijeshi katika eneo la Mariupol mapema mwaka huu.

Wafungwa wa kigeni walioachiliwa huru ni pamoja na Waingereza wawili na raia mmoja wa Morocco, ambaye alikuwa amehukumiwa kifo mnamo mwezi Juni baada ya kukamatwa akiwasaidia wanajeshi wa Ukraine katika uwanja wa mapambano.

Wengine walioachiliwa ni Wamarekani wawili, raia mmoja wa Croatia na mwengine wa Uswidi.

Hata hivyo, muda na ukubwa wa hatua hiyo ya kubadilishana wafungwa ndio imewashangaza wengi hasa ikizingatiwa kuwa Rais Putin alikuwa ametangaza uhamasishaji wa vijana kujiunga na kikosi cha jeshi na kuongeza hofu ya mzozo huo.

Makundi ya wapiganaji na wanaoungwa mkono na Russia walisema mwezi uliopita kuwa makamanda wa Mariupol watapandishwa kizimbani.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenksy alisema, hatua hiyo ya kubadilishana wafungwa ambayo ilihusisha mazungumzo kutoka Uturuki na Saudi Arabia, ilikuwa inafanyiwa kazi kwa muda mrefu.

Chini ya masharti ya makubaliano hayo, Waukraine 215- ambao wengi wao walikamatwa baada ya eneo la Mariupol kuwa chini ya udhibiti wa vikosi vya Russia, waliachiliwa huru.

Kwa upande wa Ukraine, iliwarudisha Warusi 55 na raia kadhaa wa Ukraine wanayoiunga mkono Russia pamoja na Viktor Medvedchuk, kiongozi wa chama kinachoungwa mkono na nchi hiyo ambacho kilipigwa marufuku. Medvedchuk, alikuwa anakabiliwa na mashtaka ya uhaini.

Katika ujumbe kwa njia ya video, Zelenksy alisema "Huu ni ushindi kwa nchi yetu na jamii yetu kwa ujumla. Lakini jambo la msingi ni kwamba familia 215 zitapata nafasi ya kuonana na wapendwa wao wakiwa salama nyumbani."

Zelenksy alitoa shukrani kwa Rais wa Uturuki Tayyip Erdogan kwa mkono wake katika kufanikisha hilo.

Rais huyo wa Ukraine alisema kuwa makamanda hao wa Ukraine watasalia Uturuki hadi mwisho wa vita hivyo.

Alieleza kuwa umekuwa mchakato mrefu wenye panda shuka katika kuhakikisha raia hao wanaachiliwa huru. Miongoni mwa walioachiliwa ni Luteni Kanali Denys Prokopenko, Kamanda wa jeshi wa kikosi cha Azov, naibu wake Svyatoslav Palamar.

Mwingine ni kamanda wa jeshi la wanamaji Serhiy Volynsky.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DSM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 1717/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SWALEHE BAKARI KIMBOKO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MOHAMED HAMIS KISEMBO**

**TANGAZO**
**(kanuani ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowowte/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 09 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**PASKALI JOSEPH MUHALE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1177/018/2016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAMIRE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MBE/TUK/RB/399242/2021**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 185 YA MWAKA 2022.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**JOHN JAPHETH KIBOKO**

**GEORGE JAPHETH KIBOKO ......MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 03 mwezi wa Novemba, 2022.
**Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 19 mwezi wa Septemba, 2022.**

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......64/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: YAHAYA HEMED WA KASANGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA AYUBU YAHAYA HEMED**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 06 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 09 mwaka 2022

HAKIMU MFAWIDHI

---

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA IMARISHA MAISHA TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 21/10/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA SUZUKI ALTO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 581 DJJ MALI YA MARK LUHUMBIKA BUTINGO, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE.

KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.

---

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UHUMA FINANCIAL SERVICES TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 21/10/2022 SAA SITA MCHANA WA KUUZA NYUMBA PLOT NO. 92 BLOCK "B" MLIMWA NORTH MALI YA LINDA MONGI, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA, MNADA UTAFANYIKA MAHALI NYUMBA ILIPO.

KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.

---

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UHUMA FINANCIAL SERVICES TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 21/10/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA MITSUBUSH CANTER NYENYE NAMBA ZA USAJILI T 721 CTF MALI YA DANIEL LAMBA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA, MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE.

KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha HANETI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 03/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MALAYA SAGALAGWA wa HANETI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MAGANGA MALAYA SAGALAGWA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 21 Mwezi 09 Mwaka 2022

HAKIMU MAHAKAMA HAKIMU YA MWANZO HANETI DODOMA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PELISI MESHAKI KAMARA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota **LITEACE** yenye namba za usajili **T857DXD.** Chassis No. **KM700017630, Engine No. 7K0725392.** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/375788/2022**

---

## PASSPORT IMEPOTEA



**FESTO ANAM MWEMUTSI** anatangaza kupotelewa na **PASSPORT** yenye **No. TAE294656** Iliyotolewa **tarehe 02 FEB. 2020** na kuisha **tarehe 02 feb 2030.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/376960/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**DEOGRATIAS KULWA NCHEYE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA YA FAW ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T 271 BDX**
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**KAH /RB/ 625 /2022.**
NA GARI AINA YA **FAW** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 280 BDX**
TAARIFA YA POLISI
**KAH/RB/626/2022**

---


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## BURUDANI

# DIAMOND NAMBA 5 AFRIKA



**NEW YORK, Marekani**

MSANII wa bongofleva, Naseeb Abdul maarufu kwa jina la Diamond Platnumz anashika nafasi ya tano barani Afrika kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi kwenye mtandao wa Youtube.

Kwa mujibu wa Youtube, Diamond ana wafuasi milioni 7.1 katika mtandao huo.

Pia anashika nafasi ya kwanza kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Afrika Kusini.

Katia orodha hiyo, msanii, Mohamed Ramadan kutoka nchini Misri ana shika nafasi ya kwanza akiwa na wafuasi milioni 14.2 akifuatiwa na Saad Lamjarred wa Morocco ambaye ana wafuasi milioni 14.

Nafasi ya tatu inashikwa na Soolking kutoka Algeria ambaye anawafuasi milioni 9.5 huku namba nne yupo Tamer Hosny wa Misri mwenye wafuasi milioni 7.77.

Nafasi ya sita inashikiliwa na Zouhair Bahaoui wa Morocco mwenye wafuasi milioni 6.7 na namba saba imekamatwa na Balti kutoka nchini Tunisia mwenye wafuasi milioni 6.36.

# LULU HAMFUATILII KABISA MUMEWE

**DAR ES SALAAM, Tanzania**



NYOTA wa filamu nchini, Elizabeth Michael maarufu Lulu amesema hana muda wala tabia ya kumfuatilia mumewe kujua kama ana mwanamke mwingine.

Lulu amefunguka hivyo wakati akichati na mashabiki wake kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram.

Shabiki wake mmoja alimuuliza swali Lulu kama anamfuatilia mumewe baada ya habari ya majuzi kutoka nchini Nigeria kuripotiwa kwamba mwanamke mmoja alifariki kwenye ajali ya gari wakati akimkimbiza mume wake aliyekuwa na mchepuko kwenye gari jingine.

Lulu ambaye ni mke wa mfanyabiashara, Francis Ciza maarufu Majizzo alijibu hivi: "Watu wangu wa karibu wananijua, mimi mwenyewe kuna muda sijifuatilii. Na kutofuatilia sio kwamba hujali. Ni kuchagua kuwa upande chanya wa kuepeusha matatizo yasiyo na suluhu.

"Yani ukifuatilia hakikisha utakachokutana nacho unajua namna ya kutatua. La sivyo unakuwa umeongeza shida juu ya shida."



# DICAPRIO ATEMWA NA MCHUMBA WAKE

**LOS ANGELES, Marekani**

NYOTA wa filamu za Hollywood za Marekani, Leonardo DiCaprio amejikuta katika wakati mgumu baada ya kutemwa na mpenzi wake ambaye ni mwanamitindo, Camila Morrone.

Kwa mujibu wa mtandao wa habari za wasanii wakubwa wa Hollywood, TMZ.com, sababu ya DiCaprio kutemwa na mpenzi wake huyo ni kutaka kutulia naye na kuanzisha familia.

DiCaprio ambaye mtindo wake wa maisha kwa muda mrefu amekuwa akitoka na wasichana wasiozidi umri wa miaka 25 na alitaka kutulia na Camila ili waanzishe familia kwa sababu yeye hivi sasa anakaribia kufikisha umri wa miaka 50, akiwa na miaka 47.

Lakini baada ya Camila mwenye umri wa miaka 25 kugundua hilo, ripoti hiyo imethibitisha yeye ndiye aliamua kuvunja penzi hilo.

Sababu kubwa ni Camila hataki kufikiria kuhusu kuwa na familia kwa sababu bado anataka kutumia muda wake mwingi kwenye kazi yake ya uanamitindo.

Hata hivyo, wakati huo huo, DiCaprio tayari alikuwa anatoka na mwanamitindo mwingine Gigi Hadid, lakini uhusiano wao sio siriazi na pia anatajwa kutoka na binti wa mwanamuziki, Zayn Malik, wote wakiwa chini ya umri wa miaka 25.

# KOCHA AZAM ATOA NENO, WAKIJIPIMA NA MAZEMBE

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA wa zamani wa Afrika, TP Mazembe wanatarajia kuikaribisha Azam FC katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini Zambia.

TP Mazembe na Azam FC zinatumia mechi hiyo kujiandaa na michuano ya kimataifa na michezo ya ligi za nyumbani.

Kocha Mkuu wa Azam FC, Mfaransa Denis Lavagne, amesema mechi hiyo itakuwa kipimo sahihi kwa kikosi chake kuelekea katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo watacheza mwezi ujao.

Lavagne ambaye amejiunga na Azam hivi karibuni alisema ili kushiriki vizuri katika michuano ya CAF, uwe na kikosi imara kitakachoweza kutoa ushindani.

"Nadhani TP amzembe ni timu nzuri na katika kujiandaa na michuano ya Kombe la Shirikisho ni lazima ucheze na timu nzuri, ili wachezaji wawe na utimamu unaofanana na michuano yenyewe," alisema Lavagne.

**Kocha huyo alisema katika kipindi hiki cha mapumziko ya mechi za kimataifa si vizuri wachezaji kukaa bila kucheza.**

"Tuna wachezaji saba kwenye timu ya taifa, na tumebaki na wachezaji 20 tu, kwa hiyo tusingeweza kucheza mechi nyingi zaidi ya hii moja. Tutacheza mechi nyingi sana huko mbele, tuna mechi nane ndani ya mwezi mmoja ifikapo Oktoba.

Mechi moja ya kirafiki inatosha, na baada ya hapo kuna siku nyingine saba za kupumzika, nadhani zitatosha," alisema kocha huyo aliyechukua nafasi ya Abdihamid Moallin.

Aliongeza katika mechi hiyo atatumia fursa ya kuwapanga wachezaji ambao hawakupata nafasi ya kucheza dhidi ya Mbeya City iliyokuwa mechi yake ya kwanza akiwa anakiongoza kikosi hicho ili kuwafahamu vizuri.

Naye Msemaji wa Azam FC, Zakaria Thabiti (Zaka), alisema mechi hiyo ya kirafiki pia ni mwendelezo wa maandalizi kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons itakayochezwa Septemba 30, mwaka huu.

"Lengo kubwa la kwenda Zambia na kucheza mechi hiyo dhidi ya TP Mazembe ni kumpa nafasi ya kocha wetu (Lavagne) kuwatumia baadhi ya wachezaji ambao hajawaona na wala hawakucheza mechi mbili, tulivyocheza dhidi ya Yanga na Mbeya City,".

"Kocha Denis amekuja siku tunacheza na Yanga, mchezo uliofuata dhidi ya Mbeya City aliendelea kuwatumia wachezaji wale wale, ameomba hii mechi dhidi ya TP Mazembe kuwapa nafasi nyota ambao hawakucheza mechi hizo mbili," alisema Zaka.

TP Mazembe inajiandaa kuivaa Vipers ya Uganda katika mechi ya raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Azam yenyewe itakutana na Al Akhdar ya Libya kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (kushoto), akimkabidhi nahodha wa Timu ya Soka ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), Noela Luhala, mfano wa Bima itakayoisaidia timu hiyo pamoja na Tembo Warriors zinazotarajia kwenda kushiriki mashindano ya dunia. **PICHA: TFF**

# *Zimamoto yaipigia hesabu Jang'ombe*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Ali Hilali "Tedi" amesema bado anasaka ufumbuzi wa timu yake ambayo imeanza vibaya katika msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo inaendelea visiwani hapa.

Zimamoto inatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Amaan leo kuikabili Taifa Jang'ombe katika mechi ya raundi ya nne ya ligi hiyo ya juu Zanzibar ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Tedi alisema Ligi Kuu Zanzibar msimu huu imeanza kwa kasi kubwa na kila timu inayoshuka dimbani inahitaji kupata matokeo mazuri.

Kocha huyo alisema kikosi chake kilianza maandalizi ya msimu mapema mpaka bado anashindwa kufahamu tatizo linalowakwamisha wachezaji kutocheza vizuri.

"Natarajia kukutana na uongozi wa juu wa zimamoto SC kabla ya raundi ya nne haijaanza ili tujadili kwa pamoja na kuwapa hamasa wachezaji wafanye vizuri katika michezo yetu, naamini pengine wachezaji wana matatizo yao binafsi au kuna mambo mengine wakiambiwa wataweza kujituma," alisema Tedi.

Aliongeza viwango vya wachezaji wa Zanzibar vyote vinafanana hivyo haimanishi kufanya vibaya katika michezo ya ligi hiyo hadi sasa kumetokana na nyota wake kushuka viwango.

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunapata matokeo bora ili kujiweka sehemu salama katika msimamo wa ligi," aliongeza kocha huyo.

# Kiduku : Mkanda wa UBO utabakia Tanzania

**Na Saada Akida,** MTWARA

BONDIA Twaha Kiduku amesema anaamini pambano lake dhidi ya Abdo Khaled kutoka Misri litamfungulia njia ya kutambulika kimataifa huku akitimiza malengo yake ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Kiduku anatarajia kuvaana na Khaled katika pambano la kuwania mkanda wa ubingwa wa UBO wa uzito wa kilogramu 76 ambalo litakuwa la raundi 10 litakalofanyika kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani hapa.

Bondia huyo alisema amejiandaa vyema kuelekea pambano hilo kwa kutowaangusha Watanzania na wadau wa mchezo huo wanaomsapoti.

"Nimefanya maandalizi mazuri, nimemsoma mpinzani wangu na niko tayari kwa ajili ya pambano hilo, nitahakikisha nampiga mpinzani wangu," alisema Kiduku.

Mara ya mwisho Kiduku kupanda ulingoni ilikuwa ni dhidi ya Mkongomani Alex Kabangu katika pambano lililofanyika Machi 26, mwaka huu mkoani Morogoro ambapo mwenyeji huyo aliibuka mshindi.

Naye bondia Karim Mandonga ambaye amejipatia umaarufu mkubwa alisema amejiandaa vizuri kumchapa mpinzani wake, Salim Abeid kama vile amemwibia mke.

"Safari hii nimejiandaa vizuri sana, nimefanya maandalizi ya kutosha, Jumamosi nitampiga mpinzani wangu kama vile ameniibia mke, maana uchungu wa kuibiwa unauma," alisema Mandonga.

Mapambano mengine ya utangulizi yatakuwa ni kati ya bondia Nasra Msami dhidi ya Halima Bandora, Francis Miyeyusho atazichapa na Adam Lazoro huku Selema Galileo atavaana na Shabani Ndaro.

Wengine watakaopigana ni Alto Kyenga dhidi ya Ibrahim Tamba, Bosco Bakari atazichapa na Maliki Deo, Joseph Mchapeni atadundana na Pascal Manyota.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM AGEUKA LULU

KLABU ya Borussia Dortmund inamtathimini kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, ambaye pia anawindwa na Manchester United na Liverpool, kwa takriban pauni milioni 130. (***Athletic***)

### DE JONG ALIIKATAA UNITED

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, amesema "siku zote nilitaka kubakia Barcelona" baada ya kukataa uhamisho wa pauni milioni 65 kwenda Manchester United wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto. (***Mirror***)

### LOCATELLI ANUKIA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Juventus, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 24, amehusishwa na uhamisho wa Arsenal. Mtaliano huyo ameshindwa kumfurahisha Kocha, Massimiliano Allegri tangu alipohamia timu hiyo kwa ada ya pauni milioni 30 kutoka Sassuolo. (***Calciomercato via Sun***)

### ARSENAL YAMTAKA LINDSTROM

ARSENAL wamewasiliana na kiungo wa kati wa Eintracht Frankfurt, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 22, kuhusu uhamisho wa pauni milioni 17 kwa raia huyo wa Denmark, Januari. (***Bild***)

### FLAMENGO YAMZUIA GOMES

UONGOZI wa klabu ya Flamengo umesema "hakuna ofa" kwa Joao Gomes mwenye umri wa miaka, 21, huku kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil akihusishwa na Liverpool na Manchester United (***ESPN***)

### PEREIRA ALITAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United iliripotiwa imeonyesha nia ya kumtoa kiungo wa Ubelgiji, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 28, kama sehemu ya makubaliano ya kubadilishana na Joao Gomes msimu wa joto, kabla ya Pereira kujiunga na Fulham. (***Talksport***)

### KLABU ZILICHEMKA KWA GAKPO

HAKUNA klabu iliyofikia bei iliyotakiwa msimu wa joto kwa winga wa PSV Eindhoven ya Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, ambaye alihusishwa na kuhamia Manchester United, Southampton, Leeds United na Arsenal. (***Voetbal International via TalkSpor***t)

### ANDERSON APEWA MKATABA

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Elliot Anderson mwenye umri wa miaka 19, ametia saini mkataba mpya wa muda mrefu katika klabu hiyo. (***Chronicle***)

### KOCHA AIKATAA LEICESTER

KOCHA wa Celtic, Ange Postecoglou, amesema kuondoka na kwenda kuchukua mikoba ya Leicester City "haiko kwenye rada yangu". (***Sky Sports***)

### BUSQUETS KUMFUATA BECKHAM

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Hispania, Sergio Busquets mwenye umri wa miaka 34 yuko tayari kujiunga na Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Marekani ambayo mmoja wa wamiliki wake ni David Beckham. (***Spor***t)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE JONG: SIKUFIKIRIA KUONDOKA BARCELONA

## ●●● Nyota huyo aeleza hakuwa tayari kujiunga na United, Chelsea ambapo...

**BARCELONA,** Hispania

FRENKIE de Jong amethibitisha hakuwahi kufikiria kuondoka Barcelona wakati wa majira ya joto licha ya klabu hiyo kutaka kumuuza huku akitakiwa na Manchester United na Chelsea.

**Hali ya fedha ya Barcelona ilikuwa mbaya, huku klabu hiyo ya Katalunya ikilazimika kushusha mishahara ya wachezaji ili kusajili wachezaji wapya.**

De Jong alikuwa mmoja wa wachezaji ambao walikuwa wanapangwa kuuzwa, licha ya Kocha Mkuu, Xavi kushikilia yeye bado ni mchezaji 'muhimu'.

United ilikubaliana na Barcelana ada ya euro milioni 85 kumsajili, lakini mpango huo ulikwama kwa sababu mchezaji alikuwa anadai malimbikizo ya mishahara yake.

Viongozi wa Old Trafford bado walikuwa na uhakika wa kukamilisha uhamisho huo, lakini hawakufanikiwa na Chelsea pia waliingia kwenye mazungumzo na Barcelona na wakagonga mwamba.

Na sasa nyota huyo wa zamani wa Ajax ameeleza aliamua kubaki hao Camp Nou tangu Mei, mwaka huu.

"Nilijua nilichotaka, kubaki Barcelona," alisema akiiambia NOS.

"Klabu wakati mwingine huwa na mawazo yake kuhusu mambo na mimi pia. Wakati mwingine hiyo inagongana, lakini kwa ujumla ilikwenda sawa. Siku zote nilikuwa nikiweka wazi kile nilichotaka. Kulikuwa na kelele nyingi na mengi yalitokea. Kwa kweli imekuwa tofauti na madirisha mengine ya uhamisho kwangu.

"Manchester United na Chelsea? Mei nilikuwa tayari nimeamua ningeendelea na Barca. Sikuwahi kubadili mawazo yangu."

De Jong amekuwa ndani na nje ya kikosi cha kwanza cha Barcelona hadi sasa msimu huu. Ameshaingia akitokea benchi mara tano hadi sasa kwenye LaLiga, lakini ameanza katika mechi mbili za mwisho za klabu hiyo dhidi ya Cadiz na Elche.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,033,2

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 23 SEPTEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/22 | 20:30 | Bastia Borgo vs Le Mans | 2.78 | 3.13 | 2.46 |
| 02. 23/09/22 | 20:30 | Saint Brieuc vs Orleans | 2.48 | 3.15 | 2.75 |
| 03. 23/09/22 | 20:30 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 2.35 | 3.14 | 2.94 |
| 04. 23/09/22 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Avranches | 2.63 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 23/09/22 | 20:30 | FC Versailles 78 vs Nancy | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/09/22 | 20:30 | Sedan vs Le Puy | 2.34 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 23/09/22 | 21:00 | Ireland U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 23/09/22 | 21:45 | Italy vs England | 2.62 | 3.17 | 2.68 |
| 09. 23/09/22 | 21:45 | Finland vs Romania | 2.29 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 23/09/22 | 21:45 | Alloa Athletic vs Airdrieonians | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 11. 23/09/22 | 22:00 | Dordrecht vs Maastricht | 2.33 | 3.53 | 2.68 |
| 12. 23/09/22 | 22:00 | Morocco vs Chile | 2.70 | 3.27 | 2.60 |
| 13. 23/09/22 | 22:00 | The New Saints vs Dundee FC | 2.64 | 3.57 | 2.27 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa airtel money EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAYWEATHER, MCGREGOR SASA KURUDIANA MWAKANI

**AS VEGAS, Marekani**

BONDIA Floyd Mayweather amethibitisha pambano la marudiano na mpinzani wake, Conor McGregor liko mbioni na litafanyika mwakani.

Imepita takriban miaka mitano tangu Mayweather ampige nyota huyo McGregor kwa TKO raundi ya 10 mjini Las Vegas, katika pambano lililofanyika Agosti, 2017.

Mayweather ameiambia Sportsmail yuko katika mazungumzo ya mwisho na McGregor kuhusu masharti ya pambano hilo la marudiano na akafichua pambano hilo lilikuwa la malipo ya juu zaidi.

"Nataka kwenda huko wikendi hii katika pambano la Mikuru Asakura. Halafu nina pambano jingine Dubai ifikapo Novemba, mwaka huu. Mimi na Conor McGregor ni mwaka 2023.

"Kumekuwa na mazungumzo ya wote wawili. Naamini litakuwa na malipo ya aina yake."

Pambano la Mayweather na McGregor lilikuwa pambano lake la mwisho la kulipwa, na kufikisha rekodi yake ya kushinda mara 50 bila kupoteza wala sare.

Floyd aliingiza dola milioni 280 kutokana na pambano hilo lililozua kizaazaa.


Wakati McGregor alilipwa dola milioni 130 kwenye pambano lake la kwanza na la pekee la ndondi, kwani yeye anacheza zaidi mchezo wa ngumi na mateke (kickboxing).

# Modric hafikirii kustaafu Croatia

**MAKSIMIR, Croatia**

LUKA Modric amesema hafikirii kuhusu kustaafu kuichezea Timu ya Taifa ya Croatia kabla ya mchezo wa jana dhidi ya Denmark kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Mkongwe huyo wa Real Madrid anatazamia nahodha wa nchi yake hadi kwenye fainali za Kombe la Dunia la Qatar baadaye mwaka huu.



Miaka minne baada ya kutinga fainali kule Urusi, Modric ni miongoni mwa wachezaji wakongwe katika mchezo huo uwanjani, akiwa na umri wa miaka 37, huku wengi wakijiuliza iwapo michuano ya mwaka huu itakuwa ndio ya mwisho kwake kimataifa.

Lakini akizungumza kabla ya mechi yao ya Kundi A1 kwenye Uwanja wa Maksimir jana, mchezaji huyo amemwaga maji baridi juu ya uvumi wowote wa kustaafu.

"Sifikirii juu ya hilo," alisema Modric alisema. "Sijafanya uamuzi wowote.

"Nitajaribu kufanya uamuzi bora zaidi. Wakati huo, nitazungumza na kocha wetu mkuu, na watu ninaowaamini. Sifikirii hilo kwa sasa."

HABARI MICHEZO

283,276/-

# NMB MARATHON YAPATA WADHAMINI MBALIMBALI

Na Mwandishi Wetu

WIKI moja kabla ya kufanyika kwa mbio za hisani za NMB Marathon 'Mwendo wa Upendo', Benki ya NMB inayoandaa mbio hizo imetangaza wadhamini zaidi ya 20, ambao wameeleza siri ya uamuzi wa kukubali kudhamini imetokana na kuguswa na wazo chanya la kuwakomboa wanawake hapa nchini.

NMB Marathon 2022, zinazolenga kukusanya Sh. milioni 600 ili kusaidia matibabu ya wanawake wenye tatizo la Fistula wanaotibiwa katika Hospitali ya CCBRT, zitafanyika Oktoba Mosi, mwaka huu kwenye viwanja vya Leaders Club, Dar es Salaam na mgeni rasmi atakuwa ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, aliwashukuru wadhamini hao kwa kusapoti mbio hizo na kurahisisha lengo lengo la kukusanya kiasi hicho cha fedha, hivyo kutoa nafasi mapato ya mia-ka miwili ijayo ya mbio hizo yataelekeza katika maeneo mengine yenye uhitaji.

"Mwaka jana wakati tukizindua NMB Marathon tuliweka lengo la kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne, mwitikio mkubwa ukatuwezesha kukusanya Sh. milioni 400 badala ya 250 tulizotarajia. Ndipo tulipoona umuhimu wa kupata Sh. milioni 600 mwaka huu, ili kukamilisha bilioni moja.

"Tunawashukuru wadhamini wetu waliogawanyika katika kategori zaidi ya tano, zikiwamo za Executive, Gold, Bronze na Media Partner kwa kujitokeza kutusapoti kama tulivyowaomba wakati tukizindua mbio hizi mwaka huu, na kutoa michango yao katika kufanikisha mchakato huu wa kusaidia kinamama wetu," alisema Kimori.




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori (katikati), akitambulisha wadhamini wa NMB Marathon 2022 zitakazofanyika Oktoba Mosi, mwaka huu kwenye viwanja vya Leaders, Dar es Salaam. Kulia ni Mkuu wa Biashara Maendeleo na Masoko wa Kampuni ya Bima ya UAP, Mariam Hussein na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam Life Insurance Tanzania, Julius Magabe. **PICHA: FATUMA ATHUMANI, TUDARco**

Aliwataja wadhamini wakuu ni Sanlam Life Insurance na UAP Insurance (Executive), huku Jubilee General Insurance (ikiwa kategori ya Gold) na walioko Kundi la Bronze ni Alliance Life Assurance, Britam Insurance Tanzania, Reliance Insurance na ARiS Risk and Insurance Solutions.

Wengine wa kundi hilo ni Jubilee Life Insurance na Metropolitan Life Insurance, huku Toyota, TBL, Strategis, Serena Hotel, Azam, na Johari Rotana Hotel wakiwa ni miongoni mwa wadhamini wengineo.

Katika kategori ya vyombo vya habari washirika, Kimori aliitaja EFM Radio, TV E, Mwananchi Communications Limited, IPP Media na Almasi Productions, orodha iliyokamilishwa na Kampuni za SGA Security Tanzania, Gelato na Grano Coffee.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam, Julius Magabe, aliishukuru NMB kwa kuwashirikisha katika suala hilo la tiba kwa kinamama wenye fistula na kwao hiyo ni nafasi muhimu na adhimu ya kusapoti wanawake, huku akieleza watakuwa bega kwa bega na NMB katika jambo lolote la kijamii.

Naye Mariam Hussein, ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mauzo wa Kampuni ya Bima ya UAP, alisema amani na kuboresha maisha ya kila mtu ni kati ya vipaumbele vya UAP na hiyo ndio siri ya uharaka wao katika kudhamini NMB Marathon, ambayo hawataishia kudhamini tu, bali watakimbia mbio hizo.

# Simba yawaendea Waangola Zanzibar

INATOKA UK. 32

kikosi chake tangu alipojiunga na timu hiyo.

"Kama utakumbuka wakati Mgunda anakuja Simba kesho yake tu alipanda ndege na timu kuelekea Malawi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Nyasa Big Bullets na tuliporejea hapo tulikwenda Mbeya kucheza na Prisons, na kabla hajakaa vizuri tukawa na mechi ya marudiano dhidi ya Nyasa Big Bullets. Amefurahi sana, hizi siku za mapumziko ya mechi za ligi zitampa muda zaidi wa kuongezea ufundi mwingine ambao bado hajautoa," Ahmed alisema.

Aliongeza hali za wachezaji, Gadiel Michael aliyeumia kwenye mechi za kimataifa za kirafiki nchini Sudan dhidi ya Al Hilal na Shomari Kapombe, zinaendelea vyema.

# MAYELE AFUNGUKA

INATOKA UK. 32

na mazoezi ya uwanjani kwa ajili ya kuiweka sawa miili ya wachezaji wao na kuwa tayari kwa ushindani katika mechi zinazofuata.

Alisema, wanaupa umuhimu mchezo huo kwa sababu anafahamu hawawezi kushiriki tena mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao bila kubeba ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunaupa umuhimu mkubwa mchezo huo ili malengo yatimie, kuendelea kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu ni sehemu ya malengo tuliyojiwekea. Tunahitaji kulitetea kombe letu, ingawa tunafahamu ligi ni ngumu," aliongeza kocha huyo.

Alisema, hali ya ushindani wa namba kwenye kikosi hicho unaongezeka kwa sababu wachezaji wanahitaji kujitangaza na vilevile, kuitwa katika timu za mataifa wanayotoka.

Yanga yenye pointi 10 sawa na Simba ndio inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ya FIFA.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo***



## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 24/09/22 | 17:00 | Morecambe vs Cambridge Utd | 2.85 | 3.30 | 2.44 |
| 02. 24/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Charlton | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 24/09/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Accrington | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 04. 24/09/22 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 05. 24/09/22 | 17:00 | Hartlepool vs Gillingham | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 06. 24/09/22 | 17:00 | Sutton United vs Salford City | 2.42 | 3.28 | 2.88 |
| 07. 24/09/22 | 17:15 | Mirandes vs Zaragoza | 2.98 | 3.18 | 2.41 |
| 08. 24/09/22 | 19:00 | Sarmiento vs Arsenal Sarandi | 2.36 | 3.14 | 3.24 |
| 09. 24/09/22 | 19:30 | Malaga vs Villarreal B | 2.31 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 24/09/22 | 19:30 | Ponferradina vs Tenerife | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 11. 24/09/22 | 21:30 | Lanus vs San Lorenzo | 2.49 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 24/09/22 | 21:45 | Israel vs Albania | 2.41 | 3.18 | 3.08 |
| 13. 24/09/22 | 22:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.36 | 3.12 | 3.07 |
| 14. 25/09/22 | 04:00 | Mexico vs Peru | 2.29 | 3.21 | 3.21 |
| 15. 25/09/226 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.77 | 3.88 | 2.30 |
| 16. 25/09/22 | 15:00 | Burgos vs Levante | 3.39 | 3.04 | 2.26 |
| 17. 25/09/22 | 17:15 | Lugo vs Real Oviedo | 3.24 | 2.99 | 2.37 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 23/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5512 | South Korea vs Costa Rica | 1.58 | 3.86 | 5.89 |
| 15:00 | 2728 | Hull City U23 vs Birmingham U23 | 2.44 | 3.83 | 2.33 |
| 15:25 | 2219 | Japan vs USA | 2.54 | 3.22 | 2.81 |
| 18:00 | 2888 | USM Annaba vs USM EL Harrach | 2.85 | 2.60 | 2.75 |
| 18:00 | 3881 | JSM Skikda vs JS Bordj Menaiel | 4.23 | 3.05 | 1.87 |
| 18:30 | 4518 | FC KTP vs KPV Kokkola | 1.40 | 4.51 | 6.08 |
| 19:00 | 2009 | Iceland U21 vs Czech Republic U21 | 2.80 | 3.15 | 2.35 |
| 19:00 | 2176 | Slovakia U21 vs Ukraine U21 | 2.39 | 3.14 | 2.75 |
| 19:00 | 2696 | Iran vs Uruguay | 3.77 | 3.52 | 1.96 |
| 19:00 | 4179 | Georgia vs North Macedonia | 2.11 | 3.28 | 3.43 |
| 19:00 | 4332 | Estonia vs Malta | 1.87 | 3.27 | 4.33 |
| 19:00 | 4478 | Croatia U21 vs Denmark U21 | 2.39 | 3.15 | 2.75 |
| 20:00 | 2924 | Canada vs Qatar | 2.10 | 3.51 | 3.36 |
| 20:00 | 4146 | Paraguay vs United Arab Emirates | 1.68 | 3.77 | 4.99 |
| 20:30 | 1349 | Red Star vs FC Martigues | 1.93 | 3.34 | 3.73 |
| 20:30 | 2566 | Bastia Borgo vs Le Mans | 2.79 | 3.18 | 2.43 |
| 20:30 | 3071 | FC Versailles 78 vs Nancy | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 20:30 | 3165 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 2.35 | 3.14 | 2.94 |
| 20:30 | 3668 | Sedan vs Le Puy | 2.42 | 3.13 | 2.83 |
| 20:30 | 4412 | Saint Brieuc vs Orleans | 2.48 | 3.15 | 2.75 |
| 20:30 | 5334 | Paris 13 Atletico vs Avranches | 2.36 | 3.13 | 2.93 |
| 20:30 | 5354 | Cholet vs Concarneau | 3.63 | 3.28 | 1.98 |
| 21:00 | 3533 | Ireland U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.06 | 3.01 |
| 21:00 | 3680 | Ecuador vs Saudi Arabia | 1.91 | 3.36 | 4.17 |
| 21:30 | 5324 | Brazil vs Ghana | 1.20 | 6.32 | 14.27 |
| 21:45 | 2416 | Glenavon vs Glentoran Belfast | 3.38 | 3.53 | 1.92 |
| 21:45 | 3766 | Italy vs England | 2.67 | 3.11 | 2.68 |
| 21:45 | 3914 | Penybont vs Aberystwyth Town | 1.50 | 4.11 | 5.29 |
| 21:45 | 4127 | Bulgaria vs Gibraltar | 1.10 | 8.67 | 22.19 |
| 21:45 | 4309 | Falkirk FC vs Partick Thisle | 3.82 | 3.82 | 1.73 |
| 21:45 | 4562 | Carrick Rangers vs Larne | 4.13 | 4.03 | 1.64 |
| 21:45 | 4594 | Dungannon Swifts vs Portadown FC | 1.85 | 3.57 | 3.57 |
| 21:45 | 4875 | Coleraine FC vs Newry City AFC | 1.50 | 4.22 | 5.10 |
| 21:45 | 5215 | Crusaders Belfast vs Ballymena Utd | 1.47 | 4.33 | 5.32 |
| 21:45 | 5466 | Airbus UK Broughton vs Newtown AFC | 4.21 | 3.87 | 1.66 |
| 21:45 | 5861 | Finland vs Romania | 2.29 | 3.24 | 3.09 |
| 21:45 | 5883 | Alloa Athletic vs Airdrieonians | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 21:45 | 5890 | Annan Athletic vs Kelty Hearts FC | 3.05 | 3.64 | 2.01 |
| 21:45 | 5892 | Germany vs Hungary | 1.30 | 5.18 | 9.26 |
| 21:45 | 5911 | Bosnia and Herzegovina vs Montenegro | 1.74 | 3.52 | 4.73 |
| 22:00 | 1069 | Dordrecht vs Maastricht | 2.21 | 3.58 | 2.83 |
| 22:00 | 3026 | The New Saints vs Dundee FC | 2.64 | 3.57 | 2.27 |
| 22:00 | 3072 | Morocco vs Chile | 2.66 | 3.12 | 2.76 |
| 22:00 | 3388 | Algeria vs Guinea | 1.64 | 3.81 | 5.28 |
| 22:00 | 3809 | FC Oss vs Willem II Tilburg | 4.16 | 3.82 | 1.72 |
| 22:00 | 3903 | Heracles Almelo vs Helmond Sport | 1.34 | 4.98 | 7.16 |
| 22:00 | 4818 | VVV Venlo vs Telstar | 2.08 | 3.53 | 3.13 |
| 22:00 | 5805 | Sporting Gijon vs UD Ibiza Eivissa | 1.80 | 3.30 | 4.50 |
| 23:00 | 1339 | FC Aguablanca vs Deportes Quindio | 2.78 | 2.78 | 2.63 |
| 23:00 | 2706 | Bogota FC vs Orsomarso | 1.62 | 3.90 | 5.80 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 23, 2022
Nipashe

UKURASA 30



## Mayweather, McGregor sasa kurudiana mwakani



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Uganda itakayochezwa kesho nchini Libya. Stars itashuka tena dimbani Septemba 27, kuwakabili wenyeji katika mchezo mwingine wa kirafiki ulioko kwenye kalenda ya FIFA. **PICHA: TFF**

# Mayele afunguka watasonga mbele

## ●●●Mkongomani huyo aeleza namna Yanga itakavyowamaliza Al Hilal na...

**Na Waandishi Wetu**

STRAIKA namba moja wa Yanga, Fiston Mayele, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuelekea katika mechi ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan.

Yanga ilisonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kuiondoa Zalan FC ya Sudan Kusini kwa kichapo cha jumla cha mabao 9-0.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajia kuikaribisha Al Hilal kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya Oktoba 7 na 9, mwaka huu na kurudiana baada ya wiki moja huko Khartoum.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Mayele, alisema yeye na wachezaji wenzake hawana wasiwasi wala hofu kuelekea mchezo huo hasa watakapokuwa ugenini kukamilisha hatua hiyo.

Mayele alisema, wachezaji wa Yanga wameshapata uzoefu na kwao hawana presha ya kucheza kwenye viwanja vinavyojaza idadi kubwa ya mashabiki kama huko Sudan watakapokwenda.

Mkongomani huyo alisema, hata namna wapinzani wao walivyoshangilia wakati wanacheza dhidi ya St. George ya Ethiopia, hawajaingiwa na wasiwasi kwa sababu ni matukio ya kawaida kwenye mchezo huo wa soka hasa mwenyeji anapohitaji kulinda ushindi.

"Sisi kama wachezaji hatuna presha, Yanga hii ina wachezaji wakubwa sana ambao wameshacheza kwenye viwanja vya ugenini vilivyojaa na vyenye mashabiki wanaoshangilia mwanzo hadi mwisho. Kuna Shaaban Djuma, Yanick Bangala, Bernard Morrison, Stephane Aziz Ki na mimi (Mayele), wote sisi ni wachezaji wazoefu ambao hatutishiki sana na umati ule wa mashabiki kwa sababu tumeshacheza sana mechi za aina ile," alisema Mayele.

Nyota huyo aliongeza binafsi wakati akiwa na AS Vita Club alishawahi kucheza kwenye viwanja wa timu za Afrika Kaskazini, hivyo hana hofu na mechi dhidi ya Al Hilal hasa itakayochezwa ugenini jijini Khartoum.

"Mwaka wa kwanza kucheza nilikuwa na AS Vita na tulicheza dhidi ya JS Kabliye ya Algeria, halafu tukacheza na Raja Casablanca ya Morocco, ule uwanja ulijaa sana na walikuwa wanashangilia sana, kwa hiyo mashabiki wa Al Hilal hawawezi kutupa shida. Tutajitahidi tupate ushindi mkubwa hapa, ili iturahisishie kazi tutakapokwenda ugenini," Mayele alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga jana kiliendelea ma mazoezi yake kwenye ufukwe wa Coco kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Oktoba 3, mwaka huu.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze, aliliambia gazeti hili baada ya kumalizika kwa mazoezi wachezaji wake wote waliobakia kikosini wameshiriki programu iliyoandaliwa kikamilifu.

"Baada ya kumaliza mchezo wetu wa kimataifa, tuliwapa mapumziko mafupi wachezaji wetu jana (juzi) walifanya mazoezi ya Gym na leo (jana) wamefanya mazoezi ya ufukweni," alisema Kaze.

Kocha huyo, alisema leo wataendelea

INAENDELEA UK. 31

## Simba yawaendea Waangola Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha Simba kinatarajiwa kuwasili Visiwani hapa leo kwa ajili ya kucheza mechi mbili za kirafiki kwa lengo la kujiimarisha kuelekea mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

Simba inatarajia kucheza mechi yake ya kwanza ya kirafiki dhidi ya Wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi SC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar hapo keshokutwa na mchezo wa pili utafanyika Septemba 27, mwaka huu dhidi ya wawakilishi pekee wa Zanzibar waliobakia kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kipanga FC.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema tayari wameshapokea barua ya kukubali na timu hiyo kutua visiwani hapo na kucheza michezo miwili ya kirafiki.

Vuai alisema, Simba inauzoefu mkubwa katika mashindano ya kimataifa hivyo matarajio ya ZFF ni kuona mchezo huo utawasaidia pia Kipanga inayojiandaa kuwakabili Club Africain ya Tunisia na Malindi iliyoanza vyema msimu huu.

"Kwa upande wa Malindi timu hiyo imeanza vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar, mechi hii itasaidia kurejesha hamasa kwa mashabiki wao, timu (Simba) hiyo imekuja Zanzibar kwa mwaliko wa ZFF wenye lengo la kuzipa hamasa na uzoefu timu zake zinazocheza Ligi Kuu, ambapo kwa upande wa Kipanga inakabiliwa na mechi ya mashindano ya kimataifa, lakini timu hizo zilikuwa na ushindani zilipokutana zinakutana miaka ya nyuma timu katika Ligi ya Muungano," alisema Vuai.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamefurahi kupata mwaliko huo ambao utazisaidia timu zote mbili kiufundi na kuimarisha mahusiano.

"Mazoezi yameshaanza kwenye Uwanja wa Mo Arena, lakini kesho (leo) tunatarajia kwenda Zanzibar kwa mwaliko wa Chama cha Soka Zanzibar, Jumamosi tunatarajia kucheza dhidi ya Kipanga, na Jumatatu pia tutacheza dhidi ya Malindi, zote hizo zitachezwa kuanzia saa 1:00 usiku," alisema Ahmed.

Aliongeza mechi hizo za kirafiki zitampa nafasi ambayo hajawahi kuipata Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda ya kukitazama vyema

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >